# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TISA

### Kikao cha Saba – Tarehe 15 Novemba, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa mwaka 2017 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (Na.4) Bill, 2017).*

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA):**

Maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa mwaka 2017 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2017).*

**MHE. ABDALLAH A. MTULIA (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA):**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Musdwada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa mwaka 2017 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2017).*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 82

### Kuwezesha Vijana Wajasiriamali – Singida

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE** aliuliza:-

Vijana wengi wa Mkoa wa Singida wamejikita katika shughuli za ujasiriamali ili kuondokana na umaskini, lakini wanakosa mbinu za kitaalam za kuwawezesha kupiga hatua kubwa kimaendeleo kupitia kazi wanazofanya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia mbinu endelevu, zana za kisasa pamoja na mitaji ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwapatia vijana wa Singida mbinu endelevu na zana za kisasa pamoja na mitaji

ya kufanyia kazi kwa ufanisi, Serikali inaendelea kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Kukuza Ujuzi Nchini ambayo imelenga kutoa mafunzo ya ujuzi kwa vijana katika fani mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujasiriamali. Hadi kufikia mwezi Oktoba jumla ya vijana 11,340 wamepatiwa mafunzo ya ujuzi wa fani mbalimbali na wengine wanaendelea na mafunzo ya kujenga ujuzi kutoka katika mikoayote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano dhahiri wa mafunzo ya kukuza ujuzi ni pamoja na utumiaji wa teknolojia ya kitalu nyumba *(green house)* ili kuwawezesha vijana wetu kufanya kilimo kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuongeza tija ya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa mikoa yote kushiriki katika program hii, mikoa ilielekezwa kutenga eneo la kujenga *green house* ya kufundishia; kutenga maeneo ya kilimo kwa vijana pamoja na kuweka miundombinu muhimu na upatikanaji wa maji; kuandaa vijana wenye nia ya kujifunza kilimo kwa kutumia teknolojia ya *green house.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote Wizara yangu imeendelea kusimamia Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa vijana wote wa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aysharose swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vijana ndiyo kundi muhimu katika kujenga uchumi wa Taifa letu, je, Serikali ina mpango ganiwa kuwapatia vijana nchini wakiwemo wa Mkoa wa Singida vitendea kazi na mikopo yenye riba nafuu ili kuwawezesha kujikita katika shughuli za ujasiriamali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Serikali ina Maafisa Maendeleo vijana kote nchini lakini maafisa hawa hawana vitendea kazi kuweza kuwafikia vijana wengi walioko vijijini. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha Maafisa vijana hawa ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Aysharose kwa kazi nzuri anayoifanya ya kutetea maendeleo ya vijana katika Mkoa wa Singida na mimi binafsi nimeshuhudia kwa sababu alishanialika kuwa mgeni rasmi kwenye mafunzo ya stadi za maisha kwa vijana wa Mkoa wa Singida. Naomba aendelee hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi hatuna shida ya kuwasaidia vijana wetu vitendea kazi na mikopo na Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu ni ofisi ambayo inasimamia suala zima la uwezeshaji wananchi kiuchumi, kama nilivyosema tunayo mifuko 16 ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Mbunge awasiliane na mimi, tutaendelea kumuelekeza jinsi ya kufanya pamoja na kutumia mfuko wa maendeleo ya vijana kutoka katika Halmashauri zinazohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua ni kwa kiasi gani tutawasaidia Maafisa Vijana na Maafisa Maendeleo ya Jamii kuweza kusimamia shughuli za maendeleo ya vijana. Ni hivi juzi tu Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI alinialika na tulianza kikao cha kwanza cha kuwapa nguvu na kuwajengea uwezo Maafisa Maendeleo ya Jamii nchi nzima. Tutaendelea kufanya hivyo kwa Maafisa Vijana pia katika nchi nzima ya Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Tunaendelea na Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mbunge wa Nyamagana sasa aulize swali lake.

Na. 83

**Ahadi ya *X-ray* Hospitali ya Wilaya Nyamagana**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Rais wa Awamu ya Nne alipofanya ziara katika Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana mwaka 2014 aliahidi kupatia *x-ray.*

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo ya Rais hasa ikizingatiwa kuwa hospitali hiyo kwa sasa haina kifaa hata kimoja katika kitengo cha mionzi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ahadi hiyo ilitolewa na Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Awamu ya Nne mwaka 2014 wakati wa ufunguzi wa jengo la upasuaji katika Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana. Katika mwaka wa fedha 2017/ 2018, Serikali imetenga jumla ya shilingi 133,136,000 kwa ajili ya kununua mashine ya *x-ray* mpya ikiwa ni utekelezaji wa ahadi hiy iliyotolewa na Mheshimiwa Rais inayolenga kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kulichukulia kwa uzito suala hili na

kutenga fedha hiyo. Imani yangu ni kwamba kifaa hiki kitakamilika na kitafika kwa wakati kwenye Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana. Sasa naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana inao ujenzi wa jengo kubwa lenye ghorofa mbili kwa ajili ya wodi ya wanaume. Nataka *commitment* ya Serikali, je, watakuwa tayari baada tu ya jengo hili kukamilika mapema mwakani mwezi wa tatu kutusaidia kwa ajili ya kupata vitanda na vifaa tiba vingine ili kutoa huduma iliyo bora kuendana na kasi ya Awamu ya Tano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Wilaya ya Ilemela haina Hospitali ya Wilaya ya Ilemela lakini ni wilaya mpya na ujenzi wa hospitali yake umeanza kwa kusuasua sana. kwenye bajeti ya shilingi bilioni nne sasa hivi imeshapata milioni 500 peke yake. Nataka kujua je, Serikali itakuwa tayari kuhakikisha fedha zipatikane na kwenda kukamilisha ujenzi wa hospitali hii ya Wilaya kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Ilemela?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na upatikanaji wa vifaa ni dhahiri kwamba Serikali ina nia ya dhatikuhakikisha kwamba vifaa vinapatikana ili hospitali hiyo iweze kufanya kazi iliyotarajiwa na hivi sasa ninavyoongea tayari vitanda 25 vimeshapelekwa Nyamagana pamoja na magodoro yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba hospitali zote za Wilaya zinafanya kazi kwa kiwango cha hali ya juu kabisa. Tutakuwa tayari mara hospitali hii itakavyokuwa imekamilika tuhakikishe vifaa vyote vinapelekwa ili iweze kufanya kazi kwa ajili ya kusaidia Watanzania wa Nyamagana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto nyingi sana za Mikoa mipya na Wilaya mpya ambazo nyingi hazina Hospitali za Wilaya. Nini kauli ya Serikali ikiwemo wilaya ya kwangu ya Tanganyika ambayo haina Hospitali ya Wilaya. Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo la ukosefu wa Hospitali za Wilaya katika maeneo yote nchini ambayo hayana Hospitali za Wilaya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, swali very *general.* Jaribu kulijibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba afya kwa wananchi wa Tanzania kama ilivyo kipaumbele na ndiyo maana bajeti imeongezeka kutoka shilingi bilioni 31 mpaka shilingi bilioni 269. Hii inaonesha jinsi ambavyo Serikali itahakikisha kwamba huduma hii inawafikia wananchi na kwa kuwepo Hospitali za Wilaya maeneo yote ambayo Hospitali za Wilaya hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizitake halmashauri zote zianze kwa kutenga maeneo lakini pia kwa kutumia *own source* na wao waanza ili Serikali iweze kuunga mkono jitihada hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mollel swali la nyongeza.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niuliza kwamba Wilaya ya Siha inafanana sana na Nyamagana tuna hospitali mpya ya Wilaya ambayo Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Jafo alikuja akashirikiana na sisi kufanya kazi nzuri ya kuhakikisha hospitali hiyo inaweza

kulaza na kufanya upasuaji. Lakini sasa tuna changamoto, pamoja na vifaa lakini tuna upungufu wa asilimia 74 ya watumishi. Je, Waziri atakuwa tayari tukae na yeye kujadili kwa namna ya dharura namna ya kusaidia hospitali hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, swali zuri naamini Waziri atakubali tu. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mollel kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilifika Siha na ni kweli hata takriban wiki moja na nusu nilikuwa naongea na Mkuu wa Wilaya yako ya Siha na bahati nzuri katika kazi kubwa tunayoenda kuifanya katika umaliziaji wa hospitali tatu za awali ikiwepo Mvomero na Hospitali ya Siha na maeneo mengine tunaenda kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hilo hata bila kukaa tumeshalimaliza tayari kwa ajili ya maslahi mapana ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafo. Tunaendelea na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 84

**Ahadi ya Kuondoa Ushuru na Kodi Kero Kwa Wajasiriamali Nchini**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Wakati Rais akiwa katika kampeni aliahidi kuwa ataondoa ushuru na kodi ndogo ndogo zinazoleta usumbufu kwa wajasiriamali wadogo wadogo kama vile machinga, wachuuzi wa mboga mboga na matunda, mama lishe,

waendesha bodaboda na kadhalika, lakini mpaka sasa ahadi hiyo haijatekelezwa.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya uamuzi wa kufuta ushuru unaotozwa kwa wafanyabiashara ndogo ndogo wasio rasmi na wanaofanyia biashara katika maeneo yasiyo rasmi wakiwemo mama lishe, wauzaji mitumba wadogo, wauza mboga mboga, ndizi na matunda. Vile vile, wafanyabiashara walio nje ya maeneo maalum ya kibiashara wenye mitaji chini ya shilingi 100,000 hawaruhusiwi kulipa ada, tozo na kodi za aina yoyote.

Mheshimiwa MWenyekiti, uamuzi huu umeanza kutekelezwa kuanzia tarehe 1 Julai 2017 baada ya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 iliyotangaza kufuta ushuru na kodi kero kwa wafanyabiashara wadogo wadogo. Hatua inayoendelea sasa hivi nikuwatambua wafanyabiashara wadogo wote ili kuwapatia vitambulisho maalum vya kazi wanazozifanya. Hivyo, Serikali imetekeleza kwa vitendo ahadi hii iliyoko katika Ilani ya Chama Tawala ya mwaka 2015 inayolenga kuwapatia unafuu wa maisha wananchi wa hali ya chini kiuchumi ili waweze kukua na kuchangia vizuri katika uchumi wa Taifa lao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kw amajibu mazuri. Pamoja na majibu

mazuri hayo napenda kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji huu bado kuna maeneo mbalimbali katika Halmashauri mbalimbali katika Mkoa wangu wa Ruvuma na maeneo mengine kwenye Halmashauri nyingine maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kuwachukulia hatua kali halmashauri ambazo bado wanawanyonya kwa kuwatoza ushuru wajasiriamali wadogo wadogo wote katika Halmashauri zote zilizoko mkoani Ruvuma na maeneo mengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa wafanyabiashara hao wadogo wadogo wanafanya biashara katika mazingira magumu sana jua la kwao, mvua ya kwao, vumbi lao. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawekea mazingira bora ili wamachinga hao waweze kuepuka adha hiyo wanayoipata? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote ni mashuhuda kwamba, Sheria hii ilipitishwa na Bunge lako Tukufu na kwa vyovyote vile hakuna kisingizio chochote ambacho kinaweza kikatolewa na halmashauri eti kwa sababu, wakidhani kwamba, sheria ndogo ambazo wao hawajazipitisha zinakuwa zinakinzana kwamba hazitawaletea mapato. Naomba niwasihi Wakurugenzi wote Halmashauri zote, na jambo hili hata Mheshimiwa Rais amekuwa akilirudia, naomba niliseme kwa mara ya mwisho; Mkurugenzi yeyote wa halmashauri iwayo yoyote ambaye atapingana na maelekezo haya na sheria aambayo imetungwa na Bunge lako Tukufu, sisi kama Serikali hatutasita kumchukulia hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anaulizia namna ya kuwawekea mazingira mazuri wafanyabiashara wadogo wadogo. Ni dhamira ya Serikali na ndio maana tunaanza kwa kuwatambua kwa kuwapa vitambulisho ili tuhakikishe kwamba, wanatengewa maeneo mazuri ili wafanye kazi katika mazingira yaliyo mazuri kwa ajili ya kuongeza kipato cha nchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Pamoja na majibu yanayoridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi nilikuwa tu nataka niweke msisitizo kwenye hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, Mheshimiwa Rais amekuwa akirudia na wewe leo hapo umejaribu kuweka msisitizo, lakini bado kuna shida kule chini kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kukataa hili agizo kwa maana *circular* bado haijafika.

Sasa nataka nijue tu kabisa kwamba, je, *circular* hiyo inahusu ile mizigo ya wakulima ama wananchi wa kawaida wenye chini ya tani moja, kama Rais alivyoagiza kwamba ukisafirisha mzigo kutoka eneo moja kwenda lingine, chini ya tani moja hutakiwi kulipa ushuru; kwa hiyo, nilitaka nijue kama *circular* na yenyewe inazungumzia hivyo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetangulia katika jibu langu la msingi kwamba tozo hizi ziliondolewa ndani ya Bunge lako Tukufu na ndani ya Bunge hili tulisema ni tozo zipi ambazo zinafutwa kwa sababu ni kodi kero. Hakuna *by-law* yoyote kwenye halmashauri ambayo inazidi Sheria ambayo inatungwa na Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, nazidi kuomba na nawasihi wakurugenzi wote hawana *option* nyingine zaidi

ya kutekeleza Sheria ambayo imepitishwa na Bunge lako Tukufu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Obama swali la nyongeza.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Bunge lililopita tulitunga sheria ya kufuta *hotel levy,* lakini katika Mkoa wa Dar-es-Salaam *hotel levy* imeendelea kutozwa. Na Mheshimiwa Waziri anakiri na kusema kwamba, Sheria za Bunge zinazotungwa ziheshimiwe. Nini kauli ya Waziri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ile Sheria ya *Hotel Levy* inajieleza, ukiisoma vizuri kuna *definition* ya hoteli, inatakiwa iwe na sifa ipi ili ikidhi kuwa hoteli. Sasa kumekuwa na mchanganyiko kati ya hoteli na *guest house.* Ukiisoma Sheria ya *Hotel Levy* inaelekeza wale ambao ni *VAT registered* hawatakiwi kutoa *hotel levy,* lakini wale ambao wako chini ya Halmashauri bado sheria imesimama. Kwa hiyo, ni suala tu la kusoma sheria vizuri na kuitafsiri vile inavyotakiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa napenda tu kutoa msisitizo kuhusiana na masuala yale ya kutoza ushuru. Nilikuwa naomba Halmashauri kwa uwa, zenyewe ndio zinazoweka maeneo ya vizuizi na kukagua juu ya masuala ya kutoza ushuru ni vema sasa kuwe na mizani ambayo itawezesha hawa wananchi kuona kwamba mzigo wao una hiyo tani moja iliyoruhusiwa au la. Kinyume na hapo kwa kuangalia tu magunia kwa upande mmoja inakuwa inawafanya aidha wananchi wananyanyasika au wenyewe Halmashauri kutokupata ushuru ulio sahihi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa tunaebdelea na Mheshimiwa Lameck Okambo, Mbunge wa Rorya, swali lake linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mwita.

Na. 85

**Ahadi ya Ujenzi wa Daraja la Mto Mori – Rorya**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE (K.n.y. MHE. LAMECK O. AIRO)** Aliuliza:-

Wakati Rais akiwa kwenye ziara Wilayani Rorya aliahidi ujenzi wa Daraja la Mto Mori linalounganisha Tarafa ya Suba Luoimbo na Nyancha, lakini kwenye bajeti ya mwaka 2016/ 2017 ujenzi wa daraja hilo haukuwepo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga daraja hilo ili kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mto Mori unapita katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime na Rorya hali inayosababisha kuwepo kwa uhitaji wa madaraja mawili ili kurahisisha usafiri katika maeneo hayo mawili. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kupitia Mfuko wa Barabara imetengewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Mto Mori kwa upande wa Tarime. Taratibu za manunuzi zinaendelea, ili kumpata mkandarasi wa kujenga daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Rorya usanifu wa awali umefanyika ili kujua gharama za ujenzi wa

daraja hilo ambazo zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 300. Halmashauri ya Wilaya ya Rorya imepanga kuweka kipaumbele na kutenga fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 ili kukamilisha ujenzi huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, wakati fulani ni vizuri haya majibu nayo tukawa tunayaona vizuri kwa sababu, Mheshimiwa Mbunge anauliza Daraja la Mto Mori, Rorya. Majibu ya matumaini yanakuja Daraja la Mto Mori, Tarime inakuwa inapoteza ile ladha ya swali na hasa mtu anapokuwa ameuliza swali kwa muda mrefu katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kujua Halmashauri hazina uwezo wa kujenga hili daraja ndio maana zimeomba Serikali Kuu isaidie kwa maana ya TAMISEMI. Ni lini sasa Serikali Kuu itatoa fedha za kusaidia daraja hilo kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Rorya uchumi wake ni mdogo haiwezi kujenga hilo daraja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Jimbo la Bunda ambalo natoka mimi kuna daraja la Mto Chamtikiti ambalo limeharibika muda mrefu na hivi karibuni tumesikia kwamba kuna fedha ilitoka kwa ajili ya kutengeneza daraja, lakini mpaka leo mvua inanyesha wanafunzi hawaendi shuleni kwa sababu ya hilo daraja. Ni lini Waziri atakuja Bunda kuliona hilo daraja kwa ajili ya kusaidia hali hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Jafo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niseme ni kweli nafahamu na mimi Mheshimiwa Getere unafahamu nilikuwa kule Rorya na pale changamoto

ni kubwa. Na ni kwamba Halmashauri tunafahamu wazi kwamba kwa sasa haitaweza isipokuwa ni kwa kupitia mamlaka yetu tuliyoiunda ya *TARURA.*

Kwa hiyo, naomba niwahakikishie kwamba, suala zima la daraja hili na kwa sababu eneo hili ni eneo la kipaumbele, nitawaagiza wataalam wangu wafike katika daraja hilo, lakini na eneo lingine ambalo Mheshimiwa Getere ulilizungumza, lengo kubwa ni kwamba waende kufanya tathmini tujue thamani ya kazi halafu tutaangalia tutalitengeneza kwa kifungu gani. Aidha, kupitia *DFAD* kwamba eneo hilo saa nyingine ni eneo la vikwazo au kupitia Mfuko wa Barabara kwa kadiri itakavyoonekana inafaa, lakini nikuhakikishie kwamba, nitawatuma wataalam wangu wataenda kufanya *study* ya kutosha, lengo kubwa kuwasaidia wananchi katika maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafo. Mheshimiwa Zainab Mndolwa atafuatiwa na Mheshimiwa Massay.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi napenda kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itasitisha tozo katika Daraja la Kigamboni ili liweze kutumika kama madaraja mengine yalivyo ya Ruvu na Wami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kwanza niwashukuru Waziri wa TAMISEMI na Naibu Waziri kwa majibu mazuri yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Kigamboni limejengwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa *NSSF.* Ni kivuko ambacho kinafanya kazi kama vivuko vingine tulivyonavyo

nchini na vivuko vingine vilivyopo nchini pia vimeweka mfumo wa utozaji wa tozo kidogo ili kuhakikisha kwamba vivuko vile vinaendelea kulindwa na vinaendelea kukarabatiwa viweze kuendelea kufanya kazi.

Kwa hiyo, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge tozo iliyowekwa kwenye Kivuko cha Kigamboni na *NSSF* imefuata utaratibu wa kisheria na wa kikanuni na hivyo, itaendelea kuwepo, lakini itaendelea kuwa ikibadilishwa kulingana na mazingira na taratibu za kisheria ambazo zinaongoza tozo zote katika nchi yetu ya Tanzania katika vivuko vyote nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jenista. Mheshimiwa Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais aliahidi maeneo mengi hasa wakati wa kampeni katika Jimbo la Mbulu Vijijini aliahidi ujenzi wa barabara kilometa tano katika Mji wa Haydom na Dongobesh kilometa mbili. Je, ni lini sasa ahadi hizi za Mheshimiwa Rais zitatekelezwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Jafo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza hapa siku za nyuma zilizopita kwamba kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba uratibu wa ahadi zote za Mheshimiwa Rais umefanyiwa kazi na nikuhakikishie Mheshimiwa Flatei kwamba *commitment* yetu ni kwamba, tutakapofika mwaka 2020 tuhakikishe kwamba, zile ahadi zote za barabara hizi ambazo zimelengwa ziweze kukamilika. Na kupitia Wakala wetu wa *TARURA* tumewapa hayo maelekezo kwamba, wahakikishe kwanza jambo la kwanza wana-*identify* ahadi za Mheshimiwa Rais na ahadi za viongozi wakuu katika maeneo hayo lengo kubwa kwamba waweke mpango kazi

jinsi gani tutafanya tukifika mwaka 2020 maeneo hayo yote tuwe tumeweza kukamilisha jambo hili.

Na. 86

**Mabadiliko ya Tabianchi**

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI** Aliuliza:-

Suala la mabadiliko ya tabianchi ni mtambuka na linagusa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

(a) Je, ni mashirika ya umma mangapi yamepokea ruzuku kutoka Wizara/Idara au kwa wafadhili katika kipindi cha miaka mitano iliyopita?

(b) Je, nini madhumuni ya ruzuku hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mashirika ya umma yanayopata ruzuku kutoka kwenye Wizara, Idara au wafadhili.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye kipengele (a), haiwezekani kuelezea madhumuni ya ruzuku ambayo haitolewi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimepata masikitiko makubwa sana kutika kwenye Wizara husika ambayo inasimamia shughuli za mazingira nchini. Kwa kuwa Wizara hii ndio iliyoshikilia au

inaongoza Sheria yetu ya Mazingira ya mwaka 2014; na kwa kuwa Wizara hii ndio iliyoshikilia Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi; na kwa kuwa ni Wizara hii ambayo inasimamia Mfuko wa Mazingira Nchini; na kwa kuwa ni Wizara hii ambayo ina fedha kutoka mashirika mbalimbali nchini na duniani kote inayosimamia shughuli zote za mazingira nchini, inanijibu kwamba haitoi, haihangaiki, haina chochote, hamna jibu linalohusu shughuli za kusimamia fedha za ku-*address issues* za *climate change* nchini na tunaona dhahiri kwamba mabadiliko ya tabianchi yameleta madhara makubwa, majira ya mvua hayajulikani, kuna ukame, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua, hii Wizara ipo au haipo? Na kama ipo, mbona imenyamazia kimya *issue* ya mabadiliko ya tabianchi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninamheshimu sana Dkt. Sware ambaye *Ph.D* yake ameisoma kule Stockholm, Sweden, *Masters* yake ameichukulia Norway, namheshimu sana, lakini kwa sababu anashindwa kutofautisha kati ya maneno mawili ambayo ni rahisi sana, yeye ameuliza swali la ruzuku na ruzuku kwa kiingereza kwa faida yako Dokta tunaita *subsidies,* lakini kuna kitu kingine tunaita misaada, misaada ni *grants.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama yeye ameuliza ruzuku, ndio nimemjibu sisi hatuna ruzuku. Lakini haya aliyoyasema leo kama angejiongeza akauliza hayo, kwa faida ya Watanzania, kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na nchi yetu mpaka leo kuanzia tarehe 6 mpaka 17 wako Bonn, Ujerumani wanashiriki mkutano mkubwa wa kimataifa kujadili masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Na sisi Tanzania ni nchi wanachama ambao tulisaini Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi kule Mjini Paris na tunayo mifuko ifuatayo ambayo sisi tunakabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko wa kwanza unaitwa *Adaptation Fund,* yani kwa maana kwamba ni mfuko wa kuhimuli mabadiliko ya tabianchi. Mfuko wa pili, unaitwa ni *Least Developed Countries Fund,* yaani kwa maana Mfuko wa Nchi Maskini Duniani. Na mfuko mwingine ni *GEFT* ambao ni *Global Environmental Facility.* Mfuko mwingine ni Mfuko wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumepata *grants* hizi ambazo sasa tunapambana na athari za mabadiliko ya tabia nchi maeneo mbalimbali hapa nchini. Tuna mradi mkubwa sana ambao *Ocean Road* pale kwa sababu kina cha bahari kimeongezeka tunajenga ukuta mkubwa wa kilometa moja, ili kingo za bahari zisije zikasombwa na kuharibu makazi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Chuo cha Mwalimu Nyerere, Kigamboni tunajenga ukuta mkubwa ili kudhibiti kingo zisiendelee kubomoka. Vilevile kupitia *grants* hizo kule Rufiji tunarudishia mikoko ambayo ilikuwa imekatwa na mradi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Zanzibar Kisiwapanza, kule Zanzibar Kisakasaka pamoja na Kilimani mifuko hiyo inaendelea. Kule Pangani tunajenga ukuta pamoja na kurudishia mikoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Bagamoyo tunajenga visiwa 28 kwa wananchi wa Bagamoyo, zikiwepo na sekondari mbili mojawapo inaitwa Kinganya ambayo ni ya Mheshimiwa Dkt. Kawambwa. Mifuko hiyo, tunaitumia kwa ajili ya kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kangi Lugola. Mheshimiwa Peter Msigwa atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na athari kubwa

ambazo zimetokana na mabadiliko ya tabianchi, wakazi wa Mkoa wa Iringa wamekuwa wakihamasishwa sana namna ya kupanda miti na wamejitahidi sana kupanda miti ili kuokoa hii hali ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, kuna wakati wakazi hawa walikuwa wameambiwa kwamba jinsi wanavyoendelea kupanda miti watapata fidia kutokana na jinsi wanavyopata miti kutoka kwenye mashirika mbalimbali duniani. Je, hili limeishia wapi? Ningeomba nipate majibu kutoka Serikalini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba nchi yetu imeanza kuwa na dalili za kuwa na jangwa, nchi yetu inakuwa na ukame na hatuna *option,* lazima Watanzania kote nchini tuweze kuwa na tabia ya kupanda miti. Na kama nilivyosema juzi, ni wajibu wa kila Mtanzania kushiriki katika Ilani hii ya CCM, ukurasa wa 212 mpaka 213 unazitaka Halmashauri zote nchini wapande miti kila mwaka isiyopungua 1,500,000.

Kwa hiyo, kwa kuwa, Wananchi wa Iringa wameanza juhudi hii sisi tuko tayari kuhakikisha kwamba, hewa ya ukaa ambayo inaharibu *ozone layer* yaani tabaka la *ozone* na kusababisha miale mikubwa ya jua ule mnururisho uweze kuleta joto jingi duniani, ni kweli mashirika ya kimataifa yananunua kitu tunaita karadha, kwa jinsi ambavyo miti ile ndio inayosaidia kufyonza hewa ya ukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kuwa wananchi wa Iringa wameanza na wananchi wengine wameanza, Ofisi ya Makamu wa Rais itaanzisha utaratibu wa kuona ni kiwango gani wananchi wameweza kupanda miti ili watalaam sasa waweze kuona kiwango cha karadha ya ufyonzaji wa hewa ya ukaa, ili waweze kupata fidia kwenye mashirika ya kimataifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania hivi sasa tunaelekea katika uchumi wa viwanda. Na moja ya ajenda/ suala muhimu ambalo linazingatiwa hivi sasa ni ujenzi wa viwanda. Na kwa kuwa viwanda ni miongoni mwa mambo ambayo yanachangia uharibifu wa mazingira, kwa mfano nchi ya China pamoja na Marekani ni miongoni mwa nchi ambazo hazikukubali kusaini Mkataba wa Kyoto kutokana na viwanda. Sasa ninachotaka kujua tu ni kwamba, Tanzania kwa sababu tunahitaji viwanda.

Je, tunajiandaaje ili kuhakikisha kwamba viwanda vitakavyojengwa hapa nchini haviwi sababu ya uharibifu wa mazingira? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kulikuwa na baadhi ya nchi matajiri ambao walikuwa hawataki kusaini Mkataba wa Kyoto lakini mkutano niliouzungumzia ambao mpaka sasa wanaendelea kule Bonn, Ujerumani. Mkutano huu umekuwa wa mafanikio makubwa kwa sababu makubaliano yaliyofanyika Mjini Paris kila nchi wanatakiwa sasa wasaini mkataba ule wa mabadiliko ya tabianchi. Ka hiyo, hakutakuwa na nchi hasa hizi tajiri ambazo ndizo zinazalisha hewa ya ukaa ambayo inakuja kuathiri nchi zetu maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Tanzania ya viwanda ambayo sasa tunakwenda nayo, sheria yetu ya mazingira ambayo niko nayo hapa, Sheria Namba 20 ya mwaka 2004 ya Usimamizi wa Mazingira. Sheria hii inavitaka viwanda vyote kuhakikisha kwamba kabla hawajaanza uzalishaji wawe katika ile *Environmental Impact Assessment* pamoja na

*Environmental Management Plan* zao, namna ambavyo watakwenda ku-*manage emissions* zote ambazo zinaharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana kupitia Baraza la Hifadhi la Taifa la Mazingira *(NEMC)* tumekuwa tukikagua mara kwa mara kuhakikisha viwanda hivi vina-*comply* masharti yale ambayo hayaharibu mazingira. Ndio maana viwanda ambavyo vinakaidi tunavipiga *fine* na vingine tunavifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwahakikishia Watanzania, katika Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Jemedari Dkt. John Pombe Magufuli hakuna wazalishaji wa viwanda wanaoharibu mazingira watakaotumia nguvu za fedha kuhakikisha kwamba wanaendelea kuharibu mazingira halafu na sisi tunawatazama, lazima sheria hii itawashughulikia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 87

**Kudhibiti Uharibifu wa Mazingira Mto Songwe**

**MHE. JANET Z. MBENE** aliuliza:-

Mto Songwe umekuwa ukihama hama kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi huku ukiharibu rasilimali za wakazi wanaoishi karibu na mto huo na kingo zake kutokana na mafuriko.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudumu kudhibiti uharibifu huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa Ileje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira na maumbile ya Bonde la Mto Songwe pamoja na mgawanyiko wa unyeshaji wa mvua katika bonde hilo ndio sababu kubwa inayofanya kuwepo kwa mafuriko ya mara kwa mara kila mwaka. Inakadiriwa kuwa takribani hekta 9,000 za ardhi huathiriwa na mafuriko katika kila msimu wa mvua na kufanya Mto Songwe kubadili mkondo wake mara kwa mara, hivyo kuathiri pia mpaka kati ya nchi za Malawi na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hali hii, tatizo hili linakuwa kubwa zaidi kutokana na mabadiliko ya tabianchi na ongezeko kubwa la watu katika bonde. Aidha, matumizi mabaya yasiyo endelevu ya rasilimali zilizoko katika bonde husababisha uharibifu mkubwa wa ardhi, vyanzo vya maji, mifumo ikolojia na kutokewa kwa bioanuai zilizo katika bonde hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Malawi imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na matatizo katika Bonde la Mto Songwe. Hatua hizo ni pamoja na kuanzisha Kamisheni ya Pamoja *(Songwe River Basin Commission),* ambayo itashughulikia masuala yote ya bonde hilo. Mpaka sasa kuna sekretarieti ya mpito iliyoanzishwa ambayo inaratibu shughuli ya bonge hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tayari programu ya kuendeleza Bonde la Mto Songwe *(Songwe River Basin Development Program)* imeshaandaliwa kwa ajili ya utekelezaji. Masuala yaliyoainishwa kwenye programu kwa ajili ya utekelezaji ni kama ifuatavyo; kuendeleza kilimo endelevu, uzalishaji wa umeme kwa kutumia nguvu ya maji, kudhibiti mafuriko ya mto pamoja na kudhibiti kuhamahama kwa mto, uboreshaji wa upatikanaji na usambazaji wa maji, maendeleo ya uvuvi, kukuza utalii na uboreshaji wa mazingira na kuiwezesha kamisheni usimamizi wa pamoja wa rasilimali za Bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto za mafuriko Sekretarieti ya Mpito ya Bonde kupitia programu hii *(Songwe River Development Program)*

itajenga mabwawa matatu ambayo ni Songwe Chini, Songwe Kati na Songwe Juu. Pamoja na mabwawa hayo kutumika kudhibiti mafuriko pia yatatumika katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, usambazaji wa maji na shughuli za uvuvi. Vilevile, kutakuwa na mradi wa mazingira ambao utadhibiti kingo za mto *(River Banks Stabilization)* ili kuufanya mto usihame hame.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbene swali la nyongeza.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na naipongeza Serikali kwa kuja na huu mpango mkakati wa kuhakikisha kuwa Bonde la Mto Songwe linaendelea kuwa endelevu kwa ajili ya matumizi ya wananchi wanaozunguka mto huo. Lakini nataka niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji iliyowasilishwa hapa Bungeni kwa ajili ya mwaka 2016/2017 tulielezwa kuwa kuna mambo ambayo tayari yameshafanyika kuhusiana na juhudi za kuendeleza rasilimali za bonde hili, lakini vilevile katika masuala mazima ya kutengeneza mpango wa biashara kwa ajili ya kuendeleza bonde hili. Nataka kujua na ilisemekana kuwa vingekuwa vimekamilika kwa mwaka 2015. Je, jambo hili lilifanyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunavyozungumzia mkakati mzima wa uendelezwaji wa Bonde la Mto Songwe, wananchi wa kawaida katika maeneo ambayo yanahusika na yanaguswa na bonde hili hawana taarifa zozote wala elimu ya aina yoyote wala hawajui ni nini kinachoendelea.

Je, hii ofisi ndogo ya muda iliyoundwa imeanza kufanya kazi gani ili wananchi wetu waanze kupata uelewa ili hata mkakati huu utakapoanza kufanya kazi wawe tayari kuupokea? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nishukuru Bunge lako Tukufu, katika Bunge lililopita tulipitisha hii Kamisheni ya Songwe ambayo imeanza kazi na kwamba ofisi ipo Kyela pale na wananchi wanaitambua. Lakini tayari tumeshaomba fedha kwa ajili ya kujenga mabwawa matatu kupitia hilo Bonde la Mto Songwe ili kuweza ku-*control* mafuriko. Mabwawa hayo yatatumika pia kuzalisha umeme, lakini pia na kilimo cha umwagiliaji zaidi ya hekta 6,200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mchakato mzima wa uandaaji wa huo mradi, wananchi wote wa Mkoa wa Mbeya walishirikishwa kupitia Halmashauri zilizopo ndani ya Mkoa wa Mbeya; kwa hiyo, wananchi wapo *aware.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tuendelee kushirikiana kama kuna hitaji la kuendelea kuwafahamisha basi tuendelee kuwafahamisha, lakini mradi unakuja na kwamba tayari kupitia taasisi yetu ya *SADC* mradi huu umeshaingizwa kwa ajili ya kuombewa fedha na utekelezaji uweze kuanza. *(Makofi)*

Na. 88

**Hatima ya Wateja wa Benki ya FBME**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)* imeifutia *The Federal Bank of the Middle East (FBME)* leseni yake ya kufanya shughuli za kibenki na kuiweka chini ya ufilisi na kuiteua Bodi ya Bima ya Amana kama mfilisi kuanzia tarehe 8/5/2017.

Je, ni nini hatma ya wateja ambao waliweka fedha zao katika benki yao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa

Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatma ya wateja endapo benki au taasisi ya fedha itawekwa chini ya ufilisi imeainishwa katika kifungu namba 39(2) na (3) cha Sheria ya Benki na Taasisi za Kifedha ya mwaka 2006. Wateja wa *FBME Bank Limited* ambayo sasa hivi ipo katika ufilisi watalipwa kwa utaratibu ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kwanza ni malipo ya fidia ya bima ya amana. Kwa mujibu wa sheria, mteja mwenye amana katika benki anastahili kulipwa fidia ya bima ya amana, kiasi kisichozidi shilingi za Tanzania 1,500,000 kutegemeana na kiasi cha salio la amana yake wakati benki inafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za kulipa fidia hiyo zinatoka katika Mfuko wa Bima ya Amana *(Deposit Insurance Fund)* unaosimamiwa na Bodi ya Bima ya Amana. Wateja waliokuwa na amana zisizozidi kiwango cha juu cha fidia cha shilingi 1,500,000 wakati benki inafungwa watapata fedha zote. Aidha, wateja wenye amana zinazozidi kiwango cha juu cha fidia watalipwa shilingi 1,500,000 kwanza kutoka mfuko wa bima ya amana na salio litalipwa kwa mujibu wa Sheria ya Ufilisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili ni malipo kwa wateja ambao fidia ya bima ya amana itakuwa ndogo ikilinganishwa na salio la amana yake wakati benki inafungwa. Malipo haya yatatokana na taratibu za ufilisi ambapo mchakato wake unahusisha kukusanya madeni, fedha iliyowekezwa katika taasisi nyingine na kuuza mali na benki. Kiasi kitakacholipwa kwa kila mteja kitategemea kiasi cha fedha kitakachopatikana kutokana na mauzo ya mali, makusanyo ya madeni na fedha zilizowekezwa katika taasisi zingine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rukia Kassim una swali la nyongeza?

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti,asante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inahimiza wananchi waweke fedha benki badala ya kuweka majumbani na kwa kuwa katika jibu lako la msingi umesema kwamba malipo ya wateja hawa yatatokana na mauzo ya mali, makusanyo ya madeni na fedha zilizowekezwa katika taasisi nyingine.

Je, itakapotokea fedha za wateja ni nyingi kuliko makusanyo yaliyokuswanywa, Serikali itawasaidiaje wateja hawa ambao wao hawana makosa hasa ukizingatia kwamba benki hii ina matawi katika nchi nyingi tu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Bodi ya Akiba ya Amana wamesema kwamba hata kama mteja ameweka fedha za kigeni atalipwa fedha ya kitanzania tena kwa *rate* ambayo ilianza ufilisi yaani tarehe 8 Mei, 2017. Je, Serikali haioni kama huu ni uonevu na ipo haja ya kuingilia kati ili dhuluma hii isitendeke? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema malipo ya wateja yanalipwa kutokana na Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 kifungu cha 39. Kwa hiyo, kinachofanyika ni utekelezaji wa sheria hii na wala Serikali haina mpango wa kumuonea mteja yeyote. Nimesema madeni yatakusanywa na pesa hizo zitakusanywa. Serikali inasimamia hili kwa kiwango kikubwa na ndio maana mpaka leo tayari wameshaanza kulipwa wateja wote hawa zaidi ya wateja 695 wameshalipwa kiasi cha shilingi milioni 727,988,000. Ni Serikali yetu italisimamia hili kwa umakini mkubwa na kila mteja atapata amana yake kama ilivyowekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa walioweka fedha za kigeni, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi

tunatekeleza kazi hii kulingana na sheria yetu ya fedha na tutalisimamia hivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, swali lipo *very specific.* Mheshimiwa Machano swali fupi la nyongeza.

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Benki ya *FBME* haikufilisika na Serikali ilitambua kwa muda mrefu kwamba inatakiwa kufungwa. Na kwa kuwa wateja wake wengi walikuwa hawajapata habari ya mwanzo. Serikali haioni kwamba ilifanya uzembe ili kuwatahadharisha wateja wao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wafanyakazi wa *FBME* ambao mpaka leo hawajajua hatima zao. Je, Serikali inataka kutuambia nini kuhusu suala hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali moja tu la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa tahadhari kipindi kirefu sana na jinsi mchakato mzima ulivyoendeshwa ulikuwa wa huru na haki na wateja wote walikuwa wakifahamu nini kinaendelea ndani ya benki hii. Kama Serikali nimesema tunaendelea kusimamia sheria zetu zinazosimamia uendeshaji wa mabenki pamoja na taasisi zote za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *BOT* tumeendelea kutoa tahadhari kwa wateja wetu pale ambapo inaonekana mwenendo wa benki yoyote au taasisi yoyote ya kifedha haifanyi vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Catherine.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ili na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya benki kutofanya vizuri au kuwekwa mufilisi husababishwana *non-performing loans* au mikopo chechefu. Hesabu za Benki ya Wanawake za mwaka 2015/2016 zinaonyesha asilimia 80 ya mikopo ni mikopo chechefu *(non-performing loans).* Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha inainusuru benki hii ili isiende kuwekwa mufilisi ili iweze kuwasaidia wanawake wa Tanzania? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, uendeshaji wa benki na taasisi zote za kifedha hufuata Sheria ya Mabenki na Taasisi za Kifedha ya mwaka 2006. Nimesema Benki Kuu imekuwa ikisimamia taasisi zote hizi za kifedha kuhakikisha zinafanya vizuri. kutokana na tatizo la mikopo chechefu, Benki Kuu ya Tanzania imewaandikia na kutoa mwongozo kwa taasisi zote za kifedha kuhakikisha kwamba wanakuwa na mkakati na mkakati huo unawasilishwa Benki Kuu ya Tanzania ya jinsi gani wanashughulikia tatizo hili la mikopo chechefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho ndicho kinachoendelea kwa sasa kwa sasa mabenki yote yamekuwa makini katika kuhakikisha wanatoa mikopo kwa ajili ya nini na kwa nani kuzingatia na vigezo walivyojiwekea. Kama Serikali tuna uhakika kwamba tizo hili la mikopo chechefu litaondoka baada ya mabenki yetu na taasisi zetu za kifedha kuongeza umakini katika utoaji wa mikopo. *(Makofi)*

Na. 89

**Tozo za Sekta ya Uvuvi**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Serikali imeondoa tozo mbalimbali zilizokuwa kero kwa wananchi katika sekta ya uvuvi lakini bado kuna mkanganyiko ni tozo zipi zimefutwa na zipi zinaendelea.

(a) Je, Serikali inaweza kuainisha aina ya tozo zilizoondolewa katika sekta ya uvuvi?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa mwongozo kwa watendaji wa Halmashauri juu ya mabadiliko hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na kutekeleza Sera ya Uvuvi ya mwaka 2015 ambayo pamoja na mambo mengine inaelekeza kuweka mazingira mzuri katika kuwezesha wavuvi na wawekezaji kuendesha biashara ya uvuvi kwa ufanisi.

Aidha, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akifungua rasmi Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015 katika hotuba yake alielekeza kupitia na kuangalia tozo zote ambazo ni kero kwa wananchi ili ziondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 inaelekeza kuwezesha wavuvi wadogo kwa kuwaondolea kero mbalimbali zikiwemo tozo zisizo na tija. Ili kutekeleza maelekezo haya, wizara yangu katika Bunge la Bajeti ya mwaka 2017/2018 ilitangaza

kuondoa ada na tozo mbalimbali ambazo zilionekana kuwa kero katika sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ada na tozo zilizoondolewa katika sekta ya uvuvi ni kama ifuatavyo:-

(i) ushuru wa kaa hai (waliozalishwa na kunenepeshwa) wanaouzwa kwenda nje ya nchi.

(ii) Tozo ya cheti cha afya baada ya kukagua mazao ya uvuvi shilingi 30,000.

(iii) Ada ya ukaguzi wa kina wa kiwanda/ghala kila robo mwaka shilingi 100,000.

(iv) Tozo ya usafirishaji samaki yaani *movement permit* kuanzia kilo 101 hadi kilo 1000 shilingi 5,000; kilo 1001 hadi kilo 5000 ni shilingi 10,000; kilo 5001 hadi kilo 9999 shilingi 30,000; zaidi 10,000 na zaidi shilingi 50,000.

(v) Ada ya usajili wa chombo cha uvuvi chini ya mita 11 kwa wavuvi wadogo shilingi 20,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha mabadiliko ya tozo katika sekta ya uvuvi inatekelezwa na watendaji wa Halmashauri, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Wizara ya TAMISEMI imeshatoa maelekezo kwa Halmashauri husika kusitisha mara moja tozo ambazo zimefutwa na Serikali. Aidha, Wizara Wizara inafanya marekebisho katika Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 ili kuendana na mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kupitia Halmashauri zetu kuhakikisha kuwa maagizo haya kuhusu tozo zilizoondolewa na Serikali yanatekelezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkundi swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo nyingi katika hizi zilizoondolewa si zile zinazomgusa moja kwa moja mvuvi. Wavuvi husasan katika Ziwa Victoria, wanasumbuliwa sana na leseni kwa mfano wanazopaswa kulipa wanapotoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine, kuna ushuru wa uvuvi kwa mfano, na tozo nyingine za *SUMATRA* na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu nyingi katika hizi ziko chini ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003, Serikali sasa haioni sababu ya msingi kabisa kuleta sheria hii Bungeni ili Bunge liweze kuipitia na kuifanyia marekebisho?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa taarifa nilizonazo Mheshimiwa Waziri wewe ni mtaalam mbobezi kwenye eneo hili la uvuvi na unatoka kwenye eneo la wavuvi, kwa hiyo unaujua vizuri uvuvi na kwa sababu matatizo mengi ya wavuvi, hususan eneo la Ukerewe yanazungumzika, je, uko tayari sasa Mheshimiwa Waziri baada ya Bunge hili tuweze kuandamana kwenda katika Visiwa vya Ukerewe upate fursa ya kuzungumza na wavuvi na kusikiliza kero zao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza anasema kwamba tozo nyingi zilizofutwa sizo zile ambazo ni kero hasa inayowasumbua wavuvi na akatuomba kuleta mabadiliko ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie tu kwamba matakwa yake haya tunayachukua na tayari Serikali ipo katika mpango wa kuboresha moja ya Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003, Sheria Na. 22 na kupitia kanuni mbalimbali ambazo zitakwenda kuboresha kwa maana ya tozo hizi zilizofutwa, sawa na majibu yangu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nimhakikishie; hizi tozo, hasa ile ya *movement permit* iliyofutwa ilikuwa ni kero kubwa kwa wavuvi wetu na ndiyo maana Serikali hii ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Dkt. John Pombe Jospeh Magufuli ikaona iifutilie mbali. Na nataka nimhakikishie ya kwamba kilichobaki ni usimamizi wa kuhakikisha *movement permit* haiendelei kutozwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni la kwenda Ukerewe; ni kweli mimi ni mvuvi na uvuvi ni maisha yetu. Nataka nimhakikishie rafiki yangu ya kwamba tutafika Ukerewe kwenda kuzungumza na wavuvi na kwenda kuwatoa majaka roho yote yanayowasumbua. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy swali la nyongeza kwa ufupi na majibu yawe mafupi pia.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachukulia mfano wa mabasi, kuna utingo, kuna dereva, kuna konda, mwenye *licence* ya kuendesha chombo pale ni mmoja tu ambaye ni dereva, utingo hana *licence* wala konda. Cha ajabu katika Ziwa Tanganyika mwenye chombo anakuwa na wavuvi wake kama kumi au kumi na tano na wote wanalazimika kuwa na leseni. Je, Serikali haioni kama ni kero?

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa swali fupi Mheshimiwa Keissy. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, haya ndiyo mabadiliko tunayokwenda kuyafanya katika Kanuni za Uvuvi, kuboresha ili kuweza kumuinua mvuvi wa Tanzania. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Keissy kanuni yetu ya Uvuvi tunayokwenda kuibadilisha itazingatia matakwa haya ya Waheshimiwa Wabunge.

Na. 90

**Ahadi ya Serikali kwa Vijana Wafugaji**

**MHE. MARIA N. KANGOYE** aliuliza:-

Serikali kupitia Ilani ya CCM ya 2015 – 2020, ahadi namba 25(d) iliwaahidi vijana wafugaji kuwa itatoa dhamana ya mikopo kwenye asasi za fedha.

(a) Je, Serikali imeandaa mkakati gani wa kuwawezesha vijana wafugaji kuunda vyama vya ushirika ili waweze kunufaika na ahadi hiyo ya CCM?

(b) Je, Serikali inayo orodha ya vikundi vya vijana wafugaji ambao wamejiunga na vyama vya ushirika ambao wameweza kunufaika na utaratibu wowote ulioandaliwa na Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati ulioandaliwa na Serikali katika kuwawezesha vijana wafugaji kuunda vyama vya ushirika ni pamoja na kushirikisha Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvivi, Ofisi ya Rais TAMISEMI na wadau wengine katika kuhamasisha wafugaji, hususan vijana kuanzisha, kufufua na kujiunga na vyama vya ushirika vilivyopo. Uhamasishaji huo umefanyika kupitia mikutano na kampeni katika mikoa mbalimbali ikiwemo mikoa ya Tanga, Shinyanga, Mwanza, Iringa, Rukwa, Njombe, Manyara, Dodoma, Lindi na Mtwara ambapo wananchi walihamasika na kujiunga katika ushirika. Vilevile Wizara imeviunganisha vyama vya ushirika na wadau mbalimbali katika kuhamasisha ufugaji na uboreshaji wa mifugo. Baadhi ya wadau hao ni *Oxfam, Care International* na *CARITAS.*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni idadi ya wafugaji waliohamashishwa kujiunga na vyama vya ushirika katika mikoa mbalimbali; Tanga jamii ya Wamasai na Wabarbaig wapatao 253; Njombe na Lindi wafugaji 265 walipatiwa elimu ya ushirika; Singida vikundi 62 vyenye wanachama 1,397 vilipatiwa elimu; Rukwa jumla ya wananchi 968 walihamasika kwa kujiunga kuanzisha vikundi vya ushirika; Dodoma kuna vikundi vipatavyo 338 ambavyo vinaundwa na rika mbalimbali; Shinyanga kuna vikundi 47, kati ya hivyo viwili vinajishughulisha na unenepeshaji wa ng'ombe na usindikaji wa ngozi. Taasisi za *BRAC, Good Neighbourhood* na *World Vision* zinatoa ufadhili wa mafunzo, ujenzi wa mabanda ya mfano, mifugo ya kuanzia kama mbegu pamoja na mashine za kuchakata ngozi kwa vikundi vya Mkoa wa Dodoma.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Kangoye swali la nyongeza.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ninapenda kujua ni nini mpango wa Serikali wa kuwapatia vijana wafugaji elimu ya malisho katika ufugaji endelevu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika majibu ya Serikali kwa swali langu la msingi kipengele (b) ni dhahiri kwamba Mkoani Mwanza hakuna vikundi vya vijana/wafugaji ambao wamejiunga na vyama hivi vya ushirika.

Je, ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuambatana na mimi kwenda Mkoani Mwanza kukutana na maafisa vijana pamoja na maafisa ufugaji ili tuweze kutafuta namna ya kuwawezesha vijana hawa kujiunga na vyama hivyo vya ushirika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, mpango wa Serikali ni nini wa kuwapatia elimu vijana wa nchi hii juu ya malisho.

Kwanza, kupitia mpango mkakati kabambe kwa maana ya *Tanzania Livestock Masterplan* ambao tunakwenda kuuzindua sasa katika eneo hili la malisho tumeweka msisitizo mkubwa sana. Nataka niwaambie vijana nchi nzima ya kwamba malisho ni uchumi, leo mbegu kilo moja ya malisho inauzwa takribani 15,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya ng'ombe mwenyewe na mazao yake, lakini uwepo wa malisho mtu ama kijana akijikita katika malisho anao uwezo na uhakika wa kupata kipato chake kitakachomsaidia katika kuendesha maisha yake. Hivyo, Serikali katika kuhakikisha hili tayari tunao mpango wa kuhakikisha mbegu za malisho zinapatikana madukani ili ziweze kuuzwa kama zinavyouzwa mbegu zingine kwa maana ya mbegu za mahindi, mpunga na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la Mheshimiwa Maria Kangoye ni kwenda Mwanza kukutana na kuwahamasisha vijana juu ya shughuli za ufugaji na uandaaji wa malisho; nataka nimhakikishie Mheshimiwa Kangoye niko tayari hata baada tu ya kumaliza Bunge hili kuambatana naye kuelekea Mwanza.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea na Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza sasa aulize swali lake.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali. Lakini kabla ya hapo, niombe niungane na wananchi wa Jimbo la Ngara na Wtanzania kwa ujumla kuonesha masikitiko makubwa ya tukio kubwa ambalo lilitokea katika Jimbo la Ngara kwenye Shule ya Msingi Kihinga, mlipuko wa bomu ambao ulisababisha kupoteza uhai wa watoto wetu watano na

wengine 11 kujeruhiwa vibaya sana mpaka sasa hivi bado wapo hospitalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Ngara na Watanzania kwa ujumla. Niombe sasa swali langu namba 91 liweze kupatiwa majibu ya Serikali.

Na. 91

**Ujenzi wa Malambo – Jimbo la Ngara**

**MHE. ALEX R. GASHAZA** aliuliza:-

Jimbo la Ngara lina mifugo mingi hususan ng'ombe na mbuzi, lakini kuna tatizo kubwa la maeneo ya kunyweshea mifugo kwa maana ya malambo/ mabwawa kwa ajili ya kunyweshea mifugo.

Je, ni lini Serikali itaanza uchimbaji na ujenzi wa malambo/mabwawa kwa ajili ya kunyweshea mifugo?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, kwanza napenda kumpa pole sana rafiki yangu, Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, mpiganaji, Mbunge wa Ngara kwa maafa yaliyowapa Wanangara, lakini pia naomba kujibu swali sasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wilaya ya Ngara ina mifugo mingi ambapo pia hali hii inasababishwa na mifugo kuhamia kutoka nchi jirani bila kufuata utaratibu. Takwimu za mwaka 2016 zinaonesha Wilaya ya Ngara ina ng'ombe wa asili 70,000, ng'ombe wa maziwa 2,872 na mbuzi wa asili 190,000, mbuzi wa maziwa 169,000 na kondoo wa asili 14,600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo jitihada mbalimbali ambazo zimechukuliwa na Serikali ili kukabiliana na upungufu wa maji kwa mifugo. Serikali imekuwa ikitekeleza mkakati wa kujenga malambo ya maji kwa ajili ya mifugo katika maeneo

mengi nchini tangu mwaka 2001/2002 kwa kupitia bajeti ya Wizara na kupitia miradi shirikishi ya kuendeleza kilimo katika Wilaya ya Ngara pia katika miradi iliyoibuliwa na jamii yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi hizo, Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kupitia ufadhili wa *TASAF* Awamu ya Tatu, inatarajiwa kujenga mabirika manne ya kunyweshea mifugo katika vijiji vya Magamba, Mumuhamba, Munjebwe na Nterungwe. Aidha, mradi unajenga bwawa moja katika kijiji cha Kasulo na miradi yote ya maji ya mifugo hadi kukamilika itagharimu jumla ya shilingi 135,569,900. Ujenzi wa malambo yote umekamilika, kilichobakia ni ujenzi wa mabirika ya kunyweshea mifugo. Jumla ya watu takribani 685 watafaidika na miradi hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gashaza swali la nyongeza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali na kwa jitihada ambazo wanazifanya, natambua jitihada hizo; niombe kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Ngara kuna maeneo ambapo kuna mifugo mingi zaidi kuliko maeneo haya yaliyotajwa kuwekwa miradi hii. Kwa mfano kwenye kata za Keza, Nyamagoma, Mnusagamba katika kijiji cha Mnusagamba na Ntanga. Sasa, je, Serikali iko tayari kutenga fedha kwa ajili ya kupeleka huduma hii ya malambo katika maeneo hayo kwa sababu ndiyo maeneo yenye mifugo mingi zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwenye sekta hii ya mifugo, ikiwa ni pamoja na Jimbo la Ngara, hususan baada ya mifugo mingi kutoka maporini kwenye hifadhi kurudi vijijini, kuna tatizo kubwa la migogoro kwa maana ya wakulima na wafugaji, lakini Serikali iliunda Kamati kutoka kwenye Wizara sita ili kupitia mchakato kuona ni namna gani ambavyo wanaweza wakatoa suluhisho la kudumu.

Je, ni lini Kamati hii iliyoundwa ya Wizara sita itakuja na mpango au pengine ku-*implement* matumzi bora ya ardhi kama suluhisho la kuondoa migogoro kati ya wakulima na wafugaji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Alex Gashaza, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ameuliza juu ya lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya maeneo hayo yenye mifugo mingi. Jambo hili linapaswa yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge na wenzake katika Halmashauri waliibue na sisi Serikali tuko tayari kuhakikisha ya kwamba tunawaunga mkono ili kuweza kuondoa kero hiyo ya ukosefu wa maji kwa ajili ya mifugo katika Wilaya ya Ngara na maeneo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ameuliza juu ya Kamati iliyoundwa na Serikali kupitia Wizara sita kuondoa matatizo ya wakulima na wafugaji, ndiyo maana nilieleza katika jibu letu la msingi ya kwamba maeneo ya Ngara yanalo tatizo kubwa la kuvamiwa na mifugo kutoka nchi jirani na ndiyo maana sisi katika Serikali tumejielekeza ya kwamba hatutarudi nyuma, tutahakikisha mifugo yote iliyotoka nchi jirani kuingia Tanzania kutufanya kuwa sisi ni eneo la malisho tutaitoa kwa namna yoyote ile ama kuikamata na kuhakikisha tunaitaifisha kwa Sheria Na. 17 ya Magonjwa ya Wanyama ya mwaka 2003. Lakini vilevile kwa sheria ya mwaka 2010 inayohusu rasilimali malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na juu ya *task force* hii iliyoundwa jitihada nyingi zimeshafanyika katika maeneo haya ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba maeneo yetu ambayo tulikuwa tumeyahifadhi kama vile *Mwisa II* yanakwenda kugawanywa kwa ajili ya wafugaji waweze

kupata maeneo ya kufanyia shughuli zao za ufugaji kwa nafasi. Naomba sasa Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine watupe ushirikiano kuhakikisha jambo hili linafanikiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Naona muda wetu unakwenda. Naomba maswali yawe mafupi, moja kutoka kwa Mheshimiwa Mwita na lingine kwa Mheshimiwa pale.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Pugu, Jimbo la Ukonga kuna Mnada wa Kimataifa wa Pugu, nimuombe Mheshimiwa Waziri kama yupo tayari tumpeleke katika eneo hili akutane na wafanyabiashara wa eneo hili ili wamueleze kero kubwa ziliyopo zikiwemo za ukosefu wa malisho na bwawa la maji na vyoo na mnada huu unaitwa wa kimataifa ambao kimsingi ndio unalisha Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Waziri, upo tayari kwenda Pugu ukutane na watu hawa wakueleze kero zao kiundani zaidi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa swali fupi. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi na wewe.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari kwenda Pugu kukutana na wafugaji hawa na wauzaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa pale swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara imeanza kutekeleza ujenzi wa Bwawa la Mwanjolo, lakini mapungufu yaliyopo katika mkataba huo ni mabirika ya

kunyweshea mifugo; je, Serikali haioni haja ya kuongeza mabirika ya kutosha ukizingatia Ukanda huo una ng'ombe wengi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sisi tunatambua ya kwamba mifugo ni maisha yetu na ufugaji ndiyo maisha yetu. Nataka nimhakikishie kwamba wao kupitia Halmashauri waibue miradi hii na sisi katika Serikali tutahakikisha kwamba tunawaunga mkono ili kusudi jambo hili linalohusu malisho na maji kwa ajili ya mifugo tatizo hili liweze kuisha.

Na. 92

**Kurudisha Eneo la *VETA* Kwa Kanisa la Moravian-Tabora**

**MHE. JOHN P. KADUTU** aliuliza:-

Miaka mingi iliyopita Serikali iliwahi kuzichukua hospitali, shule na huduma nyingine nyingi kutoka katika mashirika ya dini na baadae Serikali ilirudisha huduma hizo kwa wamiliki wake, Kanisa la Moravian Tabora lilikuwa na eneo la *VETA*, Serikali wakati wa kurudisha haikurudisha eneo hilo kwa Kanisa hilo.

(a) Je, ni lini Serikali itarudisha eneo hilo kwa wamiliki wake?

(b) Je, Serikali ipo tayari kulipa fidia kwa kuwa na eneo ambalo siyo lake?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swali la

Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwaka 1973, Kanisa la Moravian Tanzania Magharibi lilikabidhi eneo, majengo na mali inayohamishika na isiyohamishika kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara. Misingi na sababu maalum ambazo zilikubaliwa na pande zote mbili ilikuwa ni kwamba eneo hilo litumike kama chuo cha kufundishia mafunzo mbalimbali ya ufundi. Walengwa walikuwa ni vijana ambao hawakupata nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari baada ya kuhitimu elimu ya msingi na lengo ilikuwa ni kwamba ni kuwapa stadi mbalimbali za ufundi kwa ajili ya kuweza kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kukabidhiwa eneo hilo, lilikabidhi kwa Shirika la *SIDO* lililokuwa chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwama 1974 ili eneo hilo litumike kuendesha mafunzo ya ufundi. Hata hivyo, mwaka 2002 eneno hilo lilikabidhiwa kwa *VETA* kwa lengo la kuendelea kutoa mafunzo ya ufundi stadi. Aidha, *VETA* imeendelea na majuku hayo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa mwenyekiti, napenda kukifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali haijarudisha maeneo yote ya kielimu ambayo awali yalikuwa yanamilikiwa na mashirika ya dini bali kuna baadhi ya maeneo ambayo yalirudishwa kwa makubaliano ya pande zote mbili. Aidha, kwa ajili ya manufaa mapana ya Taifa kwa sasa Serikali haina mpango wa kurudisha maeneo mengine kama hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter swali la nyongeza.

**MHE. JOHN P. KADUTU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa fursa ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwanza, ni vigezo gani viliifanya Serikali kurudisha mali za madhehebu mengine kama hospitali ya KCMC, Bugando

na mashule na kwa nini isirudishwe mali za Kanisa hili la Moravian?

Swali la pili, kwa kuwa mgogoro huu na utata huu umechukua zaidi ya miaka 44, je, sasa Serikali ipo tayari kukaa katika meza ya majadiliano na Kanisa kumaliza utata huu uliodumu kwa miaka hiyo 44? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba baada ya zoezi lilioendelea baada ya miaka ya 1960 ya shule nyingi zilizokuwa chini ya mashirika ya dini kupelekwa Serikalini kwa makubaliano maalum, lakini baadaye kuna baadhi ya huduma kama za hospitali ambazo zilirudishwa.

Naomba tu nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba urudishwaji wa hospitali zile na baadhi ya huduma imefanywa kwa makubaliano maalum na madhehebu ya dini, vivyo hivyo hata shule ambazo zimeendelea kubakia Serikalini ambazo zamani zilikuwa ni shule za taasisi za kidini, kubakia Serikaini vilevile ni suala la makubaliano. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kusaidia na madhehebu ya dini na mashirika mbalimbali na sekta binafsi katika kuendeleza elimu ikiwa ni pamoja na kuendelea kuzihudumia shule hizo kwa sababu inafanyika kwa maslahi mapana ya Taifa. Ifahamike kwamba miaka ya 63 zoezi hilo lilivyochukuliwa kulikuwa na makubaliano kama njia mojawapo ya kuhakikisha kwamba kunakuwa na usawa wa utoaji huduma na hususani elimu

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili kwamba ni lini majadiliano yatafanyika na Kanisa la Moravian kuhusu eneo la Chuo cha *VETA* tunachokizungumzia, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa hakuna mgogoro wowote uliopo katika umilikaji wa eneo hilo kwa sababu tokea lilipotolewa mwaka 1973 ilifanyika kwa makubaliano na makubaliano hayo bado yanafanya kazi, changamoto kidogo ambayo imetokea ni

kuhusu chuo kuendelea kutumika kwa malengo yale ambayo ilianzishwa nayo na malengo yenyewe ilikuwa ni kuwasaidia wanafunzi ambao wamekosa fursa ya kwenda katika elimu ya sekondari sasa hili linaweza likajadiliwa lakini mgogoro haupo kwenye umiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba, Wizara yangu na Serikali iko tayari kuendelea kushirikiana na Kanisa la Moravian, ni washirika wetu tokea siku nyingi sana tokea miaka ya 1970, tunawashukuru sana, tutaendelea kujadiliana nao namna bora ya kutumia chuo hiki kwa maendeleo ya Taifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, swali liko *very specific* nitatoa nafasi mbili tu lakini kwa ufupi sana. Mheshimiwa Salome na Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri katika Jimbo la Kahama, Kata ya Mwendakulima kuna mgogoro wa muda mrefu sana kati ya Kanisa la Katoliki na Kijiji cha Mwendakulima na sasa ni mtaa juu ya ardhi ambayo Kanisa hili limemiliki.

Mheshimiwa Waziri, je, uko tayari kwenda na mimi katika Jimbo hili na Kata hii kuweza kutatua mgogoro huu maana umekuwa ni wa muda mrefu na unaleta hali ya kutoelewana kati ya Kanisa na wananchi wa Mwendakulima? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri jibu kwa ufupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimahakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari kwenda naye katika eneo hilo na ikiwezekana kuwashirikisha wenzetu wa Wizara ya Ardhi tuone mgogoro huo namna ya kusuluhisha, lakini kwa kuanzia

hata leo niko tayari tukutane mimi na yeye tujadiliane kuhusu hili.

**MWENYEKITI:** Sawa, ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Zacharia swali fupi sana.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbulu Mjini limekuwa na migogoro ya ardhi hususani shule zetu za msingi na sekondari na kwa sasa karibu shule mbili ziko mahakamani kwa ajili ya kutetea ardhi zake.

Je, Serikali haiwezi kuchukua utaratibu sasa wa kuhakikisha kuwa maeneo yote ya shule za msingi na sekondari nchini zinapata kupimwa ili ziweze kuepukana na adha hii ya migogoro ya ardhi kwa taasisi hizi za Serikali?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Zacharia kwa swali ambalo ni ushauri pia. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema, Serikali inahitaji kupima hayo maeneo naomba tu nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kuna mkakati na maelekezo madhubuti ili taasisi zote za umma hususani shule kuhakikisa kwamba maeneo yao yote yanapimwa na kupatiwa hati ili kuondoa migogoro ambayo inaweza ikatokea pamoja na uvamizi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, muda wetu wa maswali siyo rafiki sana. Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, swali linaulizwa na Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi sasa aulize swali lake.

Na. 93

**Kufufua Kambi ya JKT ya Luwa-Rukwa**

**MHE. SILAFU J. MAUFI** aliuliza:-

Serikali imerejesha mafunzo ya JKT nchini. Je, ni lini Kambi ya JKT ya Luwa Mkoani Rukwa itafufuliwa ili kuandaa vijana wetu?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silafu Maufi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Luwa JKT ilifufukiwa na sasa kimekuwa Kikosi na kimepewa namba 846 Kikosi cha Jeshi yaani 846 KJ kuanzia tarehe 01 Desemba, 2016.

Aidha, vikosi vilivyoanzishwa sambamba na kikosi hicho ni pamoja na Kikosi cha Jeshi 826 kilichopo Mpwapwa hapa Dodoma, 839 Kikosi cha Jeshi kilichopo Makuyuni, Mjini Arusha, 845 Kikosi cha Jeshi kilichopo Itaka, Mkoani Songwe na 847 Kikosi cha Jesi kilichopo Milundikwa, Mkoani Rukwa

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Silafu una swali la nyongeza?

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashukuru hayo majibu niliyopewa na Mheshimiwa Waziri, lakini niliuliza swali kwamba kufufuliwa Kambi ya JKT, sikuuliza swali la kwamba mabadiliko ya matumizi ya Kambi ya JKT, la hasha. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa tunajua wazi kwamba kujiunga kwa vijana wetu kwenye JKT ndiko ambako kuna chachu ya kuwawezesha wao kujiunga na Polisi, kujiunga na JWTZ na kadhalika. Sasa je, ni sababu zipi zilizopelekea kutoka JKT na kuwa Kikosi cha Jeshi na kusababisha Mkoa wetu wa Rukwa kukosa Kambi ya Jeshi?

Swali la pili, je, vijana wetu ambao wanauhitaji wa kujiunga na JKT wa Mkoa wa Rukwa kutokana na wingi wao wa kila mwaka kuongezeka ndani ya jamii, je, hawa vijana watanufaika vipi na vikosi hivyo ambavyo vimebadilishwa makambi yao kuwa ni vikosi vya Jeshi au watajengewa Kambi ya Jeshi upande gani? Naomba uniambie katika Mkoa wetu wa Rukwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mbunge kwa kuguswa kwake na vijana hasa hasa wa Mkoa wa Rukwa na hoja yake ya kutaka vijana wapate fursa hiyo, lakini nimhakikishie tu ninapojibu maswali yake yote mawili kwa pamoja ni kwamba Kambi la Jeshi kubwa hasa linaloangaliwa ni suala la kibajeti.

Natambua katika nchi nzima vijana wengi hata maeneo ambako kuna Kambi wengi sana wanajitokeza kuomba nafasi hizo, unaweza ukakuta Wilaya ambako wamejitokeza vijana kama 500, idadi inayotakiwa kupatikana labda ni 50 mpaka 60 kwa maana hiyo sisi kama Serikali tunapokea tu hoja ya Mbunge na uhitaji mkubwa huo wa kuona vijana wanataka kujitolea kwenda kujenga Taifa ili tuliangalie kwenye upande wa bajeti kwasababu kwenye upande wa makambi hilo ni jambo rahisi tu ambalo wanaweza wakakaa tu katika Kambi yoyote ile na mafunzo haya yakaendelea kama ambavyo inafanyika katika mikoa mingine.

Na. 94

**Uchimbaji wa Gesi ya Hellium-Rukwa**

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO** aliuliza:-

Kuna taarifa zilizotolewa na Wizara ya Nishati na Madini za kugunduliwa kwa gesi ya Hellium yenye ujazo wa takribani futi bilioni 54 za ujazo nchini.

Je, Serikali imejiandaaje kimkakati kuhusu ugunduzi huo na uchimbaji wa gesi hiyo hasa ikizingatiwa kuwa mataifa makubwa kama Marekani yalishatangaza kukosekana kwa gesi hiyo ifikapo 2030?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos Nyimbo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Kampuni ya *Hellium One Ltd.* imegundua kiasi cha gesi ya Hellium yenye ujazo wa *cubic feet 54 billions* katika maeneo ya Ziwa Rukwa. Ugunduzi huo ulitokana na uchunguzi wa sampuli tazo za Mavujia yaani *gas seeps* ya gesi ya Hellium katika maeneo hayo kiasi ambacho kinakadiriwa kuwa kikubwa zaidi ya mara sita ya mahitaji ya dunia kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Hellium One Ltd.* imegundua madini ya hellium kupitia Kampuni zake tanzu za *Gogota Tanzania Ltd., Njozi Tanzania Ltd.* na *Stahamili Tanzania Ltd.* zinazomiliki leseni z utafutaji wa gesi ya hellium katika Mkoa wa Rukwa ikiwemo maeneo ya Ziwa Rukwa. Kampuni hizi zilipewa leseni za utafutaji wa hellium katika maeneo mbalimbali kuanzia mwaka 2015. Shughuli za utafutaji wa kina wa gesi ya helium unaendelea kwa kukusanya taarifa zaidi za kijiolojia, kijiokemia, kijiofizikia na *2D Seismic Survey* ili zitumike kwa ajili ya uchorongaji wa visima vya utafiti yaani *exploratoty wells.* Kazi ya uchorongaji

ikikamilika itawezesha kuhakiki kiasi halisi cha gesi ya hellium kilichopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji wa gesi ya hellium utaanza mara baada ya kazi ya utafiti wa kina, upembuzi yakinifu na tathmini ya athari za mazingira, kukamilika kwa leseni ya uchumbaji wa gesi hiyo kutolewa. Matokeo ya gesi hizo ndiyo yatakayoonyesha kama kiasi cha gesi kilichopo kinaweza kuchimbwa kibiashara kwa kipindi gani na taifa litanufaikaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufundisha wataalam stahiki yaani wajiolojia, wahandisi wa migodi na wachumi wa madini kusudi wawe na ujuzi wa kutosha na hadi sasa Serikali ina jumla ya wataalam 454 wenye fani za mafuta na gesi katika viwango mbalimbali na elimu. Pia kuna wanafunzi 137 walipo katika mafunzo ya mafuta na gesi katika ngazi za shahada za uzamivu katika vyuo mbalimbali nje ya nchi na wanafunzi 455 katika ngazi ya diploma na shahada ya kwanza ndani ya nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tauhida una swali la nyongeza?

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunijibu swali langu kiufasaha kabisa, lakini vilevile nina maswali mawili madogo.

Je, Serikali inaweza kutuambia nini uchorongaji utafanyika wa kazi hiyo?

Swali langu la pili, je, nje ya Mkoa wa Rukwa kuna Mkoa mwingine wowote umeweza kugundulika kwa gesi hii?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Tauhida kwa maswali mafupi ya Kibunge. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya uchorongaji itaanza pale taarifa za kijiolojia zikishakamilika na kwa mujibu wa taratibu zilivyokuwa zimepangwa katika Kampuni hii ya *Hellium One Tanzania Ltd.* wamepanga kuanza shughuli ya uchorongaji kuanzia mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile swali la pili, ni sehemu gani ambapo hii hellium inapatikana. Kwa kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge ni kwamba gesi ya hellium vilevile inapatikana katika Ziwa Eyasi lililoko Mkoa wa Manyara na sehemu nyongine ni sehemu ya Singida ambapo na penyewe inapatikana hii gesi ya hellium. Ahsante sana.

Na. 95

**Uuzaji wa Bidhaa za Ngozi na Nguo Kwenye *Export Processing Zone***

**MHE.BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Kupitia vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki, mwaka 2015 Serikali ya Kenya iliruhusiwa na Jumuiya hiyo kuuza ndani ya nchi hiyo bila kutozwa kodi bidhaa za ngozi na nguo zinazozalishwa nchini humo kwenye maeneo huru ya uwekezaji *(Export Processing Zones [EPZ]).*

Je, ni sababu zipi za msingi zilizotumika kufanya uamuzi huo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Itifaki ya Umoja wa Forodha ya Afrika Mashariki ibara ya 25 inahusu

kanuni zinazosimamia uzalishaji kwenye maeneo huru ya uwekezaji kutoka nje, teknolojia na kutengeneza ajira. Ibara ya 26 inaeleza kuwa viwanda vilivyopo kwenye maeneo haya havipaswi kulipa kodi hata kidogo...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mnazungumza kwa sauti kubwa naomba mtulizane.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** ...havipaswi kulipa kodi hata kidogo wanapoingiza malighafi kwa ajili ya uzalishaji. Aidha, viwanda hivi vinaanzishwa kwa ajili ya kuongeza mauzo nje na kupata fedha za kigeni na wanaweza kuuza kwenye soko la ndani asilimia 20 ya kiwango kinachozalishwa kwa mwaka huska na kulipa kodi kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia Mkutano wa 17 wa Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao ulizungumzia suala la mitumba ya na viatu, Serikali ya Kenya iliwasilisha ombi la kuuza asilimia 20 ya bidhaa zinazozalishwa katika maeneo huru ya uwekezaji yaani *EPZ* bila kulipa kodi. Sababu ya msingi iliyowasilishwa na Kenya na kukubaliwa na nchi wanachama ni kuwa kwa kuuza bidhaa hiyo bila ushuru wananchi wangenunua bidhaaa mpya kutoka maeneo huru ya uwekezaji badala ya mitumba. Pamoja na kukubali ombi hilo iliamuliwa kuwa bidhaa kutoka maeneo huru ya uwekezaji yaani *EPZ* ikiingia katika nchi za jumuia itatozwa kodi zote pamoja na ushuru wa forodha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kamala swali la nyongeza.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu lakini ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Kenya iliruhusiwa kuuza bidhaa zake zinazozalishwa *EPZ* asilimia 20 bila kodi jambo ambalo alitakiwi, lakini kwa nini wakati huo huo baada ya muda mfupi

Kenya hiyo hiyo ikaruhusiwa mitumba inayotaka nje badala ya kutozwa senti 40 kwa kilo watoze senti 20 kwa kilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi za Ethiopia, Afrika ya Kusini, India, Morocco na nyinginezo zinatoa mkakati maalum wa kusaidia viwanda vya nguo na ngozi ili watu waweze kuwekeza kwenye sekta hizo kwa kutoa *garantees* walau ya miezi ya sita na baadaye Serikali inajiondoa na wazalishaji wanaendelea na kwa kufanya hivyo Ethiopia na nchi nyingine zimefanya vizuri Je, Tanzania tuko tayari walau kujifunza kidogo kutoka katika nchi hizo?

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza suala la nguo pamoja na mitumba ni suala ambalo ni nyeti na suala ambalo linahusu viwanda vyetu vya Afrika Mashariki kwa ujumla. Kimsingi ni kwamba kufuatia maombi hayo kumekuwa na mambo mengine ambayo yameendelea ambayo yameendelea kujadiliwa na nchi. Lakini kubwa zaidi ni kama nilivyosema awali kwamba swala hilo lilikuwa limejadiliwa na Wakuu wetu wananchi.

Kwa hiyo, mabadiliko mengine yoyote yale ni muhimu lazima yarudi tena kwa wakuu wetu wa nchi na misingi hiyo naamini kwamba Serikali kwa kushirikiana na nchi ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa ujumla wake tutapata ufumbuzi wa mambo ambayo yanayoonekana labda pengine yanakuja kuwa ni kikwazo hasa katika kuhakikisha kwamba bidhaa zinazotoka kwenye nchi zetu zinalindwa vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusiana na kujifunza kutoka nchi nyingine za Morocco na kadhalika. Kimsingi wajasiriamali hawa wawekezaji wanapokuja kwenye nchi wanakuja na mitaji lakini wanakutana na sheria mbalimbali ambazo kwa upande mmoja zinakuwa zinasaidia kuwezesha uwekezaji huo, lakini upande mwingine inaweza ikatokea kwamba kuna vikwazo na sisi tumekuwa tukiendelea kujifunza

na kuona namna bora zaidi ya kuwasaidia wawekezaji wetu ili waweze kukua na kuendeleza viwanda vinavyowekezwa na ajira kwa ujumla.

Kwa hiyo, ni wazo jema tutaendelea kujifunza na vilevile kuona namna bora kadri inavyoonekana kila siku ya kuweza kuwasaidia wawekezaji wetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri hilo lilikuwa swali letu la mwisho na sasa ni wakati wa matangazo, kwanza nitaanza na wageni.

Tutaanza na wageni ambao wapo kwenye *Speaker's Gallery* ambao ni Bibi Mwanahiba Mohamedi Mzee, ni Mkurugenzi Mtendaji wa *ECO Bank* akiambatana na Bwana Respiji Kimati, Mkuu wa Kitengo cha Biashara za Kati *ECO Bank.* Karibuni sana wageni wetu kwenye *Speaker's Gallery. (Makofi)*

Lakini tuna wageni 48 wa Mheshimiwa Japhet N. Hasunga, Mbunge na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) kutoka Mbozi Mkoa wa Songwe. Karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 30 wa Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mbunge na Makamu Mwenyekiti *Bunge Sport Club* ambao ni *Muungano Jogging* kutoka Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Ahmed Khalfani. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia kuna wageni 16 wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza (Mbunge) ambao ni viongozi wa Muungano wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIMATA) na Viongozi wa Masoko yanayofanya kazi na muungano huo kutoka Mikoa mbalimbali nchini. Katibuni sana. *(Makofi)*

Pia kuna wageni watano wa Mheshimiwa Daniel Mtuka (Mbunge) ambao ni wadau kutoka *TACOSODE* Mkoa wa Dar es Salaam. Karibuni sana.

Kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Flatei G. Massay (Mbunge) ambao ni wafadhili wa shule ya sekondari Gote Dongobesa iliyopo Mbulu Mkoa wa Manyara, Ndugu Gote Stenroos ambaye amefuatana na mke wake Ulla Stenroos. Karibuni sana, *you are mostly welcome.*

Mgeni mwingine ni Dkt. Ibrahimu Shabani Salum huyu ni mwanafunzi aliyemaliza hivi karibuni *intership* pale *Dodoma General Hospital* na ni mtoto wa Mheshimiwa Asha Abdullah Juma (Mshua), karibu sana. Hongera sana Dkt. Ibrahimu na Asha Mshua kwa kuimarisha Muungano. *(Mkaofi)*

Wageni wengine ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo ni wageni watatu ambao ni watumishi kutoka Bunge la Jamhuri ya Uganda na wamekuja Bungeni kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na watumishi wa idara za Kamati za Bunge na Bajeti katika Ofisi ya Bunge nao ni ndugu Ignatius Kasirye, Ndugu Alice Mukyasi, Ndugu Ssemtumbwe J. J., karibuni sana *(Makofi)*

Mwisho ninatangazo moja hapa Wabunge wanawake wote kuwa leo tarehe 15 Novemba, 2017 kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge wanawake wote itakayofanyika katika ukumbi wa pius Msekwa semina hiyo itafanyika mara tu baada ya kusitisha kikao cha Bunge saa saba mchana. Katibu tuendelee.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA :** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Muda wa miongozo umeisha kwa leo kwa hiyo sitaupokea Katibu tuendelee.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 4 wa mwaka 2017 (*The Written Laws Miscellaneous Amendment No. 4 Bill, 2017)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Tunamkaribisha sasa Mwanasheria Mkuu aweze kuja kuwasilisha Muswada wa Sheria hiyo, karibu Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la mwaka 2016 naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 4 ya mwaka 2017 yaani *The Written Laws Miscellaneous Ammendment No. 4 Act of 2017* kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho sasa usomwe kwa mara ya pili na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitishe muswada huu kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa maelezo kuhusu muswada huu ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu ndani nan je ya Bunge hili, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wakiongozwa na Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi mnavyotekeleza majukumu ya Bunge kwa ufanisi mkubwa kabisa na kwa ushirikiano mnaoutoa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati inapotekeleza majukumu yake Bungeni na katika Kamati za Kudumu za Bunge. Aidha, ninawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya

Mwanasheria mkuu wa Serikali chini ya uongozi wa Ndugu Gerson Mdemu, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo kazi na majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ninawashukuru wananchi wote kwa kuendelea kutupatia ushirikiano na taarifa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua umuhimu wa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu ya umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki ipasavyo.

Pia ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu na watendaji wengine walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kushika nyadhifa hizo mwezi Oktoba 2017, nawatakia mafanikio katika utekelezaji wa dhamana waliokabidhiwa kuwatumikia wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hatimaye kuapishwa kuwa Mbunge. Namtakia kila la kheri katika maisha na utekelezaji wa majukumu ya Bunge. Napenda kumpongeza Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwenyezi Mungu aendelee kumbariki katika utekelezaji wa majukumu ya Katibu wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tunampongeza na kumshukuru aliyekuwa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashililah kwa kazi nzuri na kwa jinsi alivyotekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa wakati akihudumu katika nafasi hiyo katika utumishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunamtakia kila la kheri katika utekelezaji majukumu mapya katika nafasi ya Naibu Katibu Mkuu katika utumishi wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na muswada uliopo mbele ya Bunge lako Tukufu leo napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria chini ya uongozi wa Mheshimiwa Mohamed Omari Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji na Mwenyekiti na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum na Mwenyekiti wa Bunge na Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 4 ya mwaka 2017 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment Act No. 4 of 2017).* Ushauri, maoni na mapendekezo ya Kamati hiyo vimetusaidia kuuboresha muswada huu kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 4 ya mwaka 2017 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment Act No. 4 of 2017* unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tano, marekebisho yanayopendekezwa kupitia muswada huu yanalenga kuboresha utekelezaji wa sheria hizo kwa kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa kuzitumia na kuongeza masharti mengine ili kuleta uwiano kati ya sheria zinazorekebishwa na sheria zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya masuala yaliyozingatiwa katika muswaada huu ni pamoja na kubadilisha vifungu vya sheria kwa kufuta baadi ya vifungu vya sheria hizo na kuviandika upya, kufuta baaadhi ya maneno kwenye vifungu vya sheria, kuingiza maneno mapya na kuongeza vifungu vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zinazorekebishwa kupitia muswaada huu ni kama ifuatavyo; kwanza Sheria ya Mahakama ya Utatuzi wa Migogogro ya Ardhi sura 216 yaani *The Land Disputes Courts Act CAP. 216;* pili, Sheria ya Upimaji wa Ardhi Sura ya 324 yaani *The Land Survey Act, CAP. 324;* tatu, Sheria ya Mikataba ya Maliasili na Rasilimali za Nchi, Mapitio na Majadiliano ya Masharti Hasi *of 2017* yaani *The Natural Wealth and Resources Contracts Review and Re-*

*Negotiations of Unconscionable Terms Act of 2017;* nne, Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji Sura 426 yaani *The Town Planners Registration CAP. 426* na tano, Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura ya 263 *(The Workers Compasation Fund Act CAP. 263).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu sita ambapo sehemu ya kwanza ya muswada inaainisha masharti kuhusu utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa na tamko la marekebisho ya sheria mbalimbali zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho kupitia muswada huu.

Sehemu ya pili ya muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mahakama ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Sura ya 216 yaani *The Land Disputes Courts Act CAP. 216,* kifungu cha pili cha sheria hiyo kinatoa tafsiri ya maneno Halmashauri ya Wilaya yaani *District Council* kuwa ni Halmashauri ya Wilaya iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa ya Mamlaka za Wilaya Sura ya 287.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa neno hilo limetumika kutambua vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi vilivyoahidiwa katika sheria hiyo ikiwemo Baraza la Kata na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya na kwa kuwa vyombo hivi vinaweza kuanzishwa katika maeneo mengine ya kiutawala ikiwemo Miji, Manispaa na Majiji ibara ya nne inapendekeza tafasiri hiyo ifutwe na kuwekwa badala ya tafasiri ya neno Halmashauri yaani *Council* kwa lengo la kuwezesha Halmashauri ya Jiji, Manispaa na Miji ambazo zimeanzishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Miji Sura ya 288 kutambuliwa katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kuainisha kisheria kuwa Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba la Wilaya yaliyopo katika Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji yana mamlaka ya kushughulikia migogoro ya ardhi ndani ya maeneo husika ya kiutawala. Kifungu cha 10(1) cha sheria hiyo kinaweka masharti kuwa kila Baraza la Kata litakuwa na mamlaka ya kusikiliza

migogoro ya ardhi katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ambako limeanzishwa. Ibara ya tano ya muswada huu inapendekeza maneno *of the district council* yanayorejea katika kifungu hicho cha 10(1) yafutwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kuwezesha Baraza la Kata katika Halmashauri ya Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji kutambulika kisheria kuwa lina mamlaka ya kusikiliza migogoro ya ardhi katika eneo la kiutawala ambako limeanzishwa. Kifungu cha 23(1) cha sheria hiyo kinaweka masharti kuwa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya litaundwa na Mwenyekiti mmoja pamoja na washauri wasiopungua wawili. Ibara ya sita ya muswada inapendekeza maneno *one chairman* yanayorejewa katika kifungu hicho yafutwe na kuweka badala yake maneno *at least* a *chairman* ili kuweka masharti yatakayowezesha Baraza hilo kuundwa na Mwenyekiti zaidi ya mmoja pale itakapoonekana inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo kifungu hicho sasa kitasomeka kama ifuatavyo; *"The district and housing tribunal established under section 22 shall be composed at least a chairman and less than two assessors."* Marekebisho haya yanalenga kuharakisha utatuzi wa migogoro ya ardhi katika Baraza la Ardhi la Nyumba la Wilaya na kuimarisha utoaji haki katika migogoro ya ardhi.

Kifungu cha 28 cha sheria hiyo kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha pili ambacho kinaainisha masharti kuhusu sifa za mtu anayeweza kuteuliwa kuwa Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoonekana katika ibara ya 7 ya muswada sifa zinazopendekezwa ni shahada ya sheria kutoka katika chuo kinachotambulika na Serikali na uzoefu wa kazi za kisheria kwa muda usiopungua miaka kumi. Lengo la marekebisho haya ni kuweka mwongozo wa kisheria utaoisaidia mamlaka ya uteuzi wakati wa uteuzi wa Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Aidha, kufuatia mabadiliko haya vifungu vidogo vya pili, tatu na nne

sasa vitakuwa vifungu vidogo vya tatu, nne na tano kwa mfatano yaani *respectively*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho mengine katika sehemu hii yanahusu kifungu cha 33 cha sheria hiyo, ibara ya nane ya muswada kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kwamba mamlaka ya kifedha yaani *Pecuniary Jurisdiction* ya Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya yaongezwe kutoka kiasi kisichozidi shilingi milioni 50 hadi kiasi kisichozidi milioni 300 kwa mali zisizohamishika na kutoka kiasi kisichozidi shilingi milioni 40 hadi kiasi kisichozidi shilingi milioni 200 kwa mali zinazoweza kuthaminika kwa viwango vya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ibara ya tisa ya muswada kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 37 cha sheria hiyo kwa kuongeza ukomo wa mamlaka wa kifedha Mahakama Kuu kutoka kiasi kinachozidi shilingi milioni 50 hadi kiasi kisichozidi shilingi milioni 300 kwa mali zisizohamishika na kutoka kiasi kinachozidi shilingi milioni 40 hadi kiasi kinachozidi shilingi milioni 200 kwa mali zinazoweza kuthaminika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho katika ibara za nane na tisa za muswada ni kuongeza kasi ya utatumia ya migogoro ya ardhi kwa kuwezesha Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ambalo ndilo liko karibu zaidi na wananchi kuliko Mahakama Kuu kuwa na mamlaka zaidi ya kutatua migogoro ya ardhi yenye thamani inayopendekezwa. Pia marekebisho haya yanalenga kuianisha viwango vya mamlaka ya kifedha vya Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya na Makao Makuu na vile vya Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu vinavyotajwa katika Sheria ya Mahakama za Mahakimu Sura ya 11 *(The Magistrate Court CAP. 11)* ikizingatiwa pia kuwa rufaa au nafuu yoyote dhidi ya uwamuzi wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya au Mahakama hizo kufunguliwa Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 44 cha sheria hiyo kinaweka masharti kuhusu mamlaka yaMsajili wa Mahakama Kuu katika kufanya mapitio yaani *revision* baada ya kuitisha jalada husika kutoka Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

Ibara ya 10 ya muswada kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kuongeza kifungu kidogo kipya cha tatu kinachoweka masharti kuwa Mahakama Kuu itatakiwa kurejesha jalada husika katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ndani ya siku 14 baada ya kutoa amri ya mapitio husika. Marekebisho haya yanalenga kupunguza ucheleweshwaji wa kusikiliza mashauri ya ardhi kwa kuainisha muda ambao Mahakama Kuu intakiwa kurejesha majalada yanayoitishwa kwa ajili ya kufanya marejeo ili shauri husika liendelee kwa mujibu wa marejeo yaliyofanywa na Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 55 cha sheria kinaainisha masharti kuwa Mwenyekiti, Wajumbe, Maafisa, Watumishi na Mawakala wa Mabaraza ya Ardhi na Vijiji au Mabaraza hawatawajibika binafsi kwa jambo waliolitenda kwa nia njema wakti wakitekeleza wajibu wao. Ibara ya 11 ya muswada inapendekeza kifungu hicho kifutwe na kuandikwa upya kwa lengo la kufafanua zaidi kuwa Baraza linalotajwa katika sheria ya sasa ni Baraza la Kata, Baraza la Ardhi na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya. Kwa msingi huo, marekebisho haya yatawezesha wenyeviti, wajumbe, maafisa watumishi na mawakala wa Baraza la Ardhi la kijiji, Baraza la Kata na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya kutekeleza majukumu yao pasipokuwana hofu au uoga kwa kujua kuwa wana kinga kwa jambo walilolifanya kwa nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya mwisho katika sehemu hii yanahusu kifungu cha 56(2) kinachoweka masharti kuhusu kutunga kanuni. Ibara ya 12 ya Muswada inapendekeza marekebisho madogo kwa kuongeza neno *appointment* katika aya “h” na neno *chairman* katika aya “i” ili kifungu hicho kisomeke na kueleweka vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha muswada unapendekeza kuongeza aya mpya J inayompatia Waziri mwenye dhamama ya ardhi mamlaka ya kutunga kanuni kuhusu utendaji wa madalali. Marekebisho haya yanalenga kumwezesha Waziri kutunga kanuni kwa ajili ya uteuzi wa Wenyeviti na Wazee wa Mabaraza, kusimamia utendaji wa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na utendaji wa Madalali wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa ajili ya utekelezaji bora wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ya muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Upimaji wa Ardhi Sura ya 324 *(The Land Survey Act, CAP. 324).* Ibara ya 14 ya muswada inapendekeza kifungu cha pili cha sheria hiyo kirekebishwe kwa kuongeza tafsiri ya maneno Mpima Ardhi wa Kanda yaani *Zonal Land Surveyor* ambaye atakuwa msimamizi wa shughuli zote za upimaji katika kanda kwa niaba ya Mkurugenzi. Lengo la marekebisho ni kuweka tafsiri ni kuweka tafsiri ya maneno haya ambayo yametumika katika sheria hiyo kupitia muswada huu na hivyo kurahisisha utekelezaji wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha tatu cha sheria hiyo kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha pili ili kuainisha masharti yatakayowezesha Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani kukasimu madaraka na mamlaka yake chini ya sheria hiyo kwampima ardhi wa kanda yaani *Zonal Land Officer.* Lengo la marekebisho haya ni kusogeza huduma za upimaji ardhi katika ngazo ya kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 4(3) cha sheria kinaweka masharti kuwa adhabu kwa mtu anayetiwa hatiani kwa kosa la kufanya kazi za mpimaji chini ya kifungu hicho ni faini isiyozidi shilingi 50,000 au kifungo kisichozidi miezi miwili au vyote. Ibara ya 16 ya muswada kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali ya Marekebisho inapendekeza adhabu kwa kosa hilo iwe faini isiyopungua shilingi 750,000 au kifungo cha mwaka mmoja au vyote kwa pamoja. Lengo la merekebisho haya ni kuweka katika sheria adhabu inayoendana na wakati ili kuwafanya watu waogope kutenda kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 6(2) cha sheria hiyo kinaweka masharti kuwa adhabu kwa mtu anayetiwahatiani kwa kosa la kupiga picha za anga *(aerial photography)*kinyume na masharti ya kifungu hicho ni faini isiyozidi shilingi 2,000. Ibara ya 17 muswada kama ulivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza adhabu kwa kosa hilo iwe faini isiyopungua shilingi milioni tano au kifungo cha miaka miwili. Lengo la marekebisho haya ni kuweka katika sheria adhabu inayoendana na wakati, kuainisha adhabu ya kifungu kwa mtu ambaye atashindwa kulipia faini na kuwafanya watu waogope kutenda kosa hilo kwani adhabu ya sasa ni ndogo sana na haimfanyi mtu kujirekebisha au kujutia kutenda kosa hilo.

Mheshimwa Mwenyekiti, kifungu 9 cha sheria hiyo kinaweka masharti kuwa adhabu ya faini kwa mtu anayetiwa hatiani kwa kosa la kuzuia wapimaji wa ardhi kutekeleza majukumu yao chini ya sheria hiyo haitazidi shilingi 50,000. Ibara ya 18 ya muswada inapendekeza adhabu hiyo ya faini isipungue shilingi 2,000,000. Lengo la marekebisho haya ni kuweka adhabu inayoendana na wakati na kuwafanya watu waogope kutenda kosa hilo kwani adhabu ya sasa ni ndogo na haimfanyi mtu kujirekebisha au kujutia kutenda kosa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 13 cha sheria hiyo kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha nne kinachoweka masharti kuhusu kutambua kisheria michoro ya upimaji na ramani iliyoandaliwa kwa njia ya kielektroniki kama inayoonekana katika Ibara ya 19 ya muswada. Aidha, Ibara ya 20 ya mudswada kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kifungu kipya cha 18A kinachompatia Mkurugenzi wa Upimaji na ramani haki ya kipekee ya kuandaa, kutengeneza na kusambaza ramani zote zinazoonesha mipaka ya mikoa na nchi. Iwapo mtu atakiuka masharti hayo, adhabu yake itakuwa faini isiyopungua shilingi 5,000,000 lakini isiyozidi shilingi milioni 10,000,000 au kifungo kisichopungua miezi sita, lakini kisichozidi miaka miwili. Lengo la marekebisho haya ni kudhibiti ramani zinazopotosha mipaka sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne ya muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mikataba ya Maliasili na Rasilimali za Nchi, Mapitio na Majadiliano ya Masharti Hasi ya mwaka 2017 *(The Natural Wealth and Resources Contracts, (Review and Renegotiation of Unconscionable Terms) Act, (Act No. 6 of 2017)* sheria ilivyo sasa haiko wazi kama madini na mafuta ni miongoni mwa maliasili na rasilimali zinazoainishwa katika tafsiri ya maneno *natural wealth and resources* iliyoko katika kifungu cha tatu cha sheria hiyo. Hivyo basi, Ibara ya 22 ya Muswada inapendekeza kifungu hicho kirekebishwe kwa kuongeza madini na mafuta kuwamiongoni mwa maliasili na rasilimali zilizoainishwa katika tafsiri ya maneno hayo *natural wealth and resources.* Lengo la marekebisho haya ni kuainisha wazi katika sheria kuwa madini na mafuta ni maliasili na rasilimali inayosimamiwa ipasavyo na masharti ya sheriahiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano ya muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji, Sura ya 426 *(The Town Planners Registration Act, (CAP. 426).* Ibara ya 24 ya muswada inapendekeza kifungu cha pili cha sheria hiyo kirekebishwe kwa kuongeza tafsiri ya maneno *foreign fame, stop order* na *town planning practice.* Maneno hayo yametumika katika sheria hiyo lakini yalikuwa hayajapewa tafsiri. Lengo la marekebisho haya ni kurahisisha utekelezaji wa sheria hiyo kutokana na maneno hayo kupatiwa tafsiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho mengine yanahusu kifungu cha nne cha sheria hiyo ambacho kinaanzisha bodi ya usajili ya wapangamiji. Ibara ya 25 ya muswada inapendekeza kuongeza kifungu kidogo kipya cha pili kinachoainisha mamlaka ya bodi hiyo ikiwemo kushtaki na kushtakiwa, kumiliki mali na kuingia mikataba kwa jina lake kwa kuwa bodi hiyo ni taasisi ya Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye mshauri mkuu wa Serikali na taasisi zake kwa masuala yote ya kisheria na kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 59(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kuwa Mwanasheria Mkuu ana haki ya kuhudhuria na kusikilizwa katika Mahakama zote katika

Jamhuri ya Muungano, muswada unaweka masharti yatakayompatia Mwanasheria Mkuu wa Serikali haki ya kuingilia kati shauri lililofunguliwa na/au dhidi ya Tume kwa kuiwakilisha bodi hiyo Mahakamani katika shauri husika pale inapoonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Aidha, Bodi imepewa wajibu wa kumfahamisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali pale inaposhtakiwa au kushtaki Mahakamani. Marekebisho haya yanalenga kulinda mali na maslahi ya Serikali katika bodi hiyo kuanzia hatua ya awali ya shauri husika.

Mheshimiwa MWenyekiti, kifungu cha 7 cha sheria hiyo kinayaainisha masharti kuhusu uteuzi wa Msajili wa Bodi ya Wapanga Miji. Ibara ya 26 ya Muswada inapendekeza kuongeza vifungu vidogo vipya vya tatu na nne katika kifungu hicho cha saba ili kuainisha majukumu na wajibu wa msajili ikiwemo kuwa Afisa Masuuli na Katibu wa Bodi na kutekeleza majukumu mengine yanayohusiana na kazi za bodi hiyo. Aidha, kifungu cha 8(2) cha sheria hiyo kinaelekeza kuwa fomu za maombi ya usajili, leseni za kufanyia kazi na usajili wa Maofisa Mipango Miji zitaainishwa katika jedwali la sheria hiyo. Ibara ya 27 ya muswada inapendekeza kifungu hicho kifutwe na kuandikwa upya ili kuweka masharti yanayoonesha kuwa fomu hizo zitaainishwa katika kanuni zinazotungwa chini ya sheriahiyo. Lengo la marekebisho hayo ni kurahisisha utekelezaji wa sheria hiyo kwa kuwezesha fomu hizo kurekebishwa kulingana na mahitaji yatakayojitokeza pasipo kulazimika kuleta muswada Bungeni kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 22 cha sheria hiyo kinarekebishwa kama inavyoonekana katika Ibara ya 28 ya muswada kwa kuongeza adhabu kwa mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa la kufanya kazi za upangaji miji bila kusajiliwa na bodi iwe faini isiyopungua shilingi 5,000,000 lakini isiyozidi shilingi 10,000,000 au kifungo kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja. Sheria ya sasa inaainisha kuwa adhabu kwa kosa hilo ni faini isiyopungua shilingi 100,000 lakini isiyozidi lakini shilingi 500,000 au kifungo kisichopungua miezi mitatu lakini kisichozidi miaka miwili. Marekebisho haya yanalenga kudhibiti makosa ya

watu kufanya kazi za upangaji miji pasipo kusajiliwa na hivyo kuimarisha upangaji miji sahihi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoonekana katika Ibara ya 29 ya muswada, kifungu cha 23 cha sheriahiyo kinarekebishwa kwakuweka masharti kuwa ili kampuni ifanye kazi za mipango miji sharti isajiliwe chini cha sheria hiyo na kwamba angalau wabia au wanahisa wake wawili wawe wamesajiliwa chini ya sheria hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa kampuni zinazofanya kazi za mipango miji zinasimamiwa ipasavyo chini ya sheria hiyo baada ya kusajiliwa. Aidha, muswada unapendekeza kuongeza adhabu ya faini kwa mtu au kampuni itakayokiuka masharti hayo kuwa faini isiyopungua shilingi 2,000,000 lakini isiyozidi shilingi 5,000,000 badala ya faini isiyopungua shilingi 300,000 lakini isiyozidi shilingi 500,000 inayotajwa katika sheria ya sasa. Adhabu hiyo inaonekana kupitwa na wakati, jambo linaloweza kusababisha kampuni kutenda kosa hilo kwa kujua kuwa itaweza kulipia faini husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada unapendekeza pia marekebisho katika kifungu cha 25 cha sheria hiyo kinachoweka masharti kuhusu makosa yanayohusiana na usajili kwa kutoa taarifa ya uongo au kufanya udanganyifu ili kusajiliwa na bodi. Ibara ya 30 ya muswada inapendekeza kuwa adhabu wa kosa hilo iwe faini isiyopungua shilingi 2,000,000 lakini isiyozidi shilingi 5,000,000 au kifungo kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja. Adhabu inayotajwa katika sheria ya sasani faini isiyopungua shilingi 100,000 lakini isiyozidi shilingi 500,000 au kifungo kisichopungua mwaka na miezi mitatu lakini kischozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha adhabu inayoendana na wakati na kuwafanya watu waogope kutenda kosa hilo kwani adhabu ya sasa ni ndogo na haimfanyi mtu kujirekebisha au kujua kutenda kosa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 31 ya muswada inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 25A kinachoipatia bodi mamlaka ya kutoa ilani ya makatazo yaani *stop order*

kwa mtu anayejenga kwa kukiuka masharti ya sheriahiyo. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha upangaji miji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 31(2) cha sheria hiyo kinarekebishwa kama inavyoonekana katika ibara ya 32 ya muswada kwa kuongeza masharti yatakayompatia Waziri mamlaka ya kutunga kanuni zitakazoainisha masuala ya ada, fomu na taratibu za usajili wa maafisa mipango miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ibara ya 33 ya Muswada inapendekeza kufutwa kwa jedwali la pili la sheria hiyo linalohusianana fomu mbalimbali ili masharti hayo yaingizwe katika kanuni zitakazotungwa na Waziri kama ilivyopendekezwa katika muswada huo. Kama nilivyoeleza awali, marekebisho haya yanalenga kurahisha utekelezaji wa sheria hiyo kwa kuwezesha fomu hizo kurekebishwa kupitia kanuni husika kulingana na mahitaji yatakayojitokeza pasipo kulazimika kuleta muswdaa Bungeni kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita ya muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263 *(The Workers Compensation Fund Act, (CAP. 263).* Ibara ya 35 ya muswada inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu cha 48(4)(b) na (c) cha sheria hiyo kwa lengo la kuweka utaratibu utakaotumika katika kufanya tathmini ya malipo ya fidia kwa mkupuo kwa mwajiriwa atakaekuwa amepata ulemavu wa kudumu chini ya asilimia 30 akiwa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibaraya 36 ya muswada kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kurekebisha aya ya kwanza ya jedwali la kwanza la sheria hiyo linaloweka masharti kuhusu muundo wa Bodi ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Inapendekezwa kuwa bodi hiyo iundwe na wajumbe wawili wanaowakilisha vyama vya waajiri vyenye wanachama wengi kwenye mfuko, wajumbe wawili wanaowakilisha vyama vya wafanyakazi vyenye wanachama wengi kwenye mfuko, Wakili wa Serikali wa kuanzia ngazi ya mwandamizi yaani *Law Officer* anayemwakilisha Mwanasheria Mkuu wa

Serikali, mwakilishi wa Wizara yenye dhamana ya Hifadhi za Jamii, mwakilishi wa Wizara yenye dhamana ya Fedha, mwakilishi wa Wizara yenye dhamana ya Utumishi wa Umma na mwakilishi wa Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu unaotokana na kuumia au ugonjwa uliotokana na kazi. Lengo la marekebisho hayani kuainisha muundo unaoendana na mifuko mingine ya hifadhi ya jamii na kuimarisha utekelezaji wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo na kwa mara nyingine tena ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maelezo ya hoja kuhusu Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa mwaka 2017 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 4 Act of 2017)* na ninaomba Bunge lako Tukufu liujadili na kuupisha katik ahatua za kusomwa kw amra ya pili na mara ya tau ili hatimae marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ahsante. Tunaendelea na Mwenyekiti wa Kmaati ya Katiba na Sheria ili aweze kuja kuwasilisha maoni ya Kamati. Karibu Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, miwngi wa rehema aliyetujaalia kukutana mbele ya Bunge lako tukufu na kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana katika Mkutano huu wa Tisa wa Bunge hili la Kumi na Moja kwa ajili ya kujadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Mwongozo

wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2017.

Mheshimiwa Spika, ninatambua pia wapo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako hili tukufu waliopewa dhamana ya utumishi katika nafasi mbalimbali za Uwaziri na Unaibu Waziri. Wote kwa pamoja naomba niwapongeze sana na kuwatakia utumishi uliotukuka katika majukumu yao mapya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Hongereni sana!

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa mwaka 2017 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.4) Act of 2017).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu baada ya kupokea kazi ya kushughulikia Muswada kutoka kwako kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu ya Bunge, Toleo la Januari 2016, ilianza kuufanyia kazi Muswada huu kwa kuainisha aina ya wadau na kuwaalika kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana kwa mara ya kwanza na Waziri wa Katiba na Sheria, tarehe 25 Oktoba, 2017 ili kupokea maelezo kuhusu Muswada husika. Aidha, baada ya maelezo ya Waziri Kamati iliendelea kukutana na Maafisa wa Sheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yake, Waziri wa Katiba na Sheria aliieleza Kamati kuwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa mwaka 2017 unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tano kwa lengo la kuondoa mapungufu yaliyobainika wakati wa

utekelezaji wa sheria hizo; kuongeza masharti mbalimbali ili kuleta uwiano kati ya sheria hizo na sheria nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa ni kama zifuatazo:-

(i) Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 *[The Land Disputes Courts Act, (CAP 216)];*

(ii) Sheria ya Upimaji wa Ardhi, Sura ya 324 *[The Land Survey Act, (CAP 324)];*

(iii) Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Rasilimali za Nchi ya Mwaka 2017, *[The Natural Wealth and Resources Contracts, (Review and Renegotiation of Unconscionable Terms) Act, (Act No 6 of 2017)];*

(iv) Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji, Sura ya 426 *[The Town Planners Registration Act, (CAP 426)];* na

(v) Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263 *[The Workers Compensation Fund Act, (CAP 263)].*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea maelezo ya Serikali, Kamati ilipokea maoni ya wadau kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Wadau walitoa maoni yao kwa mujibu wa Kanuni tajwa kuhusu vifungu mbalimbali vinavyokusudiwa kurekebishwa kwenye sheria nilizozitaja kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau wote ambao walifika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Wadao hao ni Umoja wa Vyama vya Wafanyakazi *(TUCTA),* Kituo cha Haki za Binadamu *(LHRC)* na Chama cha Watu wenye Ulemavu *(DOLASED).* Aidha, Kamati ilipokea na kufanyia kazi maoni yaliyowasilishwa kwa maandishi kutoka Chama cha Mtandao wa Watoaji Huduma za Kisheria *(TANLAP).* Michango na maelezo ya ufafanuzi kutoka kwa wadau hao vimeainishwa katika taarifa yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; ili kamati iweze kutoa maoni na ushauri mzuri kwa Bunge lako Tukufu, ilifanya uchambuzi wa kina wa muswada huu. Katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilitaka kujiridhisha na mambo mbalimbali ambayo ni muhimu kwa utungaji wa sheria bora. Kwa mfano, Kamati ilitaka kujua:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; asili ya wazo la mapendekezo ya marekebisho ya sheria hizi; mbili, sababu na athari ya tatizo linalokusudiwa kutatuliwa kwa marekebisho yanayopendekezwa; tatu, aina ya dosari inayosahihishwa kwa mapendekezo haya; nne, hali ilivyokuwa kabla ya kufanya marekebisho haya; tano, hali itakavyokuwa ikiwa Bunge litayapitisha marekebisho ya sheria yaliyomo katika muswada huu; sita, sababu za tatizo hilo na kama linaweza kutatuliwa kwa njia nyinginezo bila kurekebisha sheria hizi na saba, faida na madhara ya kurekebisha au kutokurekebisha sheria zinazopendekezwa katika muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niwasilishe katika Bunge lako tukufu, Maoni ya Kamati ambayo yametokana na uchambuzi wa Wajumbe wa Kamati katika sehemu na ibara mbalimbali za muswada na ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya Muswada inahusu mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 na inajumuisha kifungu cha 3 hadi cha 12 cha muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 4 cha muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 6 cha sheria hiyo kinachohusu tafsiri ya maneno kwa kufuta tafsiri ya neno *"District Council*" na badala yake kuweka tafsiri ya neno *"Council"*. Madhumuni ya marekebisho hayo ni kuondoa utata uliopo kwa sasa kuwa vyombo vya utatuzi wa migogoro ya Ardhi katika ngazi ya Kata na Wilaya vinatakiwa kuazishwa katika Mamlaka za Wilaya pekee

wakati ukweli ni kuwa vyombo hivyo vinaweza kuanzishwa katika Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali katika kifungu hiki kwani yatasaidia kuondoa tafsiri finyu iliyokuwepo na kupanua wigo wa tafsiri ya maeneo ya uanzishwaji wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 6 cha Muswada kinapendekeza kurekebisha Kifungu cha 23(1) cha Sheria hiyo kwa kufuta maneno *"one chairman"* yaliyopo katika Kifungu hicho na badala yake kuweka maneno "*at least a chairman*" kwa madhumuni ya kuwezesha Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya kuwa na Mwenyekiti zaidi ya mmoja pale itakapoonekana inafaa kufanya hivyo. Kamati inaunga mkono marekebisho hayo kwa kuwa ipo haja ya Sheria kutambua uhitaji wa Wenyeviti wa kutosha katika Mabaraza mbalimbali ya Ardhi nchini kwa lengo la kurahisisha utatuzi wa migogoro ya ardhi na utoaji haki kwa wakati hivyo kupunguza mlundikano wa majalada ya mashauri katika mabaraza husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 7 cha Muswada kinapendekeza kuongeza kifungu kidogo cha (2) katika kifungu cha 28 cha Sheria hiyo ili kuweka sifa za Msajili wa Mabaraza ya Nyumba na Ardhi ya Wilaya. Sifa zinazopendekezwa kuwanazo Msajili kuwa ni Shahada ya Sheria kutoka katika chuo kinachotambulika na uzoefu wa kazi usiopungua miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono marekebisho hayo kutokana na ukweli kwamba, nafasi hiyo ni nyeti kwa kuwa inahusika na usajili na usimamizi wa mabaraza yote nchini hivyo nafasi ya Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba inahitaji mtu mwenye sifa stahiki ili aweze kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 8 na cha 9 cha Muswada vinapendekeza kufanya marekebisho katika

kifungu cha 33 na 37 vya Sheria hiyo. Kifungu cha 8 kinapendekeza kurekebisha kifungu cha 33 kwa kuongeza kiwango cha ukomo wa thamani ya ardhi inayoweza kushughulikiwa na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kutoka shilingi milioni 50 mpaka shilingi milioni 100 kwa mali isiyohamishika na kutoka shilingi milioni 40 mpaka milioni 80 kwa mali inayoweza kuthaminika. Kifungu cha 9 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 37 cha sheria hiyo kwa kuongeza kiwango cha ukomo wa thamani kwa Mahakama Kuu kutoka shilingi milioni 50 mpaka kiwango ambacho si chini ya shilingi milioni 150 kwa mali isiyohamishika na kutoka shilingi milioni 40 mpaka milioni 80 kwa mali zinazoweza kuhamishika na kuthaminika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa vifungu hivi vikisomwa kwa pamoja vina mkanganyiko kuhusu ukomo wa kiwango cha ardhi inayoweza kusikilizwa katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya na ukomo wa kiwango kinachoweza kushughulikiwa na Mahakama Kuu ambapo baadhi ya viwango vimerukwa, yaani haviwezi kusikilizwa na Baraza la Ardhi la Wilaya wala Mahakama Kuu. Kamati ilitoa mapendekezo ya kurekebisha vifungu hivi ili kuziba pengo lililoachwa wazi kuhusu ukomo wa viwango hivyo. Serikali ilikubali mapendekezo hayo ya Kamati na yamezingatiwa kama ilivyoonekana katika Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 10 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 44 cha Sheria hiyo kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3) ili kuweka muda wa siku 14 ambao Msajili wa Mahakama Kuu atatakiwa kurejesha jalada katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya baada ya kubaini kasoro katika uamuzi wa Baraza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono marekebisho hayo kwani yataondoa kero ya ucheleweshwaji wa utoaji haki kwa Wananchi katika ngazi ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ambao wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu majibu ya majalada ya mashauri yao

kutoka kwa Msajili wa Mahakama Kuu, hali ambayo imekuwa ikisababisha kero miongoni mwa Wananchi na kupoteza haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa madhumuni ya kifungu hiki hayakuwasilishwa kama iliyokusudiwa kwa kuwa, hayaendani na kifungu kidogo cha 2 cha Sheria hiyo ambacho kinaeleza kuwa Msajili wa Mahakama Kuu baada kubaini mapungufu katika uamuzi wa Baraza la Ardhi na Nyumba, atalipeleka jalada Mahakama Kuu kwa ajili ya kufanyiwa mapitio *(revision).* Katika kifungu kidogo cha (3) kinachopendekezwa kinaeleza kuwa Msajili akibaini mapungufu katika uamuzi wa Baraza, atarudisha jalada katika Baraza lililotoa uamuzi. Kwa muktadha huu haiko bayana ni wakati gani Msajili atarudisha jalada katika Baraza la Ardhi na Nyumba na wakati gani Msajili atatakiwa kupeleka jalada husika katika Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipendekeza kifungu hicho kifutwe na kuandikwa upya ili kiweze kuwasilisha maudhui yaliyokusudiwa na kuondoa mkanganyiko unaojitokeza hivi sasa na kifungu kisomeke kama ifuatavyo; *"(3) Where the High Court has exercised its revision powers under subsection (2), the Registrar shall remit the file to the District Land and Housing Tribunal within 14 days from the date of the order".* Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na kukifanyia marekebbisho kifungu hicho kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa na Mheshimiwa Mawanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 11 cha Muswada kinapendekeza kufuta kifungu cha 55 cha Sheria hiyo na kukiandika upya ili kieleweke vizuri kwa kuwa kinawahusu Watendaji katika Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, Kata na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono marekebisho yanayopendekezwa na Serikali kwani ni muhimu

kwa kuwa yanabainisha masharti kuhusu kinga kwa Watendaji wa Mabaraza ya Ardhi na Vijiji, Kata ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya hivyo kuwawezesha kutekeleza majukumu yao wakiwa huru na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 12 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 56(2) cha Sheria hiyo ili kumpa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana mamlaka ya kutunga Kanuni kwa ajili ya kuwateua Wenyeviti na Wazee wa Mabaraza, Watendaji wa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na utendaji wa Madalali wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yanalenga kuweka utaratibu bora wa utekelezaji wa majukumu yao ya utumishi kwa mujibu wa Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Upimaji wa Ardhi, Sura ya 324 na inajumuisha kifungu cha 13 hadi 20 cha muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 14 cha muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 2 cha sheria hiyo kwa kuongeza tafsiri ya neno *Zonal Land Surveyor* yaani Mpima Ardhi wa Kanda tafsiri ambayo haikuwepo. Aidha, kifungu cha 3 cha sheria hiyo kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) ambacho kinamtaka Mkurugenzi wa Idara ya Ardhi na Upimaji kukasimu madaraka yake kwa Mpimaji wa Kanda. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya vifungu husika kwa kuwa yanalenga kupanua wigo wa upimaji ardhi kwa kuanzisha Ofisi ya Kanda ili kurahisisha utoaji wa huduma hiyo na kuisogeza huduma hiyo kwa wananchi. Hata hivyo Kamati ilibaini kuwa Ibara ya 14 ya Muswada imerudiwa hivyo kupendekeza kurekebisha ili Ibara ya 14 ambayo inarekebisha kifungu cha 3 cha Sheria hiyo kuwa Ibara ya 15 ya Muswada. Serikali ilikubali mapendekezo hayo ya Kamati, kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Serikali lililowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 16 cha muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 4(3) cha sheria hiyo kwa lengo la kuongeza faini kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 150,000 kwa mtu atakayefanya kazi ya kupima ardhi wakati hajaidhinishwa kufanya kazi hiyo. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwani yanalenga kudhibiti upimaji holela wa ardhi kwa kuwa unaweza kusababisha migogoro ya ardhi isiyo ya lazima katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 17 cha muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 6(2) cha sheria hiyo kwa kuongeza faini kutoka shilingi 2,000 mpaka shilingi 5,000,000 au adhabu ya kifungo cha miaka miwili kwa mtu atakayechukua picha za angani bila kupata kibali cha Mkurugenzi wa Ardhi na Upimaji. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa inawafanya watu waogope kutenda kosa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 18 cha muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 9 cha sheria hiyo ili kuongeza faini kutoka shilingi 50,000 mpaka shilingi 2,000,000 kwa mtu atakayemzuia Mkurugenzi wa Ardhi na Upimaji au Afisa aliye chini yake kutekeleza majukumu yake aliyo nayo kwa mujibu wa sheria. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yatawafanya watu waogope kutenda kosa hili na hivyo kurahisisha utendaji kazi wa maafisa hawa kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 19 cha muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 13 cha sheria hiyo kwa kuongeza kifungu kidogo cha (4) kwa madhumuni ya kuruhusu nyaraka za upimaji zilizotolewa kwa njia ya kielektroniki kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Ardhi na upimaji kama nyaraka halali kwa matumizi yoyote. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yanaenda sambamba na maendeleo pamoja na matumizi ya sayansi na teknolojia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 20 cha muswada kinapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 18A ambacho kinampa Mkurugenzi wa Ardhi na Upimaji haki ya kuandaa, kutengeneza na kusambaza ramani zote zinazoonyesha mipaka ya mikoa na nchi. Aidha, kifungu kidogo cha (2) kinatoa adhabu kwa mtu yeyote atakayekiuka Kifungu hicho kuwa atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi 50,000 lakini isiyozidi shilingi 150,000 au adhabu ya kifungo kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi kipindi cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kuwa faini inayopendekezwa na Serikali ni ndogo na hivyo Kamati inapendekeza iongezwe na kuwa faini isiyopungua shilingi 5,000,000 na isiyozidi shilingi milioni 10 au kifungo kisichopungua miezi sita, lakini kisichozidi miaka miwili. Lengo la mapendekezo hayo ni kufanya watu waogope kutenda kosa hilo kutokana na adhabu kuwa kubwa *(deterrence)*. Kamati inapendekeza kifungu kidogo cha (2) kisomeke kama ifuatavyo, "(2) *Any person who contravenes the provision of this section commits an offence and on conviction is liable to a fine not less than one million but not exceeding two million shillings or to imprisonment for a term of not less than six months but not exceeding two years."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo hayo yalikubaliwa na Serikali na kufanya marekebisho kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne ya muswada inahusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya nchi kuhusu Umiliki wa Rasilimali za nchi namba 6 ya mwaka 2017. Aidha, inajumuisha kifungu cha 21 na 22 cha Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 22 kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 3 cha Sheria hiyo kwa kurekebisha tafsiri ya neno *natural wealth and resources* ili kuongeza rasilimali za madini na mafuta

katika tafsiri hiyo. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yanalenga kuainisha wazi katika sheria kwamba madini na mafuta ni maliasili na rasilimali inatakayosimamiwa ipasavyo kwa masharti ya sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano ya muswada inahusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji, Sura ya 426 na inajumuisha kifungu cha 23 hadi 33 vya muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 24 cha muswada kinapendkeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 2 cha sheria hiyo kwa madhumuni ya kuongeza tafsiri ya maneno *a foreign firm* na *town planning practice* katika tafsiri ya maneno kwenye sheria. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yanalenga kurahisisha utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 25 cha muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 4 cha sheria hiyo kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) kwa madhumuni ya kuipa Bodi ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji mamlaka ya kisheria ya kuweza kushitaki na kushitakiwa kwa Jina lake, kumiliki na kuuza mali na kuingia katika mikataba mbalimbali, vilevile inapendekezwa kuongeza Kifungu kidogo cha (3), (4) na (5) kwa lengo la kuweka masharti ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweza kushiriki katika mashauri ambayo bodi itahusika mahakamani. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yanaweka masharti mahsusi ya utekelezaji wa Sheria hii hususan kumwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweza kusimamia maslahi ya Taifa katika mashauri yatakayofikishwa mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 26 cha muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 7 cha sheria hiyo kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3), (4) na (5) kwa madhumuni ya kuainisha majukumu ya Msajili wa Bodi ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa

yanalenga kuweka masharti ya utekelezaji bora wa Bodi ya Wapangaji Miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 27 cha muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 8 cha sheria hiyo kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) kwa kukiandika upya ili masharti ya fomu zote za usajili, leseni za kufanyia kazi na usajili, Maafisa Mipango Miji yaainishwe kwenye Kanuni na siyo Sheria kama ilivyo sasa. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali ambayo yanaweka utaratibu bora wa utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 28 cha muswada kinapendekeza kufanya marekesho katika kifungu cha 22 cha sheria hiyo ili kuongeza adhabu kwa mtu atakayepatikana na hatia kwa makosa ya kufanya kazi za Maafisa Mipango Miji bila ya kusajiliwa kutoka kiasi cha faini isiyopungua shilingi 300,000 lakini isiyozidi shilingi 500,000 au kifungo kisichozidi miaka miwili lakini kisichopungua miezi mitatu mpaka kiasi cha faini kisichopungua shilingi milioni tano lakini kisichozidi shilingi milioni 10 au kifungo kisichozidi mwaka mmoja lakini kisichopungua miezi mitatu. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa inawafanya watu waogope kutenda makosa ya jinai na kuweka udhibiti wa shughuli za upangaji wa miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 29 cha muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 23 cha sheria hiyo. Aidha, kifungu kidogo cha (1) cha sheria kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuweka masharti ya makampuni yanayofanya kazi za Mipango Miji kuwa baada ya kusajiliwa chini ya sheria hiyo na kuwa na washirika, wanachama au wanahisa wasiopungua wawili ambao wamesajiliwa kwa mujibu wa sheria hiyo. Aidha, inapendekezwa kufanya marekebisho katika kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hicho ili kuongeza adhabu ya kampuni inayokiuka masharti ya kifungu hicho kutoka faini isiyopungua shilingi 300,000 lakini isiyozidi shilingi milioni tano. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwani yanalenga kuweka usimamizi madhubuti wa

makampuni yanayofanya kazi za Mipango Miji na kuwafanya watu waogope kufanya shughuli hiyo kinyume na masharti ya Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 30 cha muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 25 cha sheria hiyo ili kuongeza adhabu kwa mtu atakayetoa taarifa za uongo kwa Msajili wa Bodi kutoka faini isiyozidi shilingi 500,000 lakini pia, isiyopungua shilingi 150,000 au zote ziende sambamba au kifungo kisichozidi miaka mitatu. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa inawafanya watu waogope kutenda kosa hili na kuifanya Bodi kuwa na taarifa sahihi na za uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 31 cha muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 25 cha sheria hiyo kwa kuongeza kifungu kipya cha 25A ili kuipa Bodi mamlaka ya kutoa ilani za katazo *(stop order)* la kutoendelea na kazi ya Mipango Miji kutokana na kukiuka taratibu na sheria. Vilevile kifungu hicho kinaweka faini kwa mtu atakayeshindwa kutii ilani hiyo. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa inawafanya watu waogope kutenda kosa na kuimarisha shughuli za upangaji miji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita na ya mwisho ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263 na inajumuisha kifungu cha 34 hadi 36 cha muswada.

Kifungu cha 35 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho ya sheria hiyo katika kifungu cha 48(4)(b) kwa kukifuta na kukiandika upya kwa madhumuni ya kuweka utaratibu utakaotumika katika kufanya tathimini ya malipo ya fidia kwa mfanyakazi atakayeumia kazini kwa kupata ulemavu wa kudumu chini ya asilimia 30 kwamba atalipwa kwa utaratibu wa malipo ya mkupuo. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa utaratibu huo utawasaidia wafanyakazi katika kukidhi mahitaji yao

wakati watakapokuwa katika hali ya ulemavu baada ya kuumia wakiwa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 36 cha muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika jedwali la kwanza kwa kufuta aya 1(b) ya jedwali na kuiandika upya kwa madhumuni ya kuainisha upya Wajumbe wa Bodi ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ambao watateuliwa na Waziri mwenye dhamana kama ifuatavyo:-

1. Wajumbe wawili wanaowakilisha Chama cha Wafanyakazi chenye uwakilishi mkubwa.

2. Wajumbe wawili wanaowakilisha Chama cha Waajiri chenye uwakilishi mkubwa.

3. Afisa Sheria wa Serikali atakayekuwa mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

4. Mwakilishi kutoka Wizara yenye dhamana ya hifadhi ya Jamii.

5. Mwakilishi kutoka Wizara ya Fedha.

6. Mwakilishi kutoka Chama cha Watu wenye Ulemavu mwenye ujuzi na uzoefu katika mambo ya kazi au hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali hasa kwa kutambua uwakilishi katika Chama cha Wafanyakazi Waliopata Ulemavu Wakiwa Kazini kwani ndiyo walengwa hasa wa mfuko huu. Hata hivyo, Kamati ilibaini kasoro katika mapendekezo ya Serikali na inapendekeza kufanya marekebisho ifuatavyo:-

(a) Kufutwa kwa maneno ya masharti ya ujuzi na uzoefu katika masuala ya kazi au hifadhi ya jamii kwa mwakilishi kutoka Chama cha Watu Wenye Ulemavu yanayoonekana katika aya ya (b)(vi) ili kuweka usawa na wajumbe wengine walioorodheshwa katika kipengele hicho

kwani sifa zao hazikuainishwa. Kipengele hicho kisomeke; *"(vi) Representantive from an association of persons with disabilities arising from work related injuries or diseases."*

(b) Kuongeza aya (c) ili kumuongeza Mkurungenzi wa Mfuko kuwa Katibu wa Bodi lengo ni kuhakikisha kuwa Bodi inakuwa na Katibu ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aya hiyo isomeke kama ifuatavyo; *"(c) The Director General of the Fund shall be the Secretary of the Board"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na kufanya marekebisho kama itakavyoonekana katika jedwali la marekebisho litakalowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kutoa kibali ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu ya Katiba na Sheria kwa weledi na umahiri wao waliouonesha wakati wa kuchambua muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. Naomba majina yao wote yaingie kwenye *Hansard* ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa nimemshukuru Mheshimiwa Spika, lakini pia nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuwa na usikivu kwa Kamati yangu. Niwapongeze Wahesnimiwa Mawaziri ambao wote Muswada huu unagusa Wizara zao kwa kushauriwa vyema na Kamati, kuridhia ushauri wa Kamati. Kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushaurika na kupokea na kuzingatia maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda nimshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wataalamu wote kutoka Ofisi ya

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ambazo zinahusika na Sheria mbalimbali zinazopendekezwa kurekebishwa kwa kutoa ufafanuzi wa kina kwa Kamati katika maeneo mbalimbali ya Muswada. Maafisa hao walifanya kazi hiyo kwa weledi na kujituma kwa lengo la kuhakikisha kwamba, Muswada huu unachambuliwa vizuri kabla ya kuletwa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuu watumishi wote wa Bunge, hususan Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati yangu. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Angelina Langisi Sanga na Makatibu wa Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndugu Dunford Mpelumbe, Ndugu Stanslaus Kagisa, Maafisa wa Idara ya Sheria ya Bunge Ndugu Maria Mdulugu, Ndugu Hawa Manzurya na Ndugu Leocardo Kapongwa na Msaidizi wa Kamati Ndugu Rahel Masima kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha kwamba taarifa hii inakamlika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NAMBA 4 YA MWAKA 2017 (THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.4) ACT, 2017 - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa nafasi ya kukutana tena katika Mkutano huu wa Tisa wa Bunge hili la Kumi na Moja kwa ajili ya kujadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/ 2017.

**Mheshimiwa Spika**, ninatambua pia wapo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu waliopewa dhamana ya Utumishi katika nafasi mbalimbali za Uwaziri na unaibu Waziri. Wote kwa pamoja ninawapongeza sana na kuwatakia Utumishi uliotukuka katika majukumu yao mapya. Hongereni sana!

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali NA. 4 wa Mwaka 2017 [The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.4) Act of 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu baada ya kupokea kazi ya kushughulikia Muswada kutoka kwako kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu ya Bunge, Toleo la Januari 2016, ilianza kuufanyia kazi Muswada huu kwa kuainisha aina ya Wadau na kuwaalika kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana kwa mara ya kwanza na Waziri wa Katiba na Sheria, tarehe 25 Oktoba, 2017 ili kupokea maelezo kuhusu Muswada husika. Aidha, baada ya maelezo ya Waziri Kamati iliendelea kukutana na Maafisa wa Sheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

**Mheshimiwa Spika**, katika maelezo yake, Waziri wa Katiba na Sheria aliieleza Kamati kuwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa Mwaka 2017, [The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.4) Act of 2017 unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Tano (5) kwa lengo la kuondoa mapungufu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo; kuongeza masharti mbalimbali ili kuleta uwiano kati ya Sheria hizo na Sheria nyingine zilizopo.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa ni kama zifuatazo:-

1. Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 *[The Land Disputes Courts Act, (CAP 216)];*

2. Sheria ya Upimaji wa Ardhi, Sura ya 324 *[The Land Survey Act, (CAP 324)]*;

3. Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Rasilimali za Nchi ya Mwaka 2017, *[The Natural Wealth and Resources Contracts, (Review and Renegotiation of Unconscionable Terms) Act, (Act No 6 of 2017)];*

4. Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji, Sura ya 426 *[The Town Planners Registration Act, (CAP 426)]; na*

5. Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263 *[The Workers Compensation Fund Act, (CAP 263)].*

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea maelezo ya Serikali, Kamati ilipokea maoni ya Wadau kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Wadau walitoa maoni yao kwa mujibu wa Kanuni tajwa kuhusu vifungu mbalimbali vinavyokusudiwa kurekebishwa kwenye Sheria nilizozitaja kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

**Mheshimwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wadau wote ambao walifika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Wadao hao ni Umoja wa Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Kituo cha Haki za Binadamu (LHRC) na Chama cha Watu wenye Ulemavu (DOLASED). Aidha, Kamati ilipokea na kufanyia kazi maoni yaliyowasilishwa kwa maandishi kutoka Chama cha Mtandao wa Watoaji Huduma za Kisheria (TANLAP). Michango na maelezo ya ufafanuzi kutoka kwa Wadau hao, vimeisaidia Kamati kwa kiasi kikubwa kuboresha Muswada huu.

## 1.1 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, ili kamati iweze kutoa maoni na ushauri mzuri kwa Bunge lako Tukufu, ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu. Katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilitaka kujiridhisha na mambo mbalimbali muhimu kwa utungaji wa Sheria bora. Kwa mfano, Kamati ilitaka kujua:-

i) Asili ya wazo la mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hizi;

ii) Sababu na athari ya tatizo linalokusudiwa kutatuliwa kwa marekebisho yanayopendekezwa;

iii) Aina ya dosari inayosahihishwa kwa mapendekezo haya;

iv) Hali ilivyokuwa kabla ya kufanya marekebisho haya;

v) Hali itakavyokuwa ikiwa Bunge litayapitisha marekebisho ya Sheria yaliyomo katika Muswada huu;

vi) Sababu za tatizo hilo na kama linaweza kutatuliwa kwa njia nyingine bila kurekebisha Sheria hizi; na

vii) Faida na madhara ya kurekebisha au kutokurekebisha Sheria zinazopendekezwa katika Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa niwasilishe katika Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ambayo yametokana na uchambuzi wa Wajumbe wa Kamati katika Sehemu na Ibara mbalimbali za Muswada na ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatiwa na Serikali.

## 2.0 SEHEMU YA PILI

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Muswada inahusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 na inajumuisha Kifungu cha 3 hadi cha 12 cha Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 4 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 2 cha Sheria hiyo kinachohusu tafsiri ya maneno kwa kufuta tafsiri ya neno ***"District Council***" na badala yake kuweka tafsiri ya neno ***"Council"***. Madhumuni ya marekebisho hayo ni kuondoa utata uliopo kwa sasa kuwa vyombo vya utatuzi wa migogoro ya Ardhi katika ngazi ya Kata na Wilaya vinatakiwa kuazishwa katika Mamlaka za Wilaya pekee wakati ukweli ni kuwa vyombo hivyo vinaweza kuanzishwa katika Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali katika Kifungu hiki kwani yatasaidia kuondoa tafsiri finyu iliyokuwepo na kupanua wigo wa tafsiri ya maeneo ya uanzishwaji wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba Nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 6 cha Muswada kinapendekeza kurekebisha Kifungu cha 23(1) cha Sheria hiyo kwa kufuta maneno ***"one chairman"*** yaliyopo katika Kifungu hicho na badala yake kuweka maneno "***at least a chairman"*** kwa madhumuni ya kuwezesha Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya kuwa na Mwenyekiti zaidi ya Mmoja pale itakapoonekana inafaa kufanya hivyo.
Kamati inaunga mkono Marekebisho hayo kwa kuwa ipo haja ya Sheria kutambua uhitaji wa Wenyeviti wa kutosha katika Mabaraza mbalimbali ya Ardhi nchini kwa lengo la kurahisisha utatuzi wa migogoro ya Ardhi na utoaji haki kwa wakati hivyo kupunguza mlundikano wa majalada ya mashauri katika Mabaraza husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 7 cha Muswada kinapendekeza kuongeza Kifungu kidogo cha (2) katika Kifungu cha 28 cha Sheria hiyo ili kuweka sifa za Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Sifa zinazopendekezwa Msajili kuwa nazo ni Shahada ya Sheria kutoka katika chuo kinachotambulika na uzoefu wa kazi usiopungua Miaka Kumi (10).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaunga mkono marekebisho hayo kutokana na ukweli kwamba, nafasi hiyo ni nyeti kwa

kuwa inahusika na usajili na usimamizi wa Mabaraza yote nchini hivyo nafasi ya Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba inahitaji Mtu mwenye sifa stahiki ili aweze kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 8 na cha 9 cha Muswada vinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 33 na 37 vya Sheria hiyo. Kifungu cha 8 kinapendekeza kurekebisha Kifungu cha 33 kwa kuongeza kiwango cha ukomo wa thamani ya Ardhi inayoweza kushughulikiwa na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kutoka Shilingi Milioni Hamsini mpaka Shilingi Milioni Mia Moja kwa mali isiyohamishika na kutoka Shilingi Milioni Arobaini mpaka Milioni Themanini kwa mali inayoweza kuthaminika.

Kifungu cha 9 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 37 cha Sheria hiyo kwa kuongeza kiwango cha ukomo wa thamani kwa Mahakama Kuu kutoka Shilingi Milioni Hamsini mpaka kiwango ambacho si chini ya Shilingi Milioni Mia Moja na Hamsini kwa mali isiyohamishika na kutoka Shilingi Milioni Arobaini mpaka Milioni Themanini kwa mali zinazoweza kuhamishika na kuthaminika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa vifungu hivi vikisomwa kwa pamoja vina mkanganyiko kuhusu ukomo wa kiwango cha Ardhi inayoweza kusikilizwa katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya na ukomo wa kiwango kinachoweza kushughulikiwa na Mahakama Kuu ambapo baadhi ya viwango vimerukwa yaani haviwezi kusikilizwa na Baraza la Ardhi la Wilaya wala Mahakama Kuu. Kamati ilitoa mapendekezo ya kurekebisha vifungu hivi ili kuziba pengo lililoachwa wazi kuhusu ukomo wa viwango hivyo.

Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na yamezingatiwa kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 10 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 44 cha Sheria hiyo kwa kuongeza Kifungu kidogo cha (3) ili

kuweka muda wa Siku Kumi na Nne (14) ambao Msajili wa Mahakama Kuu atatakiwa kurejesha jalada katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya baada ya kubaini kasoro katika uamuzi wa Baraza hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaunga mkono marekebisho hayo kwani yataondoa kero ya ucheleweshaji utoaji haki kwa Wananchi katika ngazi ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ambao wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu majibu ya majalada ya mashauri yao kutoka kwa Msajili wa Mahakama kuu , hali ambayo imekuwa ikisababisha kero miongoni mwa Wananchi na kupoteza haki zao.

**Mheshimiwa Spika.**, hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa Madhumuni ya kifungu hiki hayakuwasilishwa kama iliyokusudiwa kwa kuwa hayaendani na Kifungu kidogo cha 2 cha Sheria hiyo ambacho kinaeleza kuwa Msajili wa Mahakama Kuu baada kubaini mapungufu katika uamuzi wa Baraza la Ardhi na Nyumba, atalipeleka jalada Mahakama Kuu kwa ajili ya kufanyiwa mapitio (revision). Katika Kifungu kidogo cha 3 kinachopendekezwa kinaeleza kuwa Msajili akibaini mapungufu katika uamuzi wa Baraza, atarudisha jalada katika Baraza lililotoa uamuzi. Kwa muktadha huu haiko bayana ni wakati gani Msajili atarudisha jalada katika Baraza la Ardhi na Nyumba na wakati gani Msajili atatakiwa kupeleka jalada katika Mahakama Kuu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipendekeza Kifungu hicho kifutwe na kuandikwa upya ili kiweze kuwasilisha Maudhui yaliyokusudiwa na kuondoa mkanganyiko unaojitokeza hivi sasa na Kifungu kisomeke kama ifuatavyo:-

"(3) **Where the High Court has exercised its revision powers under subsection (2), the Registrar shall remit the file to the District Land and Housing Tribunal within 14 days from the date of the order**".

Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na kukifanyia marekebbisho Kifungu hicho kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho la Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 11 cha Muswada kinapendekeza kufuta Kifungu cha 55 cha Sheria hiyo na kukiandika upya ili kieleweke vizuri kwa kuwa kinawahusu Watendaji katika Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, Kata na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaunga mkono marekebisho yanayopendekezwa na Serikali kwani ni muhimu kwa kuwa yanabainisha masharti kuhusu kinga kwa Watendaji wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, Kata na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya hivyo kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa uhuru na ufanisi.

Kifungu cha 12 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 56(2) cha Sheria hiyo ili kumpa Waziri mwenye dhamana Mamlaka ya kutunga Kanuni kwa ajili ya kuwateua Wenyeviti na Wazee wa Mabaraza, utendaji wa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na utendaji wa Madalali wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yanalenga kuweka utaratibu bora wa utekelezaji majukumu ya Watumishi hao kwa mujibu wa Sheria hii.

## 3.0 SEHEMU YA TATU

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tatu ya Muswada inahusu marekebisho ya Sheria ya Upimaji wa Ardhi, Sura ya 324 na inajumuisha Kifungu cha 13 hadi 20 cha Muswada.

Kifungu cha 14 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 2 cha Sheria hiyo kwa kuongeza tafsiri ya neno ***"Zonal Land Surveyor"*** yaani Mpima Ardhi wa Kanda tafsiri ambayo haikuwepo.

Aidha, Kifungu cha 3 cha Sheria hiyo kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza Kifungu kidogo cha (2) ambacho kinamtaka Mkurugenzi wa Idara ya Ardhi na Upimaji kukasimu Madaraka yake kwa Mpima Ardhi wa Kanda.

Kamati inaunga mkono Mapendekezo ya vifungu husika kwa kuwa yanalenga kupanua wigo wa Wapimaji Ardhi kwa kuanzisha Ofisi ya Kanda ili kurahisisha utoaji wa huduma hiyo na kuisogeza huduma hiyo kwa Wananchi. Hata hivyo Kamati ilibaini kuwa namba ya Ibara ya 14 ya Muswada imerudiwa hivyo kupendekeza kurekebisha ili Ibara ya 14 ambayo inarekebisha Kifungu cha 3 cha Sheria kuwa Ibara ya 15 ya Muswada. Serikali ilikubali mapendekezo hayo na kurekebisha kama inavyoonekana katika jedwali la Serikali la marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 16 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 4(3) cha Sheria hiyo kwa lengo la kuongeza faini kutoka Shilingi Hamsini Elfu mpaka Shilingi Mia Saba Hamsini Elfu kwa Mtu atakayefanya kazi ya kupima Ardhi wakati hajaidhinishwa kufanya kazi hiyo.

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwani yanalenga kudhibiti upimaji holela wa Ardhi kwa kuwa unaweza kusababisha migogoro ya Ardhi isiyo ya lazima katika jamii.

Kifungu cha 17 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 6(2) cha Sheria hiyo kwa kuongeza faini kutoka Shilingi Elfu Mbili mpaka Shilingi Milioni Tano au adhabu ya Kifungo cha Miaka Miwili kwa Mtu atakayechukua picha za angani bila kupata kibali cha Mkurugenzi wa Ardhi na Upimaji .

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa inawafanya Watu waogope kutenda kosa hili

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 18 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 9 cha Sheria hiyo ili kuongeza faini kutoka Shilingi Elfu Hamsini mpaka Shilingi Milioni Mbili kwa Mtu atakayemzuia Mkurugenzi wa Ardhi na Upimaji au Afisa aliye chini yake kutekeleza majukumu yake aliyo nayo kwa mujibu wa Sheria

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yatawafanya Watu waogope kutenda kosa hili na hivyo kurahisisha utendaji kazi wa Maafisa hawa kwa manufaa ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 19 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 13 cha Sheria hiyo kwa kuongeza Kifungu kidogo cha (4) kwa madhumuni ya kuruhusu nyaraka za upimaji zilizotolewa kwa njia ya kielektroniki kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Ardhi na upimaji kama nyaraka halali kwa matumizi yoyote.

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yanaenda sambamba na maendeleo pamoja na matumizi ya Sayansi na Teknolojia nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 20 cha Muswada kinapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 18A ambacho kinampa Mkurugenzi wa Ardhi na Upimaji haki pekee ya kuandaa, kutengeneza na kusambaza Ramani zote zinazoonyesha Mipaka ya Mikoa na Nchi. Aidha, Kifungu kidogo cha (2) kinatoa adhabu kwa Mtu yeyote atakayekiuka Kifungu hicho kuwa atatakiwa kulipa faini isiyopungua Shilingi Elfu Hamsini lakini isiyozidi Shilingi Mia Moja Hamsini Elfu au adhabu ya kifungo si chini ya Miezi Sita lakini kisichozidi Mwaka Mmoja.

Kamati ina maoni kuwa, faini inayopendekezwa na Serikali ni ndogo na hivyo Kamati ilipendekeza iongezwe na kuwa faini isiyopungua Milioni Tano na isiyozidi Milioni Kumi au kifungo kisichopungua Miezi Sita lakini kisichozidi Miaka Miwili. Lengo la mapendekezo hayo ni kufanya Watu waogope kutenda kosa hilo kutokana na adhabu kuwa kubwa (Deterrence). Kamati inapendekeza Kifungu kidogo cha (2) kisomeke:-

**"(2)** *Any person who contravenes the provision of this section commits an offence and on conviction is liable to a fine not less than One Million but not exceeding Two Million Shillings or to imprisonment for a term of not less than Six Months but not exceeding Two Years.*

Mapendekezo hayo yalikubaliwa na Serikali na kufanya marekebisho kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho lililowasilishwa na Serikali.

## 4.0 SEHEMU YA NNE:

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Nne ya Muswada inahusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Rasilimali za Nchi Namba 6 ya Mwaka 2017. Aidha, inajumuisha Kifungu cha 21 na 22 cha Muswada.

Kifungu cha 22 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 3 cha Sheria hiyo kwa kurekebisha tafsiri ya neno ***"natural wealth and resources"*** ili kuongeza Rasilimali za Madini na Mafuta katika tafsiri hiyo.

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yanalenga kuainisha wazi katika Sheria kwamba Madini na Mafuta ni Maliasili na Rasilimali inayosimamiwa ipasavyo kwa masharti ya Sheria hii.

## 5.0 SEHEMU YA TANO:

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tano ya Muswada inahusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji, Sura ya 426 na inajumuisha Kifungu cha 23 hadi 33 vya Muswada.

Kifungu cha 24 cha Muswada kinapendkeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 2 cha Sheria hiyo kwa madhumuni ya kuongeza tafsiri ya maneno ***"a foreign firm' na 'town planning practice"*** katika tafsiri ya maneno kwenye Sheria.

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yanalenga kurahisisha utekelezaji wa Sheria hii

Kifungu cha 25 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 4 cha Sheria hiyo kwa kuongeza Kifungu kidogo cha (2) kwa madhumuni ya kuipa

Bodi ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji Mamlaka ya Kisheria ya kuweza kushitaki na kushitakiwa kwa Jina lake, kumiliki na kuuza mali na kuingia katika Mikataba mbalimbali, Vile vile inapendekezwa kuongeza Kifungu kidogo cha (3) , (4) na (5) kwa lengo la kuweka masharti ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweza kushiriki katika mashauri ambayo Bodi itahusika Mahakamani.

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yanaweka masharti mahsusi ya utekelezaji wa Sheria hii hususan kumwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweza kusimamia maslahi ya Taifa katika mashauri yatakayofunguliwa Mahakamani.

Kifungu cha 26 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 7 cha Sheria hiyo kwa kuongeza Kifungu kidogo cha (3), (4) na (5) kwa madhumuni ya kuainisha majukumu ya Msajili wa Bodi ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji.

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yanalenga kuweka masharti ya utekelezaji bora wa Bodi ya wapangaji Miji.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 27 cha Mswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 8 cha Sheria hiyo kwa kufuta Kifungu kidogo cha (2) na kukiandika upya ili masharti ya Fomu zote za Usajili, Leseni za kufanyia kazi na Usajili wa Maafisa Mipango Miji yaainishwe kwenye Kanuni na siyo katika Sheria kama ilivyo sasa.
Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali ambayo yanaweka utaratibu bora wa utekelezaji wa Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 28 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekesho ya Kifungu cha 22 cha Sheria hiyo ili kuongeza adhabu kwa Mtu atakayepatikana na hatia kwa makosa ya kufanya kazi za Maafisa Mipango Miji bila ya kusajiliwa kutoka kiasi cha faini kisichopungua Shilingi Mia Tatu Elfu lakini isiyozidi Shilingi Mia Tano Elfu au kifungo kisichozidi Miaka Miwili lakini kisichopungua Miezi

Mitatu mpaka kiasi cha faini kisichopungua Shilingi Milioni Tano lakini kisichozidi Shilingi Milioni Kumi au kifungo kisichozidi Mwaka Mmoja lakini kisichopungua Miezi Mitatu.

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa inawafanya Watu waogope kutenda kosa hili na kuweka udhibiti wa shughuli za upangaji wa Miji.

Kifungu cha 29 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 23 cha Sheria hiyo. Aidha Kifungu kidogo cha (1) cha Sheria kinapendekezwa kufutwa na kukiandika upya ili kuweka masharti kwa Kampuni inayofanya kazi za Mipango Miji kuwa baada ya kusajiliwa chini ya Sheria hiyo na kuwa na Washirika, Wanachama au Wanahisa wasiopungua Wawili ambao wamesajiliwa kwa mujibu wa Sheria hiyo. Aidha, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Kifungu kidogo cha (4) cha Kifungu hicho ili kuongeza adhabu kwa Kampuni itakayokiuka masharti ya Kifungu hicho kutoka faini isiyopungua Shilingi Mia Tatu Elfu lakini isiyozidi Shilingi Mia Tano Elfu mpaka faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili lakini isiyozidi Shilingi Milioni Tano.

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwani yanalenga kuweka usimamizi madhubuti wa Makampuni yanayofanya kazi za Mipango Miji na kuwafanya Watu waogope kufanya shughuli hiyo kinyume na masharti ya Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 30 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 25 cha Sheria hiyo ili kuongeza adhabu kwa Mtu atakayetoa taarifa za uongo kwa Msajili wa Bodi kutoka faini isiyozidi Shilingi Mia Tano Elfu lakini isiyopungua Shilingi Mia Moja Elfu au kifungo kisichozidi Miaka Miwili jela lakini kisichopungua Miezi Mitatu au faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili lakini isiyozidi Shilingi Milioni Tano au kifungo kisichopungua Mwaka Mmoja lakini kisichozidi Miaka Mitatu jela.
Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa inawafanya Watu waogope kutenda kosa hili na kuifanya Bodi kuwa na taarifa sahihi na za uhakika.

Kifungu cha 31 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 25 cha Sheria hiyo kwa kuongeza Kifungu kipya cha 25A ili kuipa Bodi Mamlaka ya kutoa ilani ya katazo *(stop order)* la kutoendelea na kazi ya Mipango Miji kutokana na kukiuka taratibu na Sheria. Vilevile kifungu hicho kinaweka faini kwa Mtu atakayeshindwa kutii ilani hiyo.

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa inawafanya Watu waogope kutenda kosa hili na kuimarisha shughuli za upangaji Miji nchini

## 6.0 SEHEMU YA SITA

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Sita na ya mwisho ya Muswada inahusu Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263 na inajumuisha Kifungu cha 34 hadi 36 cha Muswada.

Kifungu cha 35 cha Muswada kinapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria hiyo katika Kifungu cha 48(4)(b) kwa kukifuta na kukiandika upya kwa madhumuni ya kuweka utaratibu utakaotumika katika kufanya tathimini ya malipo ya fidia kwa mfanyakazi atakayeumia kazini na kupata ulemavu wa kudumu chini ya asilimia Thelathini kwamba atalipwa kwa utaratibu wa malipo ya mkupuo.

Kamati inaunga mkono Mapendekezo ya Serikali kwa kuwa utaratibu huo utawasaidia wafanyakazi katika kukidhi mahitaji yao wakati watakapokuwa katika hali ya ulemavu baada ya kuumia akiwa kazini.

Kifungu cha 36 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Jedwali la kwanza kwa kufuta aya 1(b) ya Jedwali na kuiandika upya kwa madhumuni ya kuainisha upya Wajumbe wa Bodi ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ambao watateuliwa na Waziri mwenye dhamana kama ifuatavyo:-

1. Wajumbe Wawili wanaowaklisha Chama cha Wafanyakazi chenye uwakilishi mkubwa;

2. Wajumbe Wawili wanaowakilisha Chama cha Waajiri chenye uwakilishi mkubwa;

3. Afisa Sheria wa Serikali atakaye mwakilisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

4. Mwakilishi kutoka Wizara yenye dhamana ya hifadhi ya Jamii;

5. Mwakilishi kutoka Wizara ya Fedha; na

6. Mwakilishi kutoka Chama cha Watu wenye Ulemavu mwenye ujuzi na uzoefu katika mambo ya kazi au Hifadhi ya Jamii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali hasa kwa kutambua uwakilishi katika Chama cha Wafanyakazi waliopata ulemavu wakiwa kazini kwani ndiyo walengwa hasa wa Mfuko huu. Hata hivyo, Kamati ilibaini kasoro katika mapendekezo ya Serikali na inapendekeza kufanyika marekebisho yafuatavyo:-

(a) Kufutwa kwa maneno ya masharti ya Ujuzi na Uzoefu katika masuala ya Kazi au Hifadhi ya Jamii kwa mwakilishi kutoka Chama cha Watu wenye Ulemavu yanayoonekana katika aya (b) (vi) ili kuweka usawa na Wajumbe wengine walioorodheshwa katika kipengele hicho kwani sifa zao hazikuainishwa. Kipengele hicho kisomeke:-
"(vi) **Representantive from an association of persons with disabilities arising from work related injuries or diseases**."

(b) Kuongeza aya (c) ili kumuongeza Mkurungenzi wa Mfuko kuwa Katibu wa Bodi lengo ni kuhakikisha Bodi inakuwa na Katibu ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aya hiyo isomeke kama ifuatavyo:-
"**(c) The Director –General of the Fund shall be the Secretary of the Board".**

Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na kufanya marekebisho kama itakavyoonekana katika jedwali la marekebisho litakalowasilishwa na Serikali.

## 7.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kutoa kibali ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa weledi na umahiri wao waliouonyesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. **Naomba Majina ya Wajumbe wote walioshiriki katika Uchambuzi wa Muswada huu yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (HANSARD).**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ally Saleh Ally, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Seif Ungando Ally, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Anna Joram Girdaya, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb - Mjumbe

21. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Juma Kombo Hamad, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Zainabu Mndolwa Amiri, Mb - Mjumbe
24. Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**,vilevile napenda kuwashukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wataalamu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ambazo zinahusika na Sheria mbalimbali zinazopendekezwa kurekebishwa kwa kutoa ufafanuzi wa kina kwa Kamati katika maeneo mbalimbali ya Muswada. Maafisa hao walifanya kazi hiyo kwa weledi na kujituma kwa lengo la kuhakikisha Muswada huu unachambuliwa vizuri kabla ya kuletwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuu Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge Ndg. Stephen. N. Kagaigai kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Husein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina Langisi Sanga na Makatibu wa Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndg. Dunford Mpelumbe, Ndg. Stanslaus Kagisa, Maafisa wa Idara ya Sheria ya Bunge Ndg. Maria M. Mdulugu, Ndg, Hawa S. Manzurya na Ndg. Leocardo E. Kapongwa), na Msaidizi wa Kamati Ndg. Rahel Masima, kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamlika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**
**KATIBA NA SHERIA**
15 Novemba, 2017

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria. Sasa tunakaribisha maoni ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Uoinzani Bungeni, Mheshimiwa Bobali. Karibu Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara hii, Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu na naibu wake Mheshimiwa Abdallah Mtolea, natumia Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani Kuhusu hoja iliyo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa maoni hayo naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa upendo na fadhila zake ambazo kwa kumjaalia Mheshimiwa Tundu Lissu, Waziri Kivuli wa Wizara hii na Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani uhai hata baada ya watu ambao walitaka kutoa uhai wake tarehe 7 Septemba, 2017 katika makazi yake yaliyoko *Area D* Mjini Dodoma. Tukio la kushambuliwa na watu wanaoitwa “wasiojulikana” ni ya kulaaniwa na kila mpenda haki na anayeheshimu misingi, utu, demkorasia na haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote wanaoshindwa kujibu hoja hukimbilia kutumia mtutu wa bunduki badala ya kujirekebisha na au kujibu hoja kwa hoja. Ni wazi kuwa waliomshambulia Mheshimiwa Tundu Lissu ni waoga *(cowards)* na wenye hatia na wasioweza kujibu hoja ambazo amekuwa akisimamia kwa muda mrefu katika Taifa letu. Tukiruhusu na kuendelea kufumbia macho matukio haya hakutakuwa na namna nyingine zaidi ya kuathiri amani na utulivu nchini.

Kambi Rasmi ya Upinzani inalitaka Jeshi la Polisi na vyombo vyote vinavyotoa haki nchini kuhakikisha kuwa waliomshambulia Mheshimiwa Lissu wanakamatwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali namba 4A Juzuu ya 98 tarehe 24 Agosti, 2017. Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tano ambazo ni Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura 2016, Sheria ya Upimaji wa Ardhi, Sura 324, Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Rasilimali za Nchi ya mwaka 2017, Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji, Sura 426 pamoja na Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura 263.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeeleza kuwa madhumuni ya marekebisho ya sheria hizi ni kuondoa upungufu ambao umebainika wakati wa kutekeleza masharti ya Sheria hizi pamoja na kuongeza ufanisi kwa taasisi zinazoguswa na sheria hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa madhumuni ya Serikali na kile wanachotegemea kukirekebisha haviendani na uhalisia hasa katika ufanisi wa taasisi ambazo zinasimamiwa na sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho. Serikali imejikita kwenye masuala madogo madogo bila kugusa kiini cha matatizo ya ufanisi katika taasisi husika kama tutakavyoeleza katika taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo kuhusu Muwada. Muswada huu kuanzia ibara ya 3 mpaka 12 zinafanyia marekebisho katika Sheria ya Utatuzi wa Migogoro. Itakumbukwa kuwa katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2016 tulieleza kukosekana kwa ufanisi katika Mabaraza ya Ardhi nchini ambapo Serikali iliahidi kufanyia kazi changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko ya wananchi kuhusu thamani ya ardhi ambayo Baraza la Ardhi la Kata limekuwa na mamlaka ya kusikiliza na kutoa uamuzi. Kifungu cha 15 cha Sheria ya Utatuzi wa Migogoro kinaweka ukomo wa shilingi milioni tatu kuwa ndio thamani ya ardhi ambayo Baraza la Ardhi la Kata litakuwa na mamlaka ya kufanya uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshawahi kueleza hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa ni lazima Serikali ipitie upya ukomo wa mamlaka ya kila Baraza ili kuendana na hali iliyopo na pia kuendana na mfumuko wa bei pamoja na thamani ya shilingi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 8 ya muswada inafanya marekebisho kifungu cha 33 ambapo kiwango cha thamani ya mali isiyohamishika na inayohamishika imeongezwa kutoka viwango vya awali vya milioni 50 kwa milioni 40 hadi milioni 100 kwa milioni 80.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji sababu za kufanya marekebisho kwenye Baraza la Ardhi la Wilaya pekee na kuacha pia kufanya hivyo kwenye Baraza la Ardhi la Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama lengo lilikuwa ni kupitia upya thamani za ardhi na mali kwenye ngazi za Mabaraza ya Ardhi, Serikali ingetakiwa pia kupendekeza marekebisho kuongeza thamani ya Baraza la Ardhi la Kata ambayo imekuwa hoja ya wananchi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kutokana pia na marekebisho yanayopendekezwa kwenye ibara ya 9 ya muswada ambapo thamani ya ardhi na mali katika ngazi ya Mahakama Kuu, Kitengo cha Ardhi na yenyewe imeongezwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuna tatizo katika marekebisho haya kwa sababu baada ya muswada huu mashauri ambayo yalitakiwa yasajiliwe Mahakama Kuu sasa yataanza kusajiliwa na kusikilizwa na Mabaraza ya Wilaya kwa mujibu wa thamani za ardhi na mali nyingine zisizohamishika kama zinavyopendekezwa kurekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kifungu cha 15 cha Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi kifanyiwe marekebisho ili kuongeza angalau thamani isiyozidi milioni 20 ili kuendana sambamba na marekebisho yaliyofanywa kwenye Baraza kwa ngazi ya Wilaya na Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mapendekezo ya Serikali yataachwa kama yalivyo basi Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya yataelemewa na mashauri na mashauri mengine baada ya kuamuliwa yataenda Mahakamani Kitengo cha Ardhi kwa ajili ya rufaa au Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa pia na malalamiko kuhusu viongozi wa vijiji katika maeneo mbalimbali nchini ambao wamekuwa wakiuza ardhi kwa wawekezaji au wananchi wengine zaidi ya kile kiwango cha ekari 50 ambacho kimewekwa kwa mujibu wa sheria. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa ingekuwa ni wakati sasa kwa Serikali angalau kuja na mapendekezo ambayo yatazuia hali hiyo kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono masuala ya kuboresha mifumo ya utoaji haki nchini ikiwemo Mabaraza ya Ardhi na kuboresha miundombinu yake ambayo pia ni sehemu ya mfumo huo. Hata hivyo suala la maamuzi ya vyombo hivyo kuheshimiwa ni jambo lingine ambalo limeendelea kuleta mjadala nchini kwa kuwa sasa maamuzi yanaweza kutolewa na Mahakama au Mabaraza ya uamuzi lakini maamuzi hayo yasiheshimiwe na kutekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kuamua kubomoa makazi ya wananchi ya Kimara mpaka eneo la *TAMCO,* Kibaha Mkoani Pwani, kumekuwa na malalamiko ya wananchi hasa maeneo ya Kimara, Luguruni na Kwembe ambapo wamedai kuwa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* imebomoa nyumba za wananchi ambao walikuwa na amri ya Mahakama ambayo ilizuia kubomoa nyumba hizo mpaka pale maombi yao yatakaposikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza mbele ya Bunge lako Tukufu sababu zilizopelekea kubomolewa kwa baadhi ya nyumba huku wakijua kuwa kuna zuio la Mahakama. Aidha Serikali ieleze Bunge lako Tukufu kuhusu kauli ambazo zimetolewa na Kiongozi Mkuu wa Serikali na Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania akielekeza kuwa wananchi wa Mwanza hawatabomolewa kwa sababu walimpa kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kujua kama huo ndio utaratibu mpya wa namna Serikali inavyofanya kazi au ni katika mwendelezo wa kuwaonea wananchi ambao walitumia haki yao kutoichagua CCM wakati wa Uchaguzi Mkuu 2015? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ardhi na Makazi tulieleza pia namna Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanavyoingilia utendaji kazi wa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi wa Wilaya. Tulieleza kuwa imefikia hatua kwa Wakuu wa Wilaya kuwaeleza wananchi kuwa wasiwasilishe kwanza malalamiko/mashauri yao kwenye Mabaraza ya Ardhi mpaka watakapowasilisha malalamiko husika kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama taifa hatutakiwi kuendekeza tabia kama hizi za kuingilia mifumo ya utoaji haki. Ni vema na ni vizuri masuala ya utoaji haki yakaheshimiwa na kufuatwa na kila mtu kwa sababu hakuna mtu ambaye yuko juu ya Sheria. Tukiacha kila mtu akajichukulia Sheria mkononi bila kuheshimu misingi ambayo tumejiwekea tutahatarisha usalama wa nchi yetu kwa sababu itazua mtanziko wa namna maamuzi ya vyombo vya utoaji haki yanavyotakiwa kufuatwa na kuheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu na ya tano ya muswada zinafanyia marekebisho Sheria ya Upimaji wa Ardhi na Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipangomiji. Pamoja na kuwa Serikali imesema kuwa inafanyia marekebisho Sheria hizi kwa ajili ya kuboresha utendaji na kuongeza ufanisi kwa taasisi zinazohusika, ni wazi kuwa sehemu hii ya muswada imejikita zaidi kwenye kurekebisha faini na adhabu za kifungo kwa wataokiuka masharti ya Sheria hizo kuliko kutatua changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa Serikali imekua ikikiri kuwa kuna changamoto na gharama kubwa sana kupima ardhi na hatimaye kutoa hati ya umiliki wa ardhi kwa mujibu wa sheria zetu. Badala ya kushughulikia changamoto husika Serikali imejikita kwenye faini na adhabu kama ambavyo imekuwa ikikumbatia kodi pekee bila kutengeneza mazingira wezeshi kwa wananchi kukuza uchumi na hatimaye kuwa rahisi kulipa kodi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walio wengi wanashindwa kukidhi gharama za upimaji na wakati mwingine hata namna ya kuhamisha umiliki wa ardhi imekuwa changamoto kubwa kwa wananchi na hivyo kupelekea wengi wao kushindwa kuwa na hati miliki ya maeneo yao. Serikali ijikite kuboresha huduma hizi na kushusha baadhi ya gharama ili iwe rahisi wananchi kutumia dhamana, majengo na kuweza kupata mikopo ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 34, 35 na 36 ya muswada inafanyia marekebisho Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kwa ajili ya kuboresha bodi ya mfuko huo pamoja na kuweka utaratibu utakaotumika katika kufanya tathmini ya malipo ya fidia kwa mkupuo kwa mwajiriwa atakayekuwa amepata ulemavu wa kudumu chini ya asilimia 30 wakati akiwa bado kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 6 Novemba, 2017 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa Mjini Bukoba, Mkoani Kagera alitangaza kuwa Serikali inatarajia kuondoa utitiri wa Mifuko ya Jamii na hivyo Serikali itaifuta mifuko yote na akapendekeza kuwa itaundwa Mifuko ya Hifadhi miwili tu kwa maana ya mfuko utakaoshughulikia watumishi wa Serikali na mwingine wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu ni mpango wa hifadhi ya jamii na hivyo haina tofauti kubwa na mifuko ya jamii iliyopo kwa sasa. Kama mpango wa Serikali ni kuleta sheria inayoenda kuanzisha mifuko miwili ya hifadhi ya jamii kama alivyotangaza Rais maana yake ni kuwa marekebisho

haya ya Serikali hayatakuwa na maana kwa sababu yatafutwa muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapinga utaratibu wa kuchangia kwenye Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi wanaoumia kazini kwa sababu badala ya kuwa mfuko huo ambao badala ya mwajiri (Serikali na waajiri wengine) kuchangia kwenye mfuko huu, wafanyakazi ndio wanaokatwa kwa ajili ya kujichangia wakiumia kazini. Ikumbukwe kuwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 wafanyakazi wa sekta binafsi walitakiwa kuchanga 1% ya mishahara na posho zao wanazolipwa kwenye mfuko na 0.5% kwa wafanyakazi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa mfumo wa uchangiaji katika mfuko huu ni wa kibaguzi kwa sababu inawabagua wafanyakazi wa sekta binafsi na wale wa umma. Aidha mfuko huu unaongeza mzigo wa makato ya mishahara kwa wafanyakazi nchini. Ikumbukwe kuwa Serikali hii toka iingie madarakani haijawahi kuongeza mishahara ya wafanyakazi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wanakatwa kodi ya lipa kadri unavyopata *(PAYE)* ambayo ni kodi ya zuio ya 9%, mchango wa Chama cha wafanyakazi (3%), mfuko wa fidia kwa wafanyakazi 0.5% au 1%, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Bima ya Afya, mikopo na taratibu zingine za kuchangiana kwenye ofisi mbalimbali. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa makato haya ni mengi mno na ukizingatia kuwa mishahara haijaongezwa hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Bunge la Kumi tulishauri na kupendekeza kupitia upya mifuko ya hifadhi ya jamii na kupunguza wingi wa mifuko hiyo. Ni dhahiri na ni muhimu mifuko hiyo kuundwa upya na kutengeneza utaratibu ambao utakuwa na tija kwa wafanyakazi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha ni muhimu uwekezaji na matumizi mengine ambayo Serikali inayafanya kwa

kutumia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iwe inafuata taratibu na sheria na pia kuhakikisha kuwa madeni ambayo Serikali inadaiwa na Mifuko yanalipwa kwa ajili ya kuhakikisha fedha za wafanyakazi zinarudishwa kwenye mifuko hiyo na kutumika kwa lengo linalotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa ni vema Serikali ikajipa muda wa kujipanga kwa ajili ya kutoa muda wa kuchambua changamoto za kisheria na baadae kuleta Muswada wa Marekebisho wa Sheria Mbalimbali ili kufanya mipango na taratibu husika kuwa kwa mujibu wa sheria. Ushauri huu unatolewa kwa sababu ni lazima Waheshimiwa Wabunge na Bunge letu kwa ujumla kuelewa kuwa bila kusoma kwa makini miswada inayobadilisha sheria mbalimbali baadae linaweza kutokea tatizo na Serikali kukimbilia kutoa kauli kuwa utaratibu husika ulipata kibali na ridhaa ya Wabunge na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi inatoa rai kwa Bunge kupitia kamati zake kuielekeza Serikali kuwasilisha pamoja na Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Sheria zote zinazobadilishwa ili kutoa nafasi kwa Wabunge kupata uelewa wa vifungu vinavyofanyiwa marekebisho, badala ya sheria mama hizo kupelekwa kwenye Kamati moja tu inayohusika na marekebisho ya sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai hii kwa sababu wakati wa Bunge la Kumi Kamati ya Bajeti ya Bunge lako Tukufu ilielekeza Serikali kuhakikisha kuwa inaleta Sheria zote zinazofanyiwa marekebisho na Muswada wa Sheria ya Fedha ili kutoa nafasi kwa Wabunge kuelewa kwa undani vifungu vinavyofanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni katika awamu ya nne ambapo Sheria ya Hifadhi ya Jamii ilifanyiwa marekebisho na Wabunge walipitisha kuondoa fao la kujitoa jambo ambalo limekuwa kilio cha muda mrefu sasa kwa wafanyakazi ambao wangependa kuchukua mafao yao na

kufanya shughuli zingine za kijamii. Wakati suala la fao la kujitoa lilipovuta hisia kali na mijadala miongoni mwa wafanyakazi wa kada mbalimbali nchini, Bunge lako lilijikuta katika lawama ya kwa nini kama mhimili ulishindwa kuona athari za marekebisho ambayo yalipendekezwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa ushauri huu utasaidia Bunge kutoa ushauri wake kwa Serikali kwa ufanisi mkubwa na kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA, MHESHIMIWA TUNDU ANTIPHAS LISSU (MB) KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA. 04) WA MWAKA 2017, YAANI THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.04) ACT, 2017 - KAMA ILIVYOWASILSIHWA MEZANI**

(Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016)

---

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali namba 4 wa mwaka, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, kabla sijaanza kutoa maoni hayo naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa upendo na fadhila zake ambazo kwa kumjaalia Mheshimiwa Tundu Lissu (Waziri Kivuli wa Wizara hii na Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani) uhai hata baada ya watu ambao walitaka kutoa uhai wake

tarehe 7 Septemba, 2017 katika makazi yake yaliyoko area D Mjini Dodoma. Tukio la kushambuliwa na watu wanaoitwa "wasiojulikana" ni ya kulaaniwa na kila mpenda haki na anayeheshimu misingi utu, demkorasia na haki za binadamu.

**Mheshimiwa Spika**, siku zote wanaoshindwa kujibu hoja hukimbilia kutumia mtutu wa bunduki badala ya kujirekebisha na au kujibu hoja kwa hoja. Ni wazi kuwa waliomshambulia Mheshimiwa Tundu Lissu ni waoga (Cowards) na wenye hatia na wasioweza kujibu hoja ambazo amekuwa akisimamia kwa muda mrefu katika taifa letu. Tukiruhusu na kuendelea kufumbia macho matukio haya hakutakuwa na namna nyingine zaidi ya kuathiri amani na utulivu nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani inalitaka Jeshi la Polisi na Vyombo vyote vinavyotoa haki nchini kuhakikisha kuwa waliomshambulia Mheshimiwa Lissu wanakamatwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria.

## 2. MAELEZO YA JUMLA KUHUSU MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali namba 4A juzuu ya 98 tarehe 24 Agosti, 2017. Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tano ambazo ni Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, sura 2016, Sheria ya Upimaji wa Ardhi, sura 324, Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Rasilimali za Nchi ya mwaka 2017, Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji, sura 426 pamoja na Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, sura 263.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeeleza kuwa madhumuni ya marekebisho ya Sheria hizi ni kuondoa upungufu ambao umebainika wakati wa kutekeleza masharti ya Sheria hizi pamoja na kuongeza ufanisi kwa Taasisi zinazoguswa na Sheria hizi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa madhumuni ya serikali na kile wanachotegemea kukirekebisha haviendani na uhalisia hasa katika ufanisi wa Taasisi ambazo zinasimamiwa na Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho. Serikali imejikita kwenye masuala

madogomadogo bila kugusa kiini cha matatizo ya ufanisi katika taasisi husika kama tutakavyoeleza katika taarifa.

## 3. MAONI NA MAPENDEKEZO KUHUSU MUSWADA

**Mheshimiswa Spika**, Muswada huu kuanzia ibara ya 3 mpaka 12 zinafanyia marekebisho katika Sheria ya Utatuzi wa Migogoro. Itakumbukwa kuwa katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani katika Mkutano wa bajeti wa mwaka 2016 tulieleza kukosekana kwa ufanisi katika Mabaraza ya Ardhi nchini ambapo Serikali iliahidi kufanyia kazi changamoto hizo.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na malalamiko ya wananchi kuhusu thamani ya ardhi ambayo Baraza la Ardhi la Kata limekuwa na mamlaka ya kusikiliza na kutoa uamuzi. Kifungu cha 15 cha Sheria ya Utatuzi wa migogoro kinaweka ukomo wa Shilingi milioni tatu kuwa ndio thamani ya ardhi ambayo Baraza la Ardhi la Kata litakuwa na mamlaka ya kufanya uamuzi.

**Mheshimiwa Spika**, tumeshawahi kueleza hapa mbele ya Bunge lako tukufu kuwa ni lazima Serikali ipitie upya ukomo wa mamlaka ya kila Baraza ili kuendana na hali iliyopo na pia kuendana na mfumuko wa bei pamoja na thamani ya shilingi nchini.

**Mheshimiwa Spika**, ibara ya 8 ya Muswada inafanya marekebisho kifungu cha 33 ambapo kiwango cha thamani ya mali isiyohamishika na inayohamishika imeongezwa kutoka viwango vya awali vya milioni 50 kwa milioni 40 hadi milioni 100 kwa milioni 80. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji sababu za kufanya marekebisho kwenye Baraza la Ardhi la Wilaya pekee na kuacha pia kufanya hivyo kwenye Baraza la Ardhi la Kata.

**Mheshimiwa Spika**, kama lengo lilikuwa ni kupitia upya thamani za ardhi na mali kwenye ngazi za Mabaraza ya Ardhi, Serikali ingetakiwa pia kupendekeza marekebisho kuongeza thamani ya Baraza la Ardhi la Kata ambayo imekuwa hoja ya wananchi kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika**, Hii ni kutokana pia na marekebisho yanayopendekezwa kwenye ibara ya 9 ya Muswada ambapo thamani ya ardhi na mali katika ngazi ya Mahakama Kuu kitengo cha ardhi na yenyewe imeongezwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuna tatizo katika maboresho haya kwa sababu baada ya muswada huu mashauri ambayo yalitakiwa yasajiliwe Mahakama Kuu sasa yataanza kusajiliwa na kusikilizwa na Mabaraza ya Wilaya kwa mujibu wa thamani za ardhi na mali nyingine zisizohamishika kama zinavyopendekezwa kurekebishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kifungu cha 15 cha Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya ardhi kifanyiwe marekebisho ili kuongeza angalau thamani isiyozidi milioni 20 ili kuendana sambamba na marekebisho yaliyofanywa kwenye Baraza kwa ngazi ya Wilaya na Mahakama Kuu kitengo cha ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, kama mapendekezo ya Serikali yataachwa kama yalivyo basi Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya yataelemewa na mashauri na mashauri mengine baada ya kuamuliwa yataenda Mahakama kitengo cha Ardhi kwa ajili ya rufaa au Mahakama ya rufaa.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa pia na malalamiko kuhusu viongozi wa Vijiji katika maeneo mbalimbali nchini ambao wamekuwa wakiuza ardhi kwa wawekezaji au wananchi wengine zaidi ya kile kiwango cha ekari 50 ambacho kimewekwa kwa mujibu wa Sheria. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa ingekuwa ni wakati sasa kwa Serikali angalau kuja na mapendekezo ambayo yatazuia hali hiyo kuendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono masuala ya kuboresha mifumo ya utoaji haki nchini ikiwemo Mabaraza ya Ardhi na kuboresha miundombinu yake ambayo pia ni sehemu ya mfumo huo. Hata hivyo suala la maamuzi ya vyombo hivyo kuheshimiwa ni jambo lingine ambalo limeendelea kuleta mjadala nchini kwa kuwa sasa maamuzi yanaweza kutolewa na Mahakama au Mabaraza

ya uamuzi lakini maamuzi hayo yasiheshimiwe na kutekelezwa na serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya serikali kuamua kubomoa makazi ya wananchi ya Kimara mpaka eneo la TAMCO Kibaha Mkoani Pwani, kumekuwa na malalamiko ya wananchi hasa maeneo ya Kimara, Luguruni na Kwembe ambapo wamedai kuwa Wakala wa Barabara (TANROAD) imebomoa nyumba za wananchi ambao walikuwa na amri ya Mahakama ambayo iliwazuia kubomoa nyumba hizo mpaka pale maombi yao yatakaposikilizwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kueleza mbele ya Bunge lako tukufu sababu zilizopelekea kubomolewa kwa baadhi ya nyumba huku wakijua kuwa kuna zuio la Mahakama. Aidha serikali ieleze Bunge lako tukufu kuhusu kauli ambazo zimetolewa na Kiongozi Mkuu wa Serikali na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akielekeza kuwa wananchi wa Mwanza hawatabomolewa kwa sababu walimpa kura.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kujua kama huo ndio utaratibu mpya wa namna Serikali inavyofanya kazi, au ni katika mwendelezo wa kuwaonea wananchi ambao walitumia haki yao kutoichagua CCM wakati wa Uchaguzi Mkuu 2015?

**Mheshimiwa Spika**, katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ardhi na Makazi tulieleza pia namna Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanavyoingilia utendaji kazi wa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi wa Wilaya. Tulieleza kuwa imefikia hatua kwa Wakuu wa Wilaya kuwaeleza wananchi kuwa wasiwasilishe kwanza malalamiko/mashauri yao kwenye Mabaraza ya Ardhi mpaka watakapowasilisha malalamiko husika kwake.

**Mheshimiwa Spika**, kama Taifa hatutakiwi kuendekeza tabia kama hizi za kuingilia mifumo ya utoaji haki. Ni vema na ni vizuri masuala ya utoaji haki yakaheshimiwa na kufuatwa na kila mtu kwa sababu hakuna mtu ambaye yuko juu ya Sheria.

Tukiacha kila mtu akajichukulia Sheria mkononi bila kuheshimu misingi ambayo tumejiwekea tutahatarisha usalama wa nchi yetu kwa sababu itazua mtanziko wa namna maamuzi ya vyombo vya utoaji haki yanavyotakiwa kufuatwa na kuheshimiwa.

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya tatu na ya tano ya Muswada zinafanyia marekebisho Sheria ya Upimaji wa Ardhi na Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipangomiji. Pamoja na kuwa Serikali imesema kuwa inafanyia marekebisho Sheria hizi kwa ajili ya kuboresha utendaji na kuongeza ufanisi kwa taasisi zinazohusika ni wazi kuwa sehemu hii ya Muswada imejikita zaidi kwenye kurekebisha faini na adhabu za kifungo kwa wataokiuka masharti ya Sheria hizo kuliko kutatua changamoto zilizopo.

**Mheshimiwa Spika**, mara kadhaa Serikali imekua ikikiri kuwa kuna changamoto na gharama kubwa sana kupima ardhi na hatimaye kutoa hati ya umiliki wa ardhi kwa mujibu wa Sheria zetu. Badala ya kushughulikia changamoto husika Serikali imejikita kwenye faini na adhabu kama ambavyo imekuwa ikikumbatia kodi pekee bila kutengeneza mazingira wezeshi kwa wananchi kukuza uchumi na hatimaye kuwa rahisi kulipa kodi za serikali.

**Mheshimiwa Spika**, wananchi walio wengi wanashindwa kukidhi gharama za upimaji na wakati mwingine hata namna ya kuhamisha umiliki wa ardhi imekuwa changamoto kubwa kwa wananchi na hivyo kupelekea wengi wao kushindwa kuwa na hati miliki ya maeneo yao. Serikali ijikite kuboresha huduma hizi na kushusha baadhi ya gharama ili iwe rahisi wananchi kutumia dhamana majengo na kuweza kupata mikopo ya kibiashara.

**Mheshimiwa Spika**, ibara ya 34, 35 na 36 ya muswada inafanyia marekebisho Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kwa ajili ya kuboresha Bodi ya mfuko huo pamoja na kuweka utaratibu utakaotumika katika kufanya tathmini ya malipo ya fidia kwa mkupuo kwa mwajiriwa

atakayekuwa amepata ulemavu wa kudumu chini ya asilimia thelathini wakati akiwa bado kazini.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 06 Novemba, 2017 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa Mjini Bukoba Mkoani Kagera alitangaza kuwa Serikali inatarajia kuondoa utitiri wa mifuko ya jamii na hivyo Serikali itaifuta mifuko yote na akapendekeza kuwa itaundwa mifuko ya hifadhi miwili tu kwa maana ya mfuko utakaoshughulikia watumishi wa Serikali na mwingine wa sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko huu ni mpango wa hifadhi ya jamii na hivyo haina tofauti kubwa na mifuko ya jamii iliyopo kwa sasa. Kama mpango wa Serikali ni kuleta Sheria inayoenda kuanzisha mifuko miwili ya hifadhi ya jamii kama alivyotangaza Rais maana yake ni kuwa marekebisho haya ya Serikali hayatakuwa na maana kwa sababu yatafutwa muda mfupi ujao.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapinga utaratibu wa kuchangia kwenye mfuko wa fidia kwa wafanyakazi wanaoumia kazini kwa sababu badala ya kuwa mfuko huo ambao badala ya mwajiri (serikali na waajiri wengine) kuchangia kwenye mfuko huu, wafanyakazi ndio wanaokatwa kwa ajili ya kujichangia wakiumia kazini. Ikumbukwe kuwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 wafanyakazi wa sekta binafsi walitakiwa kuchanga 1% ya mishahara na posho zao wanazolipwa kwenye mfuko na 0.5% kwa wafanyakazi wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa mfumo wa uchangiaji katika mfuko huu ni wa kibaguzi kwa sababu inawabagua wafanyakazi wa sekta binafsi na wale wa umma. Aidha mfuko huu unaongeza mzigo wa makato ya mishahara kwa wafanyakazi nchini, Ikumbukwe kuwa Serikali hii toka iingie madarakani haijawahi kuongeza mishahara ya wafanyakazi nchini.

**Mheshimiwa Spika**, wafanyakazi wanakatwa kodi ya *lipa kadri unavyopata* (PAYE) ambayo ni kodi ya zuio (9%),

mchango wa Chama cha wafanyakazi (03%), mfuko wa fidia kwa wafanyakazi (0.5% au 1%), mifuko ya hifadhi ya jamii, bima ya afya, mikopo na taratibu zingine za kuchangiana kwenye ofisi mbalimbali, Kambi Rasmi ya Upinzania inaona kuwa makato haya ni mengi mno na ukizingatia kuwa mishahara haijaongezwa hadi leo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Bunge la 10 tulishauri na kupendekeza kupitia upya mifuko ya hifadhi ya jamii na kupunguza wingi wa mifuko hiyo, ni dhahiri na ni muhimu mifuko hiyo kuundwa upya na kutengeneza utaratibu ambao utakuwa na tija kwa wafanyakazi nchini.

**Mheshimiwa Spika**, aidha ni muhimu uwekezaji na matumizi mengine ambayo Serikali inayafanya kwa kutumia mifuko ya hifadhi ya Jamii iwe inafuata taratibu na Sheria na pia kuhakikisha kuwa madeni ambayo Serikali inadaiwa na Mifuko yanalipwa kwa ajili ya kuhakikisha fedha za wafanyakazi zinarudishwa kwenye mifuko hiyo na kutimiza lengo linalotakiwa.

## 4. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa ni vema Serikali ikajipa muda wa kujipanga kwa ajili ya kutoa muda wa kuchambua changamoto za kisheria na baadae kuleta Muswada wa Marekebisho wa Sheria mbalimbali ili kufanya mipango na taratibu husika kuwa kwa mujibu wa Sheria. Ushauri huu unatolewa kwa sababu ni lazima Waheshimiwa Wabunge na Bunge letu kwa ujumla kuelewa kuwa bila kusoma kwa makini Miswada inayobadilisha Sheria mbalimbali baadae linaweza kutokea tatizo na Serikali kukimbilia kutoa kauli kuwa utaratibu husika ulipata kibali na ridhaa ya wabunge na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, aidha Kambi Rasmi inatoa rai kwa Bunge kupitia Kamati zake kuielekeza Serikali kuwasilisha pamoja na Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali Sheria zote zinazobadilishwa ili kutoa nafasi kwa Wabunge kupata uelewa wa vifungu vinavyofanyiwa marekebisho, badala ya

sheria mama hizo kupelekwa kwenye Kamati moja tu inayohusika na marekebisho ya sheria mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai hii kwa sababu wakati wa Bunge la kumi Kamati ya Bajeti ya Bunge lako tukufu ilielekeza Serikali kuhakikisha kuwa inaleta Sheria zote zinazofanyiwa marekebisho na Muswada wa Sheria ya Fedha ili kutoa nafasi kwa Wabunge kuelewa kwa undani vifungu vinavyofanyiwa marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano ni katika awamu ya nne ambapo Sheria ya Hifadhi ya Jamii ilifanyiwa marekebisho na Wabunge walipitisha kuondoa fao la kujitoa jambo ambalo limekuwa kilio cha muda mrefu sasa kwa wafanyakazi ambao wangependa kuchukua mafao yao na kufanya shughuli zingine za kijamii. Wakati suala la fao la kujitoa lilipovuta hisia kali na mijadala miongoni mwa wafanyakazi wa kada mbalimbali nchini, Bunge lako lilijikuta katika lawama ya kwa nini kama mhimili ulishindwa kuona athari za marekebisho ambayo yalipendekezwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa ushauri huu utasaidia Bunge kutoa ushauri wake kwa Serikali kwa ufanisi mkubwa na kwa manufaa ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

Abdallah A. Mtolea (Mb)
**K.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI NA WAZIRI KIVULI WA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA**
**15 Novemba, 2017**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bobali kwa maoni hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Sasa tunaendelea na mjadala wa jumla, tutaanza na Mheshimiwa Amina Mollel na baadae Mheshimiwa Abdallah Mtulia ataendelea.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia muswada huu wa Sheria mbalimbali ambao kwangu binafsi naona kwamba ni muswada wenye manufaa na utakwenda kutatua masuala mengi hasa kwenye suala zima la migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nimshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya. Hata inapokuja miswada hii ni katika kuhakikisha kwamba yale anayoyapigania basi kusiwepo na vipingamizi, kwa hili namshukuru sana na nazidi kumtia moyo Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu ili aweze kuwatumikia Watanzania na hasa wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na sehemu ya pili ambayo inahusu migogoro ya ardhi na mabadiliko na kama nilivyosema katika mabadiliko haya ya sheria yatakwenda kusaidia kwa kiasi kikubwa kutatua migogoro ya ardhi ambayo imekuwepo kwa muda mrefu na hasa kwa kuzingatia kwamba baadhi ya watu wametokea kwamba kudhulumiwa haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa mabaraza haya ni chachu, pamoja na kwamba yalikuwepo lakini hivi sasa kwa mujibu wa sheria hii, mabaraza haya yameboreshwa zaidi. Kwa hiyo, ni faraja kubwa sana kwa Watanzania hasa wanyonge wa maendeo mengi ya vijijini ambao watakwenda sasa kunufaika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo kubwa ambalo limenifurahisha ni kwamba tofauti na ilivyokuwa hapo awali, *file* lilikuwa likienda kwa Msajili linaweza likakaa muda mrefu sana wakati mwingine hata mwaka au miaka miwili bado halijarudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria hii mabadiliko tumeona kwamba watapewa siku 14 kwa maana hiyo katika siku hizi 14 zitasaidia sana kupunguza mlolongo wa kusubiri

muda mrefu kwa wale watu ambao wamekuwa katika matatizo haya ya migogoro ya ardhi. Na tunaona kwamba katika siku hizi 14 pia itakuwa imesaidia kwamba kama ni *file* hili kama kwa upande mwingine ataona kwamba linahitaji kwenda mbele zaidi litakwenda huko. Kwa hiyo, ule mlolongo ambao ulikuwa ni mrefu utapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kipengele kingine ambacho ni sehemu ya tatu kwamba cha upimaji wa ardhi maeneo mengi. Tumeshuhudia kwamba baadhi ya maeneo yamekuwa na vibali viwili viwili na hii ni kutokana na kwamba wakati mwingine kutokuwepo na mtu maalum ambaye anahusika ni nani hasa anayepaswa kuhakikisha kwamba anatoa vibali ili eneo hilo liweze kupimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika sheria hii mpya tumeona kwamba kutakuwa na Mpima Ardhi wa Kanda. Kwa maana hiyo kama usipokuwa na kibali maalum ambacho kitaonyesha kwamba wewe lazima upate kibali ili kuweza kupima ardhi, hutoweza kufanya hivyo tofauti na siku za nyuma na hili ndilo ambalo limechangia kwa kiasi kikubwa sana, kwa mfano watu wa mabondeni ambao wamekuwa wakibomolewa na watu hao kwa upande mwingine utakuta kwamba wanazo hati kabisa ambazo wamepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kutokana na kwamba kwa namna moja au nyingine, watu ambao walikuwa wakipima kwa upande mwingine hawakuwa na vibali maalum ambavyo walikuwa wakivipata kutoka kwa wahusika. Kwa hiyo, sheria hii naona kwamba itakwenda kutatua migogoro ambayo sio ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa hasa kwangu mimi ambacho kimekuwa ni faraja kubwa na kwa moyo wangu wa dhati kabisa naipongeza Serikali, nakupongeza sana Mwanasheria Mkuu, Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu ambao ndio wanasimamia mifuko hii ya fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili mimi ndilo ambalo ndilo limenifanya hasa nikanyanyuka kuipongeza Serikali kwa moyo

wa dhati kwa sababu sasa tunaona kabisa mbali na Rais ambaye amekuwa mfano katika awamu hii ya tano kuwashirikisha watu wenye ulemavu katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mpaka Mawaziri hivi sasa tunao ambao wana ulemavu na sisi tunaamini kwamba na siku zote nimependa kutumia mfano huu,kitanda usichokilalia huwezi kujua kunguni wake. Uwepo wa Waziri katika Baraza la Mawaziri ni chachu kwa sababu ataweza kushauri. Kwa hiyo, hapa sasa katika mfuko huu wa fidia ambako Sura 263 inayojumuisha kifungu cha 34 hadi 36 cha muswada.

Mimi nimefarijika sana kuona kwamba watu wenye ulemavu pia watashiriki katika hiyo bodi. Na hapa kwa mujibu wa maoni jinsi inavyozungumza, kwamba wawakilishi kutoka Chama cha Watu Wenye Ulemavu ingawa nakubaliana na maoni ya Kamati kwamba wanasema kusiwepo na masharti. Kama umeshasema mtu mwenye ulemavu, huyu anajua ni jinsi gani ya kuweza kuwasaidia wenzake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na itasaidia sana kwa sababu katika Vyama hivi vya Watu Wenye Ulemavu sio wote tuseme kwamba wana ujuzi huo wa masuala haya ya mifuko. Kwa hiyo kwa kuweka hapa kwamba lazima awe na ujuzi, mimi naiomba Serikali iondoe kwa sababu tayari umekwishasema ni Chama cha Watu Wenye Ulemavu, tayari hawa watu wana ujuzi mpana zaidi, wana uelewa mpana zaidi wa masuala ya watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, wataweza kuishauri vyema Serikali kuhakikisha kwamba inatenda haki na kuwasaidia wale watu ambao wamepata ulemavu katika sehemu za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba sisi wote ni walemavu watarajiwa. Na kama unavyofahamu, siku hizi ajali zimekuwa nyingi lakini hasa kwa wafanyakazi, hasa kwenye viwanda, wengi wamekuwa wakipata matatizo na wengi wametelekezwa ambapo hakuna kile ambacho kweli wanastahili kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtumie aliyekuwa mwandishi wa habari waGazeti la Habari Leo, Athumani Hamisi, kama mfano, ambaye alipata ajali wakati akienda kufanya kazi Kibiti na gari ikapinduka. Mpaka leo hii, pamoja na kwamba inawezekana Kampuni ya Serikali ndiyo inamlipa mshahara kidogo sana, lakini ni mtu ambaye amesahaulika, ana maisha magumu sana katika nchi hii. Ni mtu ambaye aliitumia taaluma yake vizuri kuhabarisha na kukosoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile leo hii kwa hali aliyoipata ambayo amekuwa ni mlemavu wa kudumu, kama hii sheria ingekuwepo ninaamini kabisa angepata fidia ambayo leo hii ingemwezesha kuishi maisha ambayo angeweza kuishi maisha tofauti kama awali alivyokuwa akifanya kazi. Lakini leo hii amesahaulika huyu mwandishi na maisha yake ni magumu sana. Ninaiomba pia Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN)* imwangalie kwa jicho la pekee kwa sababu ni mtu ambaye ameitumikia kwa muda mrefu. Imuangalie kwa jicho la pekee na hata ikibidi kwa kweli kuweza kumjenga nyumba, kwa sababu anaishi maisha magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mfuko huu mimi naona kwamba sheria hii itakwenda kuboresha na wale ambao watapata ajali katika maeneo ya kazi watafidiwa. Kwa hiyo mwakilishi kutoka katika Vyama vya Watu Wenye Ulemavu atatoa ushauri ambao utakuwa ni mwafaka, utaweza kuisadia Serikali. Ninachoomba tu ni kwamba hapa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali hebu ondoa hiki kipengele kinachosema mwenye ujuzi na uzoefu katika mambo ya kazi ya hifadhi za jamii. Ninakuomba uliondoe hili ili basi hawa watu waweze kuingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hili limekuwa ni faraja kubwa sana na ndilo ambalo limenifanya mimi nisimame kuweza kuchangia. Na kwa moyo wangu wa dhati naipongeza Serikali katika hili kuhakikisha kwamba sasa watu wenye ulemavu hawaachwi nyuma na hii ni kutokana na kuridhia hii mikataba, Sheria Na. 9 ambayo inaitaka Serikali

kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanashirikishwa katika masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tumeona sasa sio tena kwa maneno ni kwa vitendo. Kwa hiyo hili mimi nasema Serikali hongera sana na msiishie hapo, na Rais wetu nampongeza sana, imekuwa ni faraja, na ninaamini kabisa kwamba watashirikishwa katika masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo katika nchi yetu. Sisi tunasema katika maendeleo tuhakikishe kwamba hakuna anayeachwa nyuma, na mimi nafurahi kuona kwamba watu wenye ulemavu hakuna anayeachwa nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naipongeza sana Serikali, nawatakia kila la heri katika sheria hii, lakini Mwanasheria Mkuu naomba sana uzingatie hiki kipengele cha ujuzi, hebu kiondoe. Tayari huyu mtu, kwanza kuwa tu na ulemavu tayari huo ni ujuzi, ana uzoefu katika masuala ya watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, ushauri wake utakuwa ni wa busara sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kusema naiheshimu sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa sababu nilishirikiana nayo vizuri. Hata wakati nikiwa na kesi ya uchaguzi ofisi hii ilionesha uwezo mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba tunashinda kesi na tukashinda kesi. Lakini nimesikitishwa sana kuona wanaleta muswada mwepese kiasi hiki. Muswada huu umekuwa mwepesi mno, sheria ambazo zinafanyiwa marekebisho hapa zina changamoto nyingi kuliko ambazo Mwanasheria Mkuu ameamua kuja kuzifanyia marekebisho hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani amedonyodonyoa vitu vichache ndivyo amevileta vifanyiwe marekebisho wakati ndani ya sheria hizo kuna vitu vingi vyenye changamoto nyingi kwa wananchi ambavyo kama angeamua kutumia uwezo wao ule ambao mimi ninautambua wakaingia ndani kwenye miswada hii, wangetuletea vitu vizito hapa na ungeona Bunge hili limejaa kwa sababu kila Mbunge angekuwa na hoja ya kutaka kuchangia kwa sababu vitu vilivyoletwa vingekuwa vinawagusa wananchi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wamejaribu kuchukua vitu vichache, sijui ni kwa sababu gani. Hata wakati naadika hotuba hii ya Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, tumepata shida sana kwa sababu vitu vingi ambavyo tulitegemea Serikali ivilete hapa hawajavileta, wameleta vitu vyepesi, kwa faida ya nani, hiyo hatuwezi kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tu; Serikali hii ya Awamu ya Tano imekuwa ikijinasibu sana kwamba ni Serikali inayobana matumizi, Serikali ambayo inaheshimu *value for money,* lakini kwa nini hawalitendei haki Bunge hili? Kikao hiki cha leo kujadili muswada huu, *value for money* haipo kwa sababu kikao ni kikubwa lakini kinajadili kitu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kila siku anapiga kelele kwamba anakerwa na utitiri wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, amelisema hili mara kadhaa. Na Serikali hii Mawaziri, Mwanasheria Mkuu ndio watu wa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha wanaharakisha mchakato wa kupunguza hii Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili iwe michache, ama uwe mmoja au miwili ili kile kilio chake na ile kero yake iweze kuondoka. Lakini ni kwa kiasi gani katika mabadiliko haya wamesaidia kuondoa hiyo kero ambayo Mheshimiwa Rais anaipigia kelele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninaamini toka Mheshimiwa Rais ameanza kukerwa na utitiri huu wa Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii, tayari *SSRA* wameshakwenda mbali kwa maana ya kufanya *research* na kuandaa maandalizi

mbalimbali ili hilo liweze kufanyiwa kazi. Lakini muswada unaletwa leo hapa mambo hayo hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku Waheshimiwa Wabunge hapa wanapiga kelele kuhusu fao la kujitoa. Wananchi wanalalamika, kwa nini wananyimwa fursa ya kujitoa kwenye Mifuko ya Jamii, wachukue fedha zao waende wakafanye shughuli nyingine. Serikali hii ndiyo inanadi kwamba inataka kuijenga Tanzania ya viwanda, Tanzania ya viwanda inahitaji mitaji, tunasema hapa kila siku. Mtu ambaye ameshafanya kazi miaka yake kumi anaona kwamba kilichopo kwenye mifuko ya jamii akilipwa kinamtosha kufanya mtaji, kinamtosha kutengeneza kiwanda chake, kwa nini unamzuia mpaka afikishe miaka 55, miaka 55 ni muda wa uzee, muda wa kula mafao, muda wa kumpizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka fedha sasa hivi ili tuweze kuwekeza, watu hao wakifika hiyo miaka 55 wawe tayari walishakuwa matajiri, au mnataka hiyo Tanzania ya viwanda wanufaike akina nani? Kama mnataka Watanzania ndio wanufaike, wapeni mafao yao. Mnazuia fao la kujitoa kwa sababu gani? Mnataka fedha ziendelee kubaki kwenye hiyo mifuko ya jamii kwa matumizi yapi? Au ndiyo hizo huwa mnazikopa wakati wa kampeni mnatushinda sisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna changamoto nyingi sana huko kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Mifuko yenyewe hiyo inafanya uwekezaji wa hasara katika maeneo chungu nzima, hayo yote yanatokana na mapungufu ya kisheria. Tulitaka Serikali sasa iende mbali iangalie kwamba kwa sababu hizi fedha ni za wananchi, mifuko hii inakwenda kufanya uwekezaji, inapata hasara, hiyo hasara ni ya nani, kwa nini hasara inapatikana, kwa inaendelea kuwekeza katika miradi ya hasara? Hayo yote ni mapungufu ya sheria, ndiyo tulitegemea hapa Mheshimiwa *AG* aje na muswada mzito uliojaa nyama za namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio tu kwenye hiyo Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, lakini hata kwenye ile Sheria ya

Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi; kuna migogoro ya ardhi kwenye nchi hii kila kona lakini marekebisho yaliyoletwa hapa yenyewe ni machache sana. Hayatibu...

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** ...hayatibu ile migogoro, hayaendi mbali kuhakikisha kwamba tunapata sheria ambayo itakwenda kutibu migogoro...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtolea, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa ndugu yangu; marekebisho ya sheria yanayofanywa sio marekebisho ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii bali ni marekebisho ya mfuko wa fidia kwa wafanyakazi, kwa hiyo kuna tofauti kati ya hizo mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na jukumu la Waheshimiwa Wabunge ni kutunga sheria, kuwawakilisha wananchi lakini pia kuisimamia Serikali. Kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali hajaleta marekebisho ya sheria, sisi Waheshimiwa Wabunge wenyewe tunayo mamlaka ya kuleta marekebisho ya sheria kwa mujibu wa Ibara za 63 na 64 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtulia, taarifa hiyo.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naitw Mtolea na sio Mtulia. Kwa Wandengereko hayo ni majina mawili tofauti na unaweza kuwa *misleading.*

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa Mtulia pokea hiyo. Aah, Mheshimiwa Mtolea. *(Kicheko)*

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Siipokei hiyo taarifa na kwa bahati mbaya sana anayetoa taarifa hii ndio Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria ambaye...

**MWENYEKITI:** Basi endelea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** ...aliongoza vikao vya kukubali muswada huu mwepesi uweze kuja hapa Bungeni. Kwa hiyo, taarifa yake ni kutetea tu haya ambayo ninaya-*challenge* hapa. Sasa ni vizuri angemuandikia Mwanasheria Mkuu ili wakati wa kuja kujibu, ndio angeweza kuyatolea maelekezo haya ambayo anafikiri alisahau kuyaingiza kwenye hotuba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia changamoto katika uwanda mzima wa masuala ambayo yanahusu ardhi, kwamba marekebisho haya yangekwenda mbali zaidi kusaidia kutatua migogoro ya ardhi kwa upana wake, sio kwa kiwango hiki kidogo ambacho Mheshimiwa *AG* ameleta hapa. Unapofanya maboresho kwenye Baraza la Ardhi la Wilaya unaacha kugusa Baraza la Ardhi la Kata, unakuwa hujalisaidia lile Baraza kwa sababu kesi za ardhi, migogoro ya ardhi, huwezi kwenda hatua nyingine yoyote – kwenye Baraza la Wilaya au Mahakamani kama hujaanza kwenye Baraza la Ardhi la Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima unapofanya maboresho yoyote uanzie kule chini ambapo ndipo migogoro yenyewe inaporipotiwa. Kufanya marekebisho kwenye Baraza la Ardhi peke yake maana yake sasa utakwenda kurundika kesi nyingi zikakae pale Baraza la Ardhi la Wilaya halafu ziwe zinachelewa kufikiwa maamuzi, hii utakuwa bado hujawasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia Waziri wa Ardhi mwenyewe akisema kwamba wapo watu, kwa kutumia fedha zao, wamejenga kwenye viwanja vya watu. Serikali yenyewe hii imekuwa sio sikivu kwa kuheshimu misingi ya sheria hizo hizo za ardhi, wamekwenda kubomoa pale Kimara nyumba za watu ambao wengine tayari wana *stop order* ya

Mahakama. Sasa kama Serikali yenyewe ni sehemu ya kutoheshimu amri za Mahakama au Mabaraza haya ya Ardhi, nani mwingine atakwenda kuheshimu? Sio kwamba tunailaumu Serikali, tunalaumu sheria ambazo zinaacha hizo nafasi za hayo mambo kuweza kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tazama ukubwa wa eneo ambalo linachukuliwa, watu wamebomolewa ili ijengwe barabara, unajiuliza ni barabara au viwanja vya mpira, robo kilometa. Watu wamevunjiwa eneo lile ni robo kilometa, inajengwa barabara ya aina gani. Ni kweli tunahitaji ile ardhi kwa ajili ya barabara au ni kwa ajili ya kukomoana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haya yote yanaweza kutibiwa na kuwa na sheria nzuri inayomlinda mwananchi. Sio tuwe na sheria ambayo inahalalisha maovu ambayo yanaweza kufanywa na Serikali yaonekane kwamba ni halali, hapo hatuwagusi wananchi. Kwa hiyo mimi niseme kwamba tunahitaji marekebisho ambayo yatawagusa wananchi.

Mheshimiwa Menyekiti, sheria zina mapungufu makubwa, maeneo yameandikwa kabisa hapa pana mgogoro pasijengwe, lakini upande mmoja wa mlalamikiwa kwa sababu una fedha unakwenda unajenga, wananchi wanapata taabu, wananchi wanateseka. Bunge hili kwa kutumia mamlaka yetu ya kutunga sheria tuishauri Serikali ituletee sheria ambazo zitaigusa jamii ya Watanzania kwa kiasi kikubwa ili tupunguze migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtolea. Tumemaliza wachangiaji wetu wa leo sasa namkaribisha mtoa hoja aweze kuhitimisha hoja yake.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa niweze na mimi kuhitimisha hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote. Muswada huu umechangiwa ukiacha taarifa za Kamati na Upinzani Muswada huu umechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wawili, na mimi napenda kuwatambua...

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba kuchangia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, majina yalikuwepo mawili tu, tumemaliza muda wao kwa hiyo tunaendelea na mtoa hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** ...wa kwanza ni Mheshimiwa Amina Mollel na wa pili ni Mheshimiwa Abdallah Mtolea. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa jinsi ambavyo mmepata fursa ya kuushughulikia Muswada huu kupitia kwenye Kamati ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme haya wakati nahitimisha; moja ni hili ambalo amemaliza kulisema Mheshimiwa Mtolea. Tunatambua kwamba iko sheria mahususi inayotawala Mabaraza ya Kata na kama mtafahamu Mwenyekiti na Wajumbe wengine wa yale Mabaraza ya Kata sio wataalam wa sheria na Baraza lile, kusudi lake hasa ni usuluhishi. Kwa hiyo, tukitaka kufanya mabadiliko katika Sheria hii ya Mabaraza ya Kata, tunahitaji mashauriano ya kina na wananchi kwenye maeneo haya, tusije tukafanya maamuzi tu kumbe tunakwenda kuleta tatizo kubwa. Ndiyo msingi wa kwamba mabadiliko kwenye hiyo Sheria ya Mabaraza ya Kata hayapo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tukishaelewana hivyo, hii hoja kwamba tungeleta mabadiliko pia kwenye yale Mabaraza ya Kata ambayo *essentially* hasa yanatumika kwenye Serikali za Mitaa, inakuwa tena haina kichwa. Kwa hiyo, ninaomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Mheshimiwa Mchengerwa ametusaidia kwamba pia hata sisi

Waheshimiwa Wabunge, tunayo mamlaka ya kuleta miswada, lakini pia tunayo mamlaka ya kuishauri Serikali ilete miswada mkiainisha changamoto zilizopo kule. Kwa hiyo hili la Baraza la Kata linahitaji mashauriano ya ndani kati ya wananchi, kati ya Waheshimiwa Wabunge na Serikali yenyewe waangalie, je, sasa ni wakati mwafaka yale Mabaraza ya Kata nayo yawe na watendaji wanasheria, wataalam ili sasa tuwaongezee viwango?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo suala hilo haliwezi kuletwa hapa kwa muswada wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Na Muswada wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wenyewe huwa ni mahususi kwa ajili ya kushughulikia masuala ya sheria, *technically* yale ambayo vipengele vimeleta shida wakati wa utekelezaji. Lakini kwenye masuala yote yanayohitaji maamuzi makubwa ya kisera yanaletwa na muswada mahususi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa sababu hiyo, nishauri tu kwamba hata hii hoja ambayo Mheshimiwa Mtolea ameisema kwamba angetegemea kwamba ungekuja hapa muswada mahususi, mkubwa kwa ajili ya kuunganisha mifuko hii ya hifadhi ya jamii, hilo nalo lisingeweza kuletwa kwenye muswada huu kwa sababu sasa ni suala la kisera. Imekuwepo mifuko mingi, wewe mwenyewe umesema ni ya utitiri, sasa unaileta iwe pamoja, unaunganisha upi na upi na utakuja na *scheme* gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila naomba kushauri Bunge lako Tukufu kwamba katika Mkutano huu wa Bunge unaoendelea sasa, Muswada huu wa Mifuko ya Hifadhi utasomwa kwa mara ya kwanza kwenye Bunge hili, ambapo pamoja na mambo mengine, utahusika pia na hiyo hoja ambayo Mheshimiwa Mtolea ameisema ya mafao ya kujitoa, itakuwa *considered* wakati huo, kama haitakuwemo Waheshimiwa Wabunge mtaamua ninyi wenyewe hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali inafanya kazi kwa makini sana. Naomba kuwashukuru Waheshimiwa

Wabunge, ninyi kuweni tu macho muisaidie wakati mnaishauri, lakini pia mtoe ushirikiano mzuri kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ametushauri Mheshimiwa Mtolea ni linalohusu wepesi wa muswada. Naomba kushauri tena kwamba ndiyo asili ya miswada hii ya mabadiliko ya sheria mbalimbali. Mambo yote kama ungetaka muswada mkubwa unakuja na muswada mahususi, hayo ni mambo ya kisera. Lakini nasema hili zoezi la kutunga sheria ni zoezi endelevu kama ambavyo pia zoezi la kufanya marekebisho ni zoezi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Serikali yenyewe imekuwa kwa kweli pia ikichukua hatua za kufanya marekebisho kwenye sheria hizi kutokana na ushauri inayoupata kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, na haya ndiyo matokeo hata ya muswada huu ambao naona kama Waheshimiwa Wabunge wote mmeunga mkono. Lakini pia niwashauri, kama mnaweza kuleta miswada mingine kwa sababu mnayo mamlaka hayo kama ambavyo Mheshimiwa Mchengerwa ameshashauri, pia msisite kufanya hivyo. *(Makofi)*

Lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Amina Mollel kwa mchango wake mzuri na sisi tunakubaliana na mchango huo na Serikali kupitia Jedwali la Marekebisho imeshafanya marekebisho kwenye hiyo hoja ya walemevu, mlemavu mnataka awe na sifa gani tena ya elimu? Kwa hiyo tumeshaweka pale kwenye jedwali la marekebisho naomba Waheshimiwa Wabunge mtambue hili ukisoma sasa kwenye Jedwali la Marekebisho Serikali imeridhia hayo marekebisho na tumeyaweka hayo marekebisho kwenye Jedwali la Marekebisho sawa sawa na mapendekezo ya Mheshimiwa Amina Mollel.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hoja pia kuhusu kauli ya Mheshimiwa Rais. Kwanza kabla sijakwenda kwenye kauli ya Mheshimiwa Rais niseme hivi, tutofautishe Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi yaani sheria tunayoijadili leo hapa ni Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi

ambayo ndani yake inaunda Mfuko wa Fidia kwa ajili ya wafanyakazi wanaoumia kazini.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hii ni tofauti na Mifuko ya Hifadhi za Jamii yaani zile *Pension Funds,* kwa hiyo hivi vitu navyo lazima tuvitenganishe, leo tuna-*deal* tu na mfuko. Sheria ya Wafanyakazi ambayo ndani yake kuna mfuko wa fidia kwa wafanyakazi, mfanyakazi yoyote anayeumia kazini mfuko huu umsaidie, kwa hiyo lakini nimeshalisema hili kwamba sheria inayounganisha mifuko itasmwa kwa mara ya kwanza kwenye mkutano huu wa Bunge lako linaloendelea.

Sasa hii ya Mheshimiwa Rais kauli hii ya kwamba watu wa Mwanza hawatabomolewa kwasababu walimpigia kura; kwanza siamini, hilo la kwanza, lakini la pili ameisema katika *context* ipi? Sikumsikia mimi hata *context* yenyewe tuangalie maudhui ya alichokisemea hicho kitu, hapana. Mimi sikumsikia lakini pia hawezi akasema hivyo akimaanisha hivyo, hapana tuchukue *context* (maudhui) yale maudhui yake. *(Kicheko)*

Lakini mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge, ninyi ndiyo mnatunga sheria hizi muwe makini muwasaidie wananchi wenu kuzingatia hizi sheria wanapojenga na ndiyo maana tunabadilisha hizi sheria za Mipango Miji na kwenye hili la mipango miji nadhani Serikali imejisahau sana. Kama Taifa haliwezi kuendelea kama unakuwa na makazi ambayo hayakupangwa, miji ambayo haikupangwa hivi. Mipango miji na makazi yaliyopangwa vizuri ni kigezo kikubwa sana katika maendeleo na huu ubomoaji unaozungumzwa katika barabara ya Morogoro ile kwanza hiyo sheria iko tangu miaka mingi, hilo la kwanza, lakini la pili hawa watu wana taarifa wanajua waliojenga pale wanafahamu na la tatu, suala hili liko Mahakamani na watu wamekwenda Mahakamani kesi nyingine wameshindwa, wengine wameendelea...

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kwa hiyo, hili suala siyo la kuja kuletwa humu ndani. Kwa hiyo naomba kusema hilo suala, Waheshimiwa Wabunge tuwashauri wananchi wetu waishi kwa kuzingatia sheria, basi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hizi ndiyo hoja za msingi ambazo Waheshimiwa Wabunge wameshazisema na mengine nimeshayajibu.

Kwa mara nyingine tena nakushukuru sana kwa kunipa fursa mimi niweze kuhitimisha hoja hii. Naomba kuwashauri Wabunge waridhie muswada huu tuendelee hatua ya pili. Marekebisho yaliyopo kwenye muswada huu ni ya muhimu sana na tumetoa sababu zake basi naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeshaungwa mkono ahsante sana Mheshimiwa *AG* na Waheshimiwa Wabunge tusipende kutafsiri maneno Kiswahili ni tungo tata, kwa hiyo tukitafsiri tunavyotaka sisi tutaharibu maana ya mtu alichokisema. Baada ya kusema hayo tunaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima. Katibu.

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24

Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nafanya *amendment* hiyo kifungu cha 28 kisomeke; *"The principle act is amended in section 22 by deleting the phrase not exceeding five hundred thousand shillings and not less than three hundred thousand shillings"* kwa hiyo, isomeke *"not exceeding"*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Ruth Mollel kwa kufukiria kuleta mapendekezo haya lakini ukisoma msingi wa mapendekezo ya mabadiliko yaliyoko kwenye muswada ukisoma sasa kifungu chenyewe kile cha 22 (3) unaanza na *"not exceeding"* sasa katika kufanya mabadiliko sisi tumeliacha neno *'not'* liko kwenye sheria bado ila tumeanzia neno *"exceeding"* kwa hiyo kama tungekuwa tumeondoa na neno *"not"* katika Sheria yenyewe, mabadiliko anayopendekeza Mheshimiwa Ruth Mollel yangekuwa ni sahihi kabisa lakini yale maneno yapo kwahiyo tunamshukuru sana mheshimiwa Ruth Mollel.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Ruth Mollel ameridhia tunaendelea.

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 29

Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 35

**MWENYEKITI:** Kuna marekebisho ya Serikali na Mheshimiwa Ruth Mollel. Tuanze na Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimependekeza ile (b) na (c) badala ya kusema *"The employee"* isomeke *"Any employee"* kwa kufuatana pia na Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini. Ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiw Ruth Mollel kwa kuleta mapendekezo haya isipokuwa tu naomba kushauri kwamba Sheria iliyopo inatumia haya maneno *'the'* hizi *define article"the"* hizi ni *articles* sasa sifa ya hizi *articles* kwenye *grammar* ni hizi; moja, unapozungumzia kitu ambacho ni *specific* yaani tayari kinajulikana ni *specific you want to make a particular stated whatever thing.* Pili ni kwamba pale ambapo unakitaja hicho kitu kwa mara ya pili na ya tatu na kuendelea. Kwa hiyo Mheshimiwa Ruth Mollel kama angekuwa na Sheria yenyewe hii kifungu cha 48 tumesema *unemployee* kweye kifungu kidogo cha kwanza, cha pili, *unemployee* lakini sasa tunapokwenda sasa kwenye kumnufaisha huyu mtu kwenye kifungu kidogo cha nne lazima sasa tuwe *specific,* tumtaje huyu mtu ambaye ameshathibitika sasa kwamba ameumia na sasa anakwenda kulipwa ndiyo msingi wa kutumia hii *definite article* inayoitwa *"the"* kwa hiyo naomba Mheshimowa Mollel aturidhie hili nalo tupige hatua tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kwenye sheria yenyewe sheria mama imesema *"unemployee"* mimi kwa mawazo yangu nilidhani kwamba hapa tunaposema "*The employee"* ni kama tumemu-*identify* huyu mtu *employee* au ni Ruth au ni David au ni Jumanne, lakini hatujamu-*identify* bado kwamba ni nani kwa hiyo kwa *grammar* ya kiingereza nilifikiri any e*mployee* bado ina-*stand.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema yaani labda ningesema vifungu vya 48(1)(2) na (3) hapo ndipo hajawa-*identified specifically* ni nani, ni Masaju au ni mtu mwingine. Sasa kwenye kumlipa umshamtambua ni Masaju ndiyo *scheme* iliyoko kwenye kifungu kidogo cha 4 inasema; *"The compensation for permanent stability shall be paid subject to the minimum and maximum set out in the regulation made by the Minister if the employee." Scheme* yake inaanza huku juu. Kwa mfano inasema; *"Where unemployee has sustain an injury set out in second schedule..."* ambaye sasa hajulikani ni nani huyo aliyekuwa *set out!!* Ni Mheshimiwa Mwakyembe au ni Mheshimiwa nani, lakini sasa hapo umeshamtambua, *process* kifungu kidogo cha kwanza, cha pili *process* zote zimeenda, umemtambua ni fulani sasa unataka kumlipa, kwa hiyo sasa unakuwa *specific* ndiyo msingi wa matumizi ya neno *"the."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kwa mara nyingine tena Mheshimiwa Ruth aridhie hii hoja ya Serikali na japokuwa pia ndivyo hivi kifungu kama kilivyo kwenye Sheria iliyopo sasa hivi ingekuwa na makosa pia hivyo ndivyo kilivyo hata kwenye Sheria iliyopo lakini kama ingekua imeandikwa vibaya bado tungeweza kurekebisha kama hii hoja ambayo Mheshimiwa Ruth Mollel ameisema ingekuwa na maelezo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 36

**MWENYEKITI:** Kina marekebisho ya Serikali na Mheshimiwa Ruth Mollel. Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimependekeza kwamba katika hawa *board members* ambao wanateuliwa na Mheshimiwa Waziri basi tujumuishe *gender, gender* iangaliwe katika idadi ya Wajumbe waliopo ili kusudi kuwe na wanawake na wanaume kwa idadi ambayo inaridhisha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Ruth Mollel kwa kuwa *sensitive* kwenye masuala haya ya maslahi ya wanawake, lakini *gender* ni *all inclusive, is not about whatever the fair sex itself,* hata mimi ni *gender.*

Kwa hiyo ukisema *gender balance* na sisi wote tunakuwepo tu na wakati fulani tunaandika Sheria watu wengine wanakuja wanasema sijui *chairperson* badala ya kusema *chairman* wanasema *chairperson* sasa mimi nawaambia ukisema *chairperson* ina maana inamu-*empower* huyu maana sasa *son* ndiyo atakayekuwa anakuwa tu hata Mwenyekiti sijui kama mnanielewa Waheshimiwa Wabunge. Yaani tunapokaa kufikiria na hasa wanaharakati wanasema pale imeandikwa *chairman* unasema *"man"* yule atakuwa mwanaume, sasa unasema tuandike *chaiperson* lakini ukisema *chaiperson* kila *son not a daughter* kila *son* ndiyo atakaekuwa ni Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uzuri kwenye Katiba yetu ni kwamba Ibara ya 13(5) imetambua umuhimu wa kuchukua hatua mahususi kwa ajili ya kurekebisha kasoro kwa kutoa upendeleo maalum mojawapo hata kwenye mambo

yanayohusu akinamama na wanawake ndivyo ilivyo. Sasa kwenye hili, hoja ya Mheshimiwa Ruth Mollel ni ya msingi lakini ukiangalia sasa Wajumbe wanaoletwa hpa huwezi kujua wanaotoka kule ni akina nani unaweza ukakuta wote ni wanawake watupu. Kwa hiyo, sisi hili tunaliona kama ni la kiutawala zaidi na mimi pale wananiletea Mawaziri majina ya kuomba kwamba fukani ateuliwe kwenye nafasi fulani na wanasema uchanganye wa *gender* zote mbili, mwanaume na mwanamke, kwa hiyo haya ni masuala ya kiutawala tumuachie Waziri akafanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama nilivyoshauri wakati nawasilisha muswada huo hapo, nilisema hivi, Muswada huu au mabadiliko haya msingi wake ni *harmonization* na jinsi ujumbe wa hizi *board* ulivyo kwenye mifuko mingine hasa ya Hifadhi za Jamii. Kwa hiyo tukija na hii ikataja tu pake yake tutakuwa tunatoka kwenye ile *scheme* ambayo iko kwenye ile mifuko mingine. Kwa mfano, sasa hawa waliotajwa hapa maana huwezi kujua kwamba watakuja mpaka sasa hatujajua watakuwa ni wanaume au ni wanawake tu, kwa hiyo ni mapema mno tumuachie Mheshimiwa Waziri na Waziri sijui kama anasikia na Waziri mwenyewe wa sasa nadhani ni mwanamke, kwa hiyo tumuachie Mheshimiwa Waziri atakuwa *so much sensitive* kuhakikisha kwamba napofanya maana kilio cha Wabunge kimesikika hapa vizuri lakini hataki kui-*compromise* na *scheme* nyingine ya uandishi wa sheria hizi za wajumbe kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo naomba Mheshimiwa Mollel alikuwa na nia njema na ina mwongozo ndani yake ya Katiba tuliachie hili kwenye taratibu za kiutawala. Naomba kushauri.

**MWENYKITI:** Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina sera ya fursa sawa na kama Serikali ina sera ya fursa sawa, Mheshimiwa *AG* anashindwaje tu kuweka tu hiki kipengele ambacho kitamfunga mamlaka ya uteuzi kuhakikisha

kwamba fursa sawa inatolewa kwa wanawake na kwa wanaume. Tunapoacha hivi hivi *open* kiutawala tu izingatiwe haitakuwa ni sawa kwa sababu na kuiweka kwenye sheria inamfunga huyu kiongozi aweze kuhakikisha ile bodi ina wanawake na wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo kuiacha hivi hivi *open ended* tu hatuna matumaini kama huyu kiongozi atakuwa ni *gender sensitive* au siyo *gender sensitive.* Kwa hiyo kama sisi tuna sera ya fursa sawa basi ijitokeze humu kwenye hizi sheria kama tulivyozipitisha. Ile tuliyopitisha juzi ya *TTCL* ilikuwa na *component* ya *gender* kwa nini hii isiwe na *component* ya *gender?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG.*

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Naomba kutoa hoja kama sikubaliwi, niungwe mkono.

**MWENYEKITI:** Nawapa watu wawili tu. Mheshimiwa Ridhiwani na huku Mheshimiwa Peter. Mheshimiwa Ridhiwani.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwanza kwa kuniona, lakini mimi binafsi yangu nasimama katika maana ya siyo naunga mkono hoja isipokuwa nataka nitoe maelezo yangu kidogo juu ya jambo hili hasa katika upande wa uandishi wa sheria. Sina uhakika sana kama mma yangu ni mwanasheria lakini katika uandishi wa sheria nchi hii au dunia nzima hakuna sheria inayoandikwa kwa kuzingatia *gender,* hilo la kwanza tuelewane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoweka kipengele chochote kile kwamba iwe kipengele hiki kimzungumzie mtu huyu awe mwanaume, ni tayari kuna watu umeshawatenga. Unaposema kuwa kipengele hiki kiwe mwanamke, maana yake kuna watu umeshawatenga. Kinachotakiwa ni busara ya wale wanaoteua, sio jambo la kuandika *gender. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana nchi yoyote duniani ambayo inaweza kutamka juu ya kabila, umri wa mtu,

urefu wa mtu, dini ya mtu wala jambo lingine lolote lile. Kwa hiyo, hili jambo nilitaka niliweke sawa ili tusichukue muda mrefu sana kubishana juu ya jambo la *specification* ya *gender.* Iandikwe hivyo na tuwaachie watu wenye mamlaka kama walivyopewa kwenye sheria waweze kufanya busara yao katika kuteua. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na hoja ya Mheshimiwa Mollel hapa, tutakuwa tunafanya makosa sana kama haturudi nyuma kwenye historia jinsi ambavyo mwanamke kwa muda mrefu ulimwenguni amefanyika kama object na ni wakati wa wanawake sasa hivi kuamka kuhakikisha mnatetea haki zenu ili tufikie kiwango kile cha 50/50 hata tunapotunga sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ku-*cement* hoja aliyoizungumza Mheshimiwa Mollel hapa ni ile sheria iliyokuwa inamlazimisha Rais katika Wabunge wa Kuteua Wabunge watano watano wa kike na wa kiume, tumeona muda uliopita Rais kwa namna moja au nyingine alikuwa ame-*over look.* Ni mpaka Wapinzani tulipopiga kelele ndio akarudia tena kuteua *gender* ziwe tofauti. Kwa hiyo, ni vizuri hii ikawa *specific* na akamuondoa mmoja alikuwa Bungeni mkampeleka Ujerumani kwa sababu ya sheria ilikuwa imeeleza *specific* kwamba lazima wanawake wawepo. Ni wakati wanawake kuiunga mkono hoja hii ili historia isirudie kwamba wanawake mmenyanyaswa. Ahsante sana.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutoagi taarifa wakati wa kuchangia hoja.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Basi ndio unapewa taarifa leo hapa. Anataka kutuyumbisha bwana. Hatuwezi kuyumbishwa, sisi tunatengeneza sheria za nchi. *(Kicheko)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Hujaruhusiwa, hata mimi nayengeneza sheria Ridhiwani.

**MWENYEKITI:** Naomba...

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Siyo namna hiyo Msigwa, acha.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Hapana natengeneza sheria hapa.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Hatuwezi kutunga sheria ambazo zipo *bias.* Huo sio utaratibu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge wote wawili naomba mkae. Mheshimiwa *AG* tuendelee.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumesoma sheria...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Manyanya ulikuwa unataka kuzungumza.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa aili ya muda sina haja ya kurejea kwenye vifungu, kwanza nilikuwa nataka kumwambia Bwana Msigwa si vyema kutumia vibaya kumtaja Mheshimiwa Rais kwa mambo ambayo siyo lazima afanye hivyo. Kwa mfano suala la kumwambia alimuondoa mtu, alimuondoa Mbunge aliyepita, mengine usipitilize. Kama mtu alijiuzuru mwenyewe uone tofauti hiyo. *(kicheko)*

Lakini la pili, kwa hali ya uelewa wa Watanzania sasa hivi kuhusiana na masuala ya jinsia, mimi sioni shaka kwa sheria hii hata kama ilivyo kwamba hatutafanya hiyo busara. *(Makofi)*

Kwa hiyo mimi nashauri suala hili halihitaji mjadala mkubwa kwa sababu Tanzania imekomaa mno katika masuala ya jinsia, na masuala ya wananwake na ndio maana

hata Makamu wa Rais wa Tanzania ni mwanamke na tunafahamu tofauti na mwanzo tulivyoanza. Kwa hiyo, tusifanye wema wa uongo, ingekuwa kweli wewe wema unaujua hata Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini angekuwa mwanamke. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu. Waheshimiwa Wabunge tumsikilize Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawashukuru Wabunge na namshukuru sana Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ametusaidia kuweka hili suala vizuri. *Scheme* ya waandishi wa sheria na tunayo sheria ya kwanza kabisa inaitwa Sheria ya Tafsiri ya Sheria *(The Interpretation of Laws Act, CAP.1)* yaani yenyewe ndio msingi wa tafsiri ya sheria zote na yenyewe ndio inaweka mwongozo wa kutafsiri Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya sheria hiyo *inasema he - person, pronouns. He including she. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kwenye sheria hapa inasema *he, he, he* sasa kwenye vifungu vyote itabidi twende tuseme *he, he, he* mbona wamesema *he* na wanawake wamo humu ndani? Haikusema *she. (Makofi)*

Kwa hiyo, hapo tunao mwongozo mahususi unaotuongoza kwenye kuandika...

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kushauri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruth Mollel naomba uhitimishe hoja yako.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasikitishwa sana kwa sababu akina mama tumetoka mbali,

na sisi wenyewe mimi nikiwepo Serikalinitukaweka sera ya fursa sawa kwa wote na tukaweka utaratibu katika sheria na kwenye bodi kuwepo na *percentage* ya wananwake, ilikuwa tunataja kabisa idadi ya wanawake *one-third shoud be women* kwenye sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimependekeza hapa *gender* kwamba inawezekana wanawake wakazidi basi wawepo wanaume na kama wanaume wamezidi wanawake wawepo na huwezi kuweka *discretion* kumpa binadamu *discretion. Discretion* ndio inatuletea matatizo ya upendeleo na uonevu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuipigie kura ili kesho na kesho kutwa mjue kwamba tulisema sisi na mmekataa kwamba kusiwe na *gender parity* katika sheria. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa nalihoji Bunge.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

*(Bunge Linarudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Sasa namkaribisha Mtoa Hoja aweze kuleta taarifa yake.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Tolea la Januari 2016 napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 4

wa mwaka 2017 yaani *The Written Laws Miscellaneous Ammendment No. 4 Bill of 2017* Ibara kwa Ibara pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 4 wa mwaka 2017 yaani *The Written Laws Miscellaneous Ammendment No. 4 Bill of 2017* kama ulivyorekebishwa na Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa *AG,* hoja imeungwa mkono. Sasa nitalihoji Bunge Zima.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*Hoja Iliamuliwa na Kukubaliwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsanteni sana, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 4 wa mwaka 2017 umepitishwa na Bunge hili ili kuwa sheria na sasa unasubirikupata kibali cha Mheshimiwa Rais upelekwe ili iweze kutumika kama sheria. Katibu.

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali zipatazo tano kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo *(A Bill for an Act to amment sertain written laws).***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, natumia fursa hii kuipongeza Serikali, kuanzia Mwanasheria Mkuu pamoja

na wadau wote walioshirikia kufanya marekebisho na kuchambua muswada huu wa sheria hadi leo hii na ninyi mkaweza kuupitisha. Nawatakia kila la heri Serikali yetu iweze kufuata sheria vizuri na kutekeleza yale ambayo tumepitisha.

Kunatangazo moja hapa kabla sijaahirisha Bunge. Ni kwamba leo siku ya Jumatano tarehe 15 Novemba, 2017 kutakuwa na Ibada ya Misa kwa wakristo wa madhehebu ya katoliki mara baada ya kuahirishwa Bunge katika ukumbi wa Pius Msekwa, ghorofa ya pili. Aidha Waheshimiwa Wabunge wote wanaopenda kushiriki katika ibada hiyo mnakaribishwa.

Baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 6:50 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 16 Novemba, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*